BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi**

			Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**

17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi**

				ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni
25.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara,**

				na Viwanda /Jimbo la Welezo
33.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**

52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**

74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem **-** **Katibu**

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 28 Mei, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Vijana, Utamaduni na Sanaa na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kibali chako na ridhaa yako kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mussa Foum Musaa (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka hati Mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2018/2019. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

MUONGOZO

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika**,** nikushukuru kwanza kwa kuniona lakini kubwa nimesimama kuomba muongozo wako wakati juzi Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aki-*windup* hoja yake, nilikuwa nimemsikiliza kwa makini sana, lakini niliwasilikiliza kwa makini sana Wahe. Mawaziri ambao walijumuisha hoja yao pamoja na Wahe. Wajumbe wa Baraza lako Tukufu ninaona Kamati yangu inakosa cha kuandika.

1. Kuwa waheshimiwa wanakwenda sana sera kuliko kwenda kwenye bajeti na vifungu vya bajeti na Wahe. Mawaziri wengi hawajibu hasa vile vifungu vya bajeti vinavyojadiliwa.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba muongozo wako juu hilo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mohamed Said Mohamed nikushukuru sana kwa hoja ambayo umeileta mbele yetu na nafikiri Mawaziri wamesikia na wamefahamu vizuri sana, kwamba hoja ambazo zinatolewa zinatakiwa zote zijibiwe zikiwemo za sera lakini zikiwemo na za vifungu vinavyohusika. Kwa hivyo nadhani hilo kama ikiwa kwamba halijazoweleka basi uwe ni

utaratibu niwaombe Mawaziri wakubaliane na utaratibu huo kwa kuzieleza hoja vile vile za bajeti ambazo zinatakiwa maelezo. Nafikiri nimeeleweka Waheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya mwaka 2018/2019. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa naomba watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali waje chini.

FUNGU KO1 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Kifungu K0112 Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu 104,095,000

Jumla Kuu

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilikuwa nimeulizia kushuka kwa pesa ambazo mwaka jana 2017/2018 tulitaka kuchangia shilingi 143,093,000 lakini mara hii zimeshuka kufikia shilingi 104,095,000. Sasa nataka kuhoji kujua kwa nini zimeshuka kiasi hichi *performance* mbaya au kuna kitu gani hata ikawa kimeweza kushuka.

Mhe. Waziri wa Elimu wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kushuka kwa pesa hapa ni kwamba mapato ambayo yameongezeka hapa ilikuwa ni kutokana na leseni za walimu na leseni za walimu tunakuwa tunafanya *review* kila baada ya miaka 5. Kwa hivyo, ina maana kwamba haitokuwa kwamba kila siku fedha zile zitakuwa zipo juu bali zitakuwa zinashuka kwa sababu ile ambavyo mwaka tulifanya zoezi hili kwa kwa nchi nzima, maan yake lilikuwa ni zoezi maalum la kuhakikisha kwamba kila mwalimu ana leseni yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo sasa hivi walimu tayari wana leseni, kwa maana mapato yatakayoyaengezeka sasa hivi ni wale walimu ambao watakuwa wapya wanaajiriwa na haitakuwa kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hivyo mapato yake hayatokuwa makubwa sana kama yalivyokuwa hapa. Ahsante sana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: tuendelee

Jumla Kuu **104,095,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU K01 – MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA PROGRAMU, PROGRAMU NDOGO NA HUDUMA.

Fungu PK0101 – Elimu na Maandalizi na Msingi

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilishauri suala la skuli za maandalizi kuona kwamba hawa wenzetu wanatoa mchango mkubwa kwa serikali na sera inakubali. Lakini sijaona kwamba wana nia gani serikali kwamba kuona nao wanapata ruzuku angalau, kwa sababu tumeshaanza *pre-primary* tumeshaanza *secondary*. Je, hawa upande wa skuli za maandalizi za jamii na sio zile za waeekezaji za jamii ambazo kuwa hawana chochote. Wizara ya Elimu itatwambia nini angalau kuzifikiria kuweza kupata ruzuku, kama mwaka huu hawakuweka basi angalau mwakani wakaweza kuziangalia kuweza kupata ruzuku. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Elimu wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mhe. Shehe Hamad Mattar ametoa ushauri, ushauri wake umepokelewa. Lakini vile vile tukizingatia kwamba tayari tumeshagatua maandalizi na msingi. Kwa hivyo tunaamini kwamba ambako imekwenda katika Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tunaamini kwamba kwa uwezo wa Wizara ya Tawala nao watalizingatia suala hili lakini kwa pamoja kwa kushirikiana baina ya sisi Wizar ya Elimu na Maandalizi ya Msingi na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ basi suala hili tutalitizama vizuri sana. Ahsante sana.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Ali Khamis Bakar:Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana namimi kwa kuniona kuweza kunipa nafasi kuweza kuuliza swali, wakati nikichangia niliuliza hapa:-

(a) Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimekosa walimu wa maandalizi na wakati akijibu hoja Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, sikumsikia kuniambia kwamba kwa awamu iliyopita Wilaya ya Micheweni tulipata walimu wangapi. Lakini vile vile kwa *quarter* hii vile vile sijasikia akisema kwamba walimu wangapi tutapata. Kwa hivyo naomba majibu nina maswali mawili hapa Mhe. Mwenyekiti.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia vile vile kwenye suala zima la elimu ya watu wanaosaidia katika masuala ya vyuo vya Qur-an, hapa vile vile niliuliza katika Wilaya ya Micheweni nilitaka kujua ni walimu wangapi hawa wanaolipwa katika hizo madrasa za Qur-ani lakini vile vile kwa mara hii katika hizo fedha ambazo zimetengwa Wilaya ya Micheweni tutapata walimu wangapi au watalipwa walimu wangapi katika hilo fungu ambalo Mhe. Waziri aliliwasilisha.

Mhe. Waziri wa Elimu wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimshukuru sana Mhe. Ali Khamis Bakar. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba

kwa upande wa Wilaya ya Micheweni kwamba katika zoezi la ajira lililopita tulipeleka walimu 37 na kwa vile bado mchakato unaendelea. Kwa hivyo ina maana inategemea na upatikanaji wa walimu kwa sasa kama ambavyo serikali itaweza kuajiri idadi ya walimu wangapi. Kwa hivyo namna tutakavyokuwa tunapata walimu wengi tutakuwa tunaangalia zaidi yale maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa walimu hao na ndio tutaweza kuwasambaza.

Mhe. Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba suala la walimu wa madrasa nadhani tulieleza kwamba sisi wizara yetu hailipi walimu wa madrasa mishahara ya aina yoyote. Kwa hivyo sisi tunachokifanya ni kusaidia katika kuwasaidia kuwasomesha ile *methodology* tu ya kusomesha ili walimu wale nao waweze kusomesha vizuri wale watoto wetu ambao wako kule. Kwa hivyo suala hili ni kwamba serikali imelipokea nayo na italiangalia kwa upana wake, lakini kwa mpaka sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hailipi mishahara kwa walimu wa madrasa, sisi tunasaidia kutoa elimu ya mitaala masuala mengine yote yako kama kawaida katika Ofisi ya Mufti. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar:Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nashukuru sana kwa kusema kwamba ametupatia walimu 37, lakini Wilaya Micheweni labda nimsomee hapa, kwamba Skuli ya Sekondari Micheweni walimu 12, Skuli ya Tumbe walimu 9, Skuli ya Kinowe walimu 7, Skuli ya Shumba Viamboni walimu 8, Skuli ya Wingwi Njuguni walimu 9.

Mhe. Mwenyekiti, hawa ni walimu wote ambao wanahitajika kwa msingi na sekondari lakini katika mara hii nimemuuliza walimu wangapi tutapa na tukizingatia kwamba katika *quarter* iliyopita kuna wastaafu wengi na bado kilio hichi Wilaya ya Micheweni ni kikubwa, pale Sinzini tu pana madarasa 15 na walimu 15 kiasi mbacho kila mwalimu mmoja ana zaidi ya vipindi 38 mpaka 40 na kuendelea. Sasa nilikuwa nataka kujua tu kwa *quarter* hii ambayo tunakwenda nayo. Je, atatuongeza walimu wangapi Wilaya ya Mcheweni bado kero yetu ni kubwa.

Mhe. Waziri wa Elimu wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar ambaye makini sana na nitaendelea kumjibu hivyo hivyo kwamba itategemea na idadi ya walimu ambao wataajiriwa, kwa sababu sasa hivi kumwambia walimu wangapi watapatikana katika wilaya yake wakati bado hawajaajiriwa itakuwa ni uongo na Baraza hili, kama tunavyosema Baraza Tukufu hatuzungumzi uongo. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Ali Khamis Bakari kwamba tuombe sana Inshaallah serikali mapato yawe mazuri sana iweze kuajiri walimu wengi, tukiajiri walimu wengi zaidi maana kila sehemu ambako kuna matatizo tunaweza kupata walimu wengi zaidi. Ahsante sana Mhe. Manyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kuwa kishasema kwamba ataangalia nitakuja msokota au tutakujaambizana huko mbele. Mhe. Mwenyekiti, acha nione utendaji wake Mhe. Waziri utakuwaje hapo mbele. Ahsante sana na tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa nachangia nilikwenda katika elimu ya maandalizi suala zima la tutu. Nilimuuliza Mhe. Waziri wa Elimu ya Mafunzo ya Amali kwamba haioni kwamba wizara yake inapoteza fedha bila ya msingi maalum kwa

sababu kile kipindi walengwa wakuu ni wale watoto wa chekechea ambao wanaweza kujifunza, kwa sababu tucheze tujifunze lakini wakati ule ambacho kipindi kile kinacholetwa katika redio zetu wanakuwa wale wako katika maskuli ndio wako kule walikolengwa. Je, kuna utaratibu gani wa kubalisha kuondoka pale kwenda katika muda mwengine *atleast* ile faidi ikapatikana kwa wale atoto waliokusudiwa. Hili Mhe. Waziri hakunijibu naomba maelezo yake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba suala la watoto kipindi kinacholetwa na *ZBC Radio* "Tucheze Tujifunze". Kile kipindi ni maalum kwa ajili ya watoto ambao wako katika vituo kwa muda ule, si kwa ajili ya watu wazima. Sasa muda ule ambao kipindi kinarushwa watoto wale wamo katika vituo vyao wanapata masomo. Kwa hivyo ni muda muafaka kwa watoto wale kuweza kusikiliza na kujifunza ndani ya vituo husika. Watu wazima kwa bahati mbaya wanasikiliza kwa sababu nao wako majumbani ni vizuri nao kusikiliza kuweza kuwasaidia watoto wao ambao hawako ndani ya vituo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, muda uliopo ni muda muafaka sana kwa sababu saa mbili na nusu watoto wale wako ndani ya vituo vyao wanapatiwa masomo yao. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana naipongeza hiyo, lakini angenambia vituo vingapi vina redio ya kusikiliza matango yale wakati wako vituoni.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri anataka idadi ya redio zilikuwemo ndani ya skuli za maandalizi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu vituo vyetu ni vingi sana lakini nimesema kuna vituo vyote vya tutu vina redio ambavyo wanasikiliza. Ahsante sana. Labda kama ana wasiwasi nimuombe sana kwa sababu mjini hakuna kituo katika jimbo lake, lakini nimuombe sana aende katika Wilaya ya Kaskazini 'B', vituo hivi vipo vingi sana na atakapokwenda kule ataweza kuona katika huo muda ambao nimemwambia, atakuta watoto wote wako vituoni na wanapata mafunzo kupitia hiyo redio na redio zipo. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Tuendelee.

Jumla ya Programu Kuu ni shilingi 10,882,100,000/-

FUNGU PK 0102 - PROGRAMU KUU YA ELIMU SEKONDARI

Jumla ya Programu Kuu hii ni shilingi 95,587,055,000/-

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilitaja Skuli ya Mtule ya Sekondari, skuli ambayo imejengwa si muda mrefu. Wananchi walionituma wa Jimbo la Paje na skuli hiyo ipo katika jimbo la Paje ni kwamba sasa hivi kumewekwa matangi ya lami badala ya kuzibwa viraka mule ndani ili maji yaingie mule ndani. Nataka kuambiwa skuli hiyo lini itafanyiwa ukarabati kutokana na hali ambayo si rafiki. Mvua yote mule ndani mmewekwa madishi na mabeseni makubwa wakati mwengine hata yale matangi makubwa hukingwa maji ya mvua. Nataka kujua lini itafanyiwa ukarabati na nisije nikaambiwa muda mrefu. Niiombe sana

wizara na wizara hii niishukuru Waziri na Naibu Waziri walikuwa walimu tunawashukuru sana wanaujua umuhimu wa elimu na ni moja ya jimboni kwangu inakotokea hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mwalimu siku zote atabaki kuwa mwalimu hata kama atakuwa anafanya kazi nyegine, kama alivyokuwa Mwalimu Nyerere.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo kama haya ambayo ameelezea tunayafahmu na yako mengi lakini tunayashughulikia. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kauli ya Mhe. Waziri haikuniridhisha niseme kweli, kushughulikia atashughulikia lakini yako mengi na kila mmoja analia mama yake. Mimi ni mtumishi wa wananchi wa jimbo la Paje skuli hairidhishi hata kidogo na nafikiri hajenda hata kuiangalia. Naibu Waziri nafikiri alikwenda kuiangalia hali hairidhishi na moja katika skuli zilizoshika mkia au ndio ya mwisho ndio hiyo na mimi nikahojiwa na pengine si makosa ya walimu, pengine makosa ya wizara, mazingira sio mazuri kutokusoma, mazingira sio rafiki kuna hatari ya kuja kufeli tena. Unajua elimu kitu kizuri nacho kinasaidia. Kwa hivyo ananambia atafanya, atafanya lini. Nataka anipe muda tumpitishie bajeti yake vyenginevyo Wajumbe nitawaomba wanisaidie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu anataka kujua muda gani mtatumia katika kurekebisha tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, suala la ukarabati kama tunavyosema kwamba kila siku tunaambiwa hapa kuwa majengo ya *maintenance* yanajengwa, mana si suala la kwamba ukishakutengeneza leo halafu ikawa basi ni suala endelevu na kama nilivyomwambia kwamba tumelipokea tutakwenda kukagua skuli yake tutaangalia na gharama ambazo zitakuwa zinahitajika wakati ambapo hali yetu itakuwa inaturuhusu. Kwa sababu kumwambia kwamba kesho au keshokutwa ndio yale tunayozungumza kuwa tusidanganye kwa Mwenyezi Mungu ilhali tuko katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Sote au wengi wetu humu tuna saumu naamini kama si sote, kwa hivyo tusidanganyane tukasema kwamba kesho lakini nimwambie kwamba namuomba sana atuamini kwamba tutatekeleza. Kwa sababu kama kawaida Ilani ya Chama cha Mapinduzi inapoahidi inatekeleza. Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa awe na imani na hilo. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe sana Waziri, hii hali hairidhishi nisije nikamuuzia mbuzi kwenye gunia, twende *physically* akaone ile hali watoto hawawezi kusoma hata kidogo. Skuli yote, nakwambia pamewekwa ndoo, madishi kwa kukinga yale maji, sasa hata skuli yenyewe imefanya vibaya katika mtihani huu ndio iliyoshika mkia Tanzania na pengine si makosa yao wanafunzi labda wizara pengine, katika mazingira yale mtu hawezi kusoma, huwezi kulala wakati nyumba inavuja. Sasa ananambia haya ndio majibu ya serikali tumo mbioni, kesho, keshokutwa, anambie tu muda miezi miwili, mwaka, sio tatizo naweza kutafuta njia gani ya ku-*solve* hili tatizo, naweza nikaziba hata viraka kama soko la Darajani lilivyo, anambie tu kama hali itaendelea miezi sita tuna Mfuko wa Jimbo tushukuru, aniambie tu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana narudia tena maneno kwamba ujenzi ama kukarabati majengo ni suala endelevu, tutatembelea kama tulivyoweza kutengeneza nyumba ya walimu ndani ya jimbo lake; alisema hapa naamini sasa hivi kafurahi sana juu ya suala lile. Kwa hivyo ndio na hilo namwambia kwamba tunapoahidi tunatekeleza hiyo ndio sera ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo nimuombe sana kwamba na hili nalo kwa sababu wanaosoma pale ni vijana wa Kizanzibari, ni vijana wetu, ni vijana wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tutalishughulikia kwa namna ambayo kama nilivyoeleza awali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kushughulika anaweza kushughulika leo, kesho...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim nafikiri Mhe. Waziri ameelezea vizuri sana, anasema kwamba suala la matengenezo ni suala endelevu. Kwa hivyo ana hakika yeye kwamba katika kipindi chochote watalishughulikia hili. Sasa muda anasema hataki kuutaja kwa sababu hana hakika inategemea mfuko, inategemea mambo mengi pamoja na huo mfuko. Sasa naona utuachie tuendelee kwa sababu tayari ameshaahidi Mheshimiwa na wewe tumekuomba ulifuatilie suala hili kwa makini sana. Kwa sababu ni kweli watoto wanateseka na inakuwa ngumu sana kuweza kuendelea kusoma vizuri. Kwa hivyo naomba ulisimamie hili kama Mwakilishi wa jimbo lako. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii, pia namshukuru sana Mhe. Waziri alivyojitahidi kutoa ufafanuzi mengi tumemuelewa. Hoja yangu niliunga mkono hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed ya kutaka kwamba Baraza lako liunde Kamati Teule ili kwenda kuyapitia yale majengo yote ambayo yamejengwa na serikali ambayo mengi yao hayako katika kiwango na majengo ambayo yanavuja, ambapo hata Mhe. Waziri ameonesha kusikitika na yeye kwamba majengo yale hayamridhishi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tulipendekeza kwamba hawa wakandarasi walioharibu majengo haya bado serikali inaendelea kuwapa kazi hao hao. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba ile kauli ambayo Mhe. Mohamed Said aliomba kuundwa Kamati Teule Mhe. Waziri hakuwahi kuitolea ufafanuzi. Kwa hivyo nilikuwa naomba utaratibu uendelee. Hoja ya Mhe. Mohamed Said nafikiri alitaja kile kifungu naona huu ndio wakati wa kufanyiwa kazi. Kwa hivyo nitaomba Mhe. Mwenyekiti, urudi kwenye kiti chako tuahirishe Kamati ya Matumizi ili sasa uwaulize Wajumbe ambao watakubaliana na kuunda Kamati Teule ya kwenda kuyaangalia majengo mabovu halafu kuja na mapendekezo ambayo yataisaidia serikali.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma lakini acha tufuate utaratibu kwanza wa Mhe. Waziri kujibu halafu baadae ndio tutarudi kama kukiwa na haja ya kuunda hiyo Kamati Teule basi tutarudi kwa ajili ya kupiga kura. Naomba Waziri ajibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muongozo wako mzuri. Mheshimiwa ni kwamba tunapozungumzia majengo skuli ni miongoni mwa majengo ya serikali lakini serikali ina majengo mengi sana zikiwemo skuli na majengo mengineyo.

Majengo haya kweli kwamba yapo ambayo yana matatizo, tumekubali na tumeeleza katika majibu yetu katika ufafanuzi kwamba kweli yana matatizo. Lakini sisi binafsi Wizara tumeunda Kamati Maalum kuyapitia majengo haya na kama ambavyo anazungumzia labda majengo yale 19 basi Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tuliunda Kamati binafsi yangu wizarani kwa kushirikiana na viongozi wenzangu kupitia kuona nini tatizo. Lakini vile vile kwa kupitia wataalamu wataishauri nini serikali ifanye na ripoti bahati nzuri sana ipo tayari ya Kamati ambayo tumeiunda labda Mhe. Mwenyekiti ni kwamba ninayo hii kabrasha ambayo niko nayo mbele yangu. Hii ni ripoti ya kamati ambayo tumeiunda sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu majengo ambayo yanavuja.

Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa kwamba sisi serikali ni kwamba tunajitahidi sana kuona ubora wa majengo yetu yanakuwa vizuri na pale ambapo yanatokezea matatizo kuona nini tunafanya ili kuweza kurekebisha hali hiyo. Kwa hivyo baada ya kuona hali hiyo na hatua ambayo tumeweza kuifanya na kwa sababu ripoti hii bahati nzuri tumeipata ile siku ya Jumamosi. Hivyo tutaifanyia kazi kuona ushauri wa wataalamu wametushauri nini tufanye ili kuona matatizo kama haya hayatokezei tena kwa siku za mbele.

Nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi na Wawakilishi wote ambao kweli hili wameliona, sote tumeliona lakini tunakubali kwamba ni kweli baadhi ya majengo ya skuli yanavuja. Tukiachia hayo tu ambayo yamejengwa skuli 19 lakini hata yale mengine ambayo ni ya zamani kwa kweli yamechakaa na tunakubali kwamba jengo ambalo limejengwa miaka 1960 halitokuwa sawa na jengo ambalo limejengwa leo hii. Kwa hivyo majengo haya yanavuja kutokana na mengine ni machakavu, lakini kwa yale ambayo anayazungumzia 19 tayari tumeunda Kamati na ripoti ya Kamati Mhe. Mwenyekiti, ni hii hapa na kama utaniruhusu basi pia nitaweza kuwasilisha katika meza yako.

Lakini kwa sababu bado haijafuata taratibu nyengine, kwa sababu tumeipata lakini kama wajibu wa serikali ulivyo tuiwasilishe serikalini, lakini ripoti ni hii hapa nashukuru sana ahsante. Kwa hivyo kwa msingi huo Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwamba hakuna haja ya kuunda Kamati hii na turidhike na tukubali tuiamini serikali kutokana na kamati ambayo tuliiunda. Niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu tukubaliane na serikali yetu na tuiamini ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tunaiamini sana serikali yetu na hata wananchi wanaiamini sana **s**erikali yetu ndio maana wakawa wanaendelea kutupigia kura ili tuwasimamie haki zao.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wizara ndio iliyoharibu, wizara hiyo hiyo ndio iliyounda Kamati ya kujiangalia walivyoharibu. Mhe. Mwenyekiti, majengo tunaanza kwa Wizara ya Elimu lakini sio Wizara ya Elimu peke yake yapo na mengine. Hiyo ripoti ambayo waliounda Kamati Mhe.

Waziri hiyo ni yake mwenyewe, tumuache aendelee na taratibu zake lakini na sisi hapa Barazani tuna utaratibu wetu, Kanuni zetu zinaturuhusu kuunda Kamati Teule. (*Makofi*).

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri majibu yake nimeshayasikia lakini bado sijaridhika. Naomba Mhe. Mwenyekiti, urudi kwenye kiti chako ili sasa tupige kura kuunda Kamati Teule na nitaomba Mhe. Mwenyekiti, Kamati utakayounda leo sio kwamba itakuja kuangalia tu majengo ya Wizara ya Elimu kwa sababu bado tunakwenda kwenye Wizara ya Afya hatujafika. Kwa hivyo Kamati hiyo itakuja kuchukua maeneo tofauti na utaratibu wetu Mhe. Mwenyekiti, kwa uzoefu Kamati si lazima iundwe leo. Baraza litakaa litasikiliza mijadala yetu kama itakuwa kuna haja na mambo mengine kuyaongezea kwenye Kamati hiyo mtakuja kuikabidhi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali ya majengo mapya yanavuja haturidhiki lazima tumtafute mchawi tushachoka, pesa za serikali wafadhili wanalalamika wanatukopesha pesa matokeo yake miradi inakuwa mibovu.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya Baraza la Wawakilishi kuisimamia serikali, zaidi kuwasimamia wale watendaji ambao wabovu ambao wanaitia hasara serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba urudi kwenye kiti chako ili sasa uwahoji Wajumbe tupige kura kwa ajili ya kuunda Kamati Teule.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Elimu kwa maelezo yake ya kina.

Aidha nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Mwenyekiti, kama linavyomuuma Mhe. Hamza ndivyo linavyowauma Wizara ya Elimu na ndivyo linavyowauma serikali nzima. Ni kweli majengo yale 19 ya Skuli za Sekondari mengi yake yanavuja na hali ile sio nzuri na ndio maana Mhe. Waziri wa Elimu alichukua hatua ya kuunda Kamati kwa msingi wa kutaka kuelewa kwa kina tatizo lililojitokeza. Kwa bahati nzuri hata Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Ustawi wa Jamii ambayo inasimamia na wizara hii ilipata maelezo kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hasa ukilitizama kwa undani halitokani na wakandarasi, tatizo limeanza mbali kidogo, limeanza kutokana na *design* na hii inatokana na mshauri mwelekezi ambaye ndio *consultant.* Yete ndiye aliyefanya ile kazi ku-*design* namna ya ujenzi. Kwa bahati mbaya au nzuri baada ya kuletewa *client* ambao ni Wizara ya Elimu na hata wewe Mheshimiwa ungeiona hiyo *design* pale kwenye hatua za awali ungeridhika nayo sana.

Sasa kwa sababu mara nyingi *client* ambao ni Wizara ya Elimu matumaini yake makubwa ni huyu *consultant,* baada ya kuleta *design* ile na hata hawa *financer* wetu *World Bank* nao waliridhika na ile bidhaa. Sasa tatizo lilianza wakati wakandarasi wapo kwenye *site* wanaendelea na kazi, ndipo hali ilipoanza kujitokeza. Wakandarasi walianza kushauri kwamba tukiendelea kujenga kwa *design* hii upo wasiwasi wa kuja kuvuja kwa majengo.

Lakini mshauri alikuwa na *confidence* kubwa kwamba *design* yake ipo nzuri na aliitetea sana. Kwa hivyo wakandarasi waliendelea na ujenzi kwa kufuata ushauri wa mshauri kwa maana ya *consultant*. Kwa hivyo ilipotokea kuvuja ndio Wizara ikachukua hatua ya kuandika hiyo ripoti. Dhamira yake ni kujua kwa kina kosa litakuwa kwa nani. Kwa mshauri au kwa wakandarasi, ili serikali iweze kuchukua hatua zinazofaa.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Hamza Hassan Juma akubaliane na maelezo ya Wizara kwamba tuijadili ndani ya serikali ripoti kama ilivyo na baadae ripoti hii hii tuiwasilishe hapa Barazani kabla ya kumalizika kwa Baraza hili la Bajeti.

Baada ya hapo ndio tuchukue hizo hatua nyengine kama hawakuridhika Wajumbe, tuchukue hatua nyengine za kuunda Kamati Teule. Lakini kwa sasa naamini kutokana na ripoti hii ikishakupitiwa na mapendekezo watakayotoa serikali itarahisisha kazi ya Wajumbe wenyewe na pia naamini kwa kiasi kikubwa Wajumbe wataweza kuridhika na hiyo taarifa iliyopo.

Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Hamza Hassan Juma na Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane tupitishe Wizara yetu ya Elimu, nae Waziri wa Elimu aiwasilishe ripoti hii serikalini ijadiliwe na baadae kabla ya kufungwa kwa Baraza tutafute siku nzima tuilete ripoti hii iwasilishwe na Waziri mhusika, tuje tuijadili hapa tuone. Naamini sana Mhe. Mwenyekiti, itakuwa imetusaidia na itakuwa imepunguza uzito wa Baraza lako kuunda Kamati Teule. Lakini kwa sasa tumuombe sana Mheshimiwa kutukubaliane na maelezo ya Mhe. Waziri.

Naomba kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Hamza Hassan Juma Mhe. Waziri amejenga hoja ya kutaka serikali iachiwe kuendelea kufanya utafiti wa hilo suala ambalo wewe umelijengea hoja. Sasa ameshauri Mhe. Waziri sasa sijui unasimama wapi?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nasimama hapa hapa. (*Makofi*)

Nilipokuwa nikichangia nilieleza vizuri ujenzi kama huu kunakuwa kuna watu watatu kuna *contractor* ujenzi, kuna *consultant* mshauri na kuna *client* serikali ndie mwenye mali. Leo Mhe. Mwenyekiti, majengo yetu haya yanaharibika kutokana na ukaidi sio kama ushauri ulikuwa hautoki mwanzo, ukaidi na kama wewe mtaalamu *consultant* kama *consultant* ina maana sisi wa kusokotana naye ni *consultant* kwa sababu serikali haiwezi kutoa fedha kama *consultant* haja-*issue certificate* kwamba mkandarasi katika hatua hii amefanya kazi vizuri. Kwa hiyo, ina maana huyu *consultant* ameipotosha serikali. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama serikali ilikubali kupotoshwa halafu waunde kamati wanakiangalia kitu gani. Mhe. Mwenyekiti, naomba sisi ndio Wawakilishi wa wananchi tunajua mengi na tunasikia mengi na tuna taarifa nyingi. Lakini tatizo letu Mhe. Mwenyekiti, wakati wa vikao vya kawaida hatuwezi tukaleta hoja. Sisi tunaweza kuisimamia serikali mwaka mmoja kwa kila mwaka, tunawaaachia ndani ya miezi kumi na moja wanaharibu hatuna pa kusema. (*Makofi*)

Naomba Mhe. Mwenyekiti, Ripoti itakayokuja ya Kamati Teule itaisaidia sana serikali. Mhe. Mwenyekiti, hao waliounda kamati ndio hao hao walioharibu. Sisi hatuwezi tukaridhika. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tusipoteze muda katika hili. Nilieleza toka siku ya mwanzo Mheshimiwa leo kuna majengo sasa hivi yanafika miaka kumi hayajesha, kwa sababu ndio hao hao wanaharibu leo majengo mapya pia yameshaharibika. Mhe. Mwenyekiti, hatuzungumzii suala la kuvuja tu majengo hata ubora hayana. (*Makofi*)

Leo Skuli mpya zina nyufa kibao Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, Mhe. Hamza Hassan Juma anajaribu kujenga hoja sasa nyie mnapogonga hivyo hasikilikani naona mwachieni.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Enh naomba nipeni raha ili Mhe. Mwenyekiti aridhike.

Mhe. Mwenyekiti: Hatumsikii huku mie sisikii. Sasa nitashindwa kutoa maamuzi mazuri. Kwa hiyo, naomba mumuachie anachokizungumza nafikiri tumeshafahamu kwamba hakubaliani na serikali kwamba wao waachiwe kuendelea kufanya utaratibu ambao sasa hivi wanaufanya na serikali sijui inataka kusema la ziada.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sisi tunamshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma na anachokisema ndicho kwa kiasi kikubwa tunazungumza lugha moja ni tafauti ya tafsiri tu. Kwa sababu Mheshimiwa na wizara imepokea ripoti ambayo naamini kabisa kama Mhe. Hamza Hassan Juma ageiona kwa kiasi kibwa angekubaliana na haya ninayosema mimi.

Mimi nimuombe tu atupe muda kidogo hatujakataa ombi lake. Lakini kuna ripoti ambayo ina maelezo mazuri sana ambayo yakija serikalini yataongezewa na ziada na maelekezo ya serikali tukayaleta hapa kwenye Baraza Tukufu hili na kama Waheshimiwa watahisi bado hawajaridhika basi watafanya maamuzi hayo Mhe. Hamza Hassan Juma anayoyasema.

Sie tunamuomba kwa leo atupe muda kidogo tukaifanyie kazi hii taarifa itazidi kumpa *input* za ziada ambazo kama atakuwa na kauli yake hii baada ya kuja ripoti hiyo basi itakuwa imemsaidia zaidi.

Lakini naamini baada ya ripoti hiyo hilo lengo ambalo yeye analikusudia litokee ndani ya ripoti litakuwemo imefanywa kazi nzuri.

Mimi namuomba sana Mhe. Hamza Hassan Juma atupe muda tuianyie kazi tuilete ripoti hapa tuitafute siku nzima na baada ya kuiona hiyo ripoti tumsikie sasa atakuwa na uamuzi gani.

Sie tunamuomba kwa heshima zote Mhe. Hamza Hassan Juma na Baraza lako Tukufu na Wajumbe wote kwa dhamira njema kabisa ili sote tunajenga nyumba moja msingi wake si kuharibu pesa za umma, msingi wake turekebishe palipokosewa na mambo yaendee vizuri nakubalibaliana nae anachokisema anasema maneno ya msingi sana. Lakini tumuombe atustahamilie ili baadae Mhe. Hamza Hassan Juma tuje na ripoti halafu mfanyie uamuzi wa kwa

pamoja baada ya kuja na ripoti hii. Tunaomba kwa heshima kubwa sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Haku Hashim Ayoub ngoja tumalize hili halafu utakuja na utaratibu wako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ndio hili hili kuliweka sawa tu Mhe. Mwenyekiti, kama utataka ushauri.

Mhe. Mwenyekiti: Aaah! Mwenye hoja ni Mhe. Hamza Hassan Juma. Kwa hiyo tumuachie Mhe. Hamza Hassan Juma aendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma ni ombi serikali imeomba kwamba hili wanalishughulikia tusubiri muda si mrefu watakuja na ripoti ambayo itaweza sasa kukuridhisha wewe kwamba serikali imeweza kulishughulikia hilo tatizo.

Sasa Mhe. Hamza Hassan Juma nakupa mara ya mwisho najua maamuzi yangu yatakuwa nini. Baada ya hapo nakupa mara ya mwisho ukubali ombi hilo au kama una jengine basi utwambie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ni aibu kubwa kwa Mjumbe ambaye anajua kazi yake kuruhusu matumizi halafu matumizi yale yanakwenda kutumika chini ya kiwango. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa bahati nzuri niliwahi kupata mafunzo ya *PAC*. *PAC* kazi yake kuikamata serikali wanapofanya matumizi vibaya. Mhe. Mwenyekiti, jengo sio moja leo tukisema tuiachie serikali mimi naanza tena Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaisimamia serikali mwaka mmoja kwa mwezi mmoja katika vikao vyote. Hatuwezi tukaja na hoja hapa sijui tuunde Kamati Teule, wakati pekee ni wakati wa bajeti. Leo Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi bado majengo yanaendelea tutaendelea kuharibikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tena serikali tunakukubalieni mambo mengi hili tuachieni kwa maslahi yenu. Kwanza nashukuru serikali wamekiri kwamba kweli majengo mengi ni mabovu. Mhe. Mwenyekiti, kwa Mkandarasi aliekuwa makini hawezi akajenga jipya likawa linavuja wanafunzi wanahamishwa skuli zinaekwa ndoo kwa ajili ya kukinga maji.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema sizungumzii suala la majengo kuvuja tu lakini hata *ratio* ya ujenzi *quality* ya majengo mabovu, majengo yameshaanza kufanya nyufa, majengo yanapukutika mapema. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nyumba zile pale za Michenzani leo mwaka wa ngapi hakuna ufaa, hakuna nini. Leo majengo juzi Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi naomba tuende kwenye kura. Sasa hivi

naomba sana serikali nimeshasikia maneno yao sijaridhika nayo naomba twende kwenye kura kama Wajumbe wataridhika pesa za umma zitumike vibaya basi hakuna tatizo mimi nitabakia peke yangu. (*Makofi*)

Naomba Mhe. Mwenyekiti, khairisha kamati rudi kwenye kiti chako vaa joho ili tupige kura. Ahsante Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante narudi.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na shughuli yetu sasa ambayo imenileta hapa kwenye kiti naomba nipate muda mchache kabisa niwatambulishe wageni wetu wakati tunatafakari haya ambayo tutakuja kuyafanya. Tuwakaribishe wageni wetu.

Waheshimiwa Wajumbe wageni wetu leo tarehe 28/05/2018 ni wageni wa Mhe. Suleiman Sarahan, wageni wa Mhe. Waziri, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Balozi Ali Karume. Wageni wenyewe ni kama hawa wafuatao.

Watendaji wakuu wa Baraza la Vijana pamoja na wenyeviti wa Mabaraza ya Vijana ya Wilaya jumla yao ni 12 wanaongoza na ndugu Catherine Pascal Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Taifa. Wengine ni Wasanii wa Kikundi cha Taifa cha Taraab jumla yao ni 15 wanaongozwa na Msanii wetu ndugu Taomur Ruku Ntaha. Wengine ni kikundi cha Sanaa za ngoma jumla yao ni 7 wanaongozwa na ndugu Asha Khatib Hassan.

Wengine ni Wajumbe wa Maigizo na filamu jumla yao ni 12 wanaongozwa na ndugu Salum Maulid Salum Stika.

Wengine ni Chama cha Wasanii wa Mziki wa Kizazi kipya Zanzibar jumla yao ni 10 wanaongozwa na ndugu Mohamed Abdalla. Wengine ni kutoka Sekta ya Michezo jumla yao ni 11 wanaongozwa na ndugu Mohamed Ali Hilal.

Wapo wangeni wengine wa Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Mwakilishi wa Viti Maalum kutoka Kusini Unguja nao ni Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kusini, ndugu Alawi Haidar Katibu UVCCM Mkoa wa Kusini ndugu Zaituni Khatib Vuai Mwenyekiti UVCCM Wilaya ya Kusini ndugu Said Hassan Mwenyekiti UVCCM Wilaya ya Kati na ndugu Ame Abdalla Ame Katibu UVCCM Wilaya ya Kusini. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe nafikiri tumefika sasa hatua nzuri ambayo kwa mujibu wa kanuni zetu kwamba tunapofikia maamuzi ya kwamba kanuni ya 111 ambayo imetupa uwezo wa kuweza kuunda kama Baraza la Wawakilishi kuunda Kamati Teule linalofuata ni upigaji wa kura. (*Makofi*)

Waheshimiwa tumesikia hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma lakini sasa nimuombe ailete hoja yake vizuri kutaka sasa tuipigie kura Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kuwa mueledi kwenye kiti chako. Lakini vile vile kuwa msikivu kwa hoja ambazo zinazokuwa za msingi zinaletwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Lakini pia naishukuru sana serikali kwa kukiri kwamba kweli miongoni mwa majengo ambayo tuliyojengewa ni mabovu na hayana kiwango. Sasa najua kuna suala zima la *collective responsibility* lakini naamini serikali katika hili wataunga mkono hoja yangu ya kuunda Kamati Teule. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba kutumia kanunia ya 111 (i) ya Baraza la Wawakilishi ili tuweze kupiga kura kwa ajili ya kwenda kusimamia maslahi ya wananchi. Mhe. Naibu Spika, naamini siku zote serikali wanatuomba wao na leo nimesimama hapa kwa niaba ya Wajumbe wa *back bencher* kuiomba serikali watuunge mkono katika suala zima la kwenda kukagua majengo haya na kuleta ripoti nzuri serikalini itakayoweza kuyasaidia ili tusijengewe tena majengo yaliokuwa chini ya kiwango. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa toa hoja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja ya kuunda Kamati Teule wanyooshe mikono. Mkono ni mmoja mmoja Waheshimiwa sio miwili, wale wanaokataa, Waheshimiwa wanaokubali hoja wamashinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe kutokana na idadi ya kura ambao wengi wao wamesema kwamba wanataka Kamati Teule iundwe ina maana kwamba Kamati Teule. Waheshimiwa naomba tusikilizane.

Waheshimiwa nina jambo muhimu nataka kulizungumza hamnipi nafasi mnazungumza nyie naomba tisikilizane.

Nasema kutokana na idadi ya kura ambazo inaonesha dhahiri kwamba wengi wao wa Wajumbe wamekubali kuwa Kamati Teule iundwe maalum kwa ajili ya kushughulikia suala ambalo tumekuwa tukilizungumza suala la majengo ya Wizara ya Elimu.

Kwa maana hiyo kwamba basi Kamati hiyo, kiti kimekubali kamati hiyo iundwe kutokana na kura ambazo zilizokuwepo. Lakini sasa ningeomba sana kuhusiana na Wajumbe mnajua kanuni zetu Wajumbe wanakuwa si zaidi ya watano, kwa hiyo ningeomba suala hili la kutizama ni kina nani ambao watakuwemo ndani ya kamati hii basi tusubiri mpaka baada ya Mhe. Spika,

atakaporudi sasa tuunde hiyo kamati. Lakini kamati tumeshakubaliana hapa kwamba kamati hiyo itaundwa. (*Makofi*)

Nafikiri hilo ndilo muhimu sana akiwemo mwenyewe Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ametoa hoja yeye ni muhimu kuwemo ndani ya kamati hiyo ili aweze kusaidiana na wengine Wajumbe ambao watateuliwa na Mhe. Spika, kuweza kuwa pamoja na wengine. Mhe. Hamza Hassan Juma ulikuwa na jambo nakuona unasimama.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru na naishukuru sana serikali najua wameunga mkono kimnya kimnya kwa sababu ya *collective responsibility*. Mhe. Mwenyekiti, naona wenyewe hawataki sawa. Mhe. Naibu Spika, naomba kufuta hiyo kauli (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwanza nawashukuru sana Wajumbe kwa kuweza kutekeleza wajibu wao kama kanuni zetu zinavyotusa. Lakini hoja yangu pia niliunganisha Mhe. Naibu Spika, kwa sababu sio majengo tu ya Wizara ya Elimu ambayo yana hizo changamoto. Kwa hiyo, kwa uzoefu ambao kipindi cha nyuma tulikuwa tukitumia kwamba hii kamati isiharakishwe kuundwa kwa sababu hatujajua huko mbele kuna hoja nyengine zipi za majengo ambazo Wajumbe hawatoridhika nayo, kwa sababu vyenginevyo tunaweza tukaunda kamati nne tano kitu ambacho kitakuwa hakisaidii sana.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Spika, siingilii mamlaka ya kiti chako lakini naomba tunapokaribia kumaliza hili Baraza nafikiri utakuwa umeshapata muda mzuri na umeshasikiliza hoja nyingi za Wajumbe ili sasa wanapopewa hiyo kazi wasifanye kazi ikawa inarudiwa hiyo kwa hiyo. Hayo ilikuwa ni ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, na ushauri unaweza ukaukubali lakini vile vile unaweza ukaukataa. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma nimekuelewa vizuri sana na nafikiria hilo suala kama ulivyosema sema utakiachia kiti kitoe maamuzi. Kwa hiyo, ningekuomba kwamba kwa hili ambalo mwanzo tulikusudia kulifanya tayari tumeshalifanya hayo mengine yatahitaji burasa na wakati mwengine.

Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba lile la mwanzo ambalo tumelikuwa tumekusudia hususan kwa sababu tulikuwa tuna- *deal* na Wizara ya Elimu hatu-*deal* na wizara nyengine.

Kwa hiyo sasa hili jengine litataka tutafakari zaidi. Hivyo nikubali hayo ambayo umeyazungumza lakini tuachie tupe muda uongozi wa Baraza ufanye maamuzi ya hayo mengine ambayo umeyazunguma nakushkuru sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma asikizonge kiti chako, nadhani Mhe. Hamza asikizonge kiti. Hoja yake ilikuwa moja, nayo Wajumbe wamemkubalia ya kuunda ya Kamati Teule kwa sababu maalum kama ambavyo Kanuni inasema na sababu wenyewe maalum ni majengo ya Wizara ya Elimu na Wajumbe wamekubaliana naye.

Sasa hii nyengine ambayo anachomekea, hiyo haikuwa katika hoja ya mwanzo. Mimi nadhani Baraza halitakiwa hata kulizingatia baadae, hoja yake ni moja ambayo imeshakubaliwa iundwe hiyo Kamati Teule ikafanye kazi, hayo mengine aje kujayasema baadae na asichomkee kwenye hoja ambayo ameruhusiwa na Baraza.(*Makofi*)

Mhe.Naibu Spika: ahsante Mwanasheria Mkuu tuendelee katibu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Muongozo wa Spika

Mhe.Naibu Spika: Mhe. tumemaliza hili, hili tumemaliza

MUONGOZO

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika jengine Mhe. Mwanasheria Mkuu wakati anasimima, sijui alisimama kwa Kanuni gani na utaratibu upi, amesimama akikuelekeza jambo ambalo hakutaja Kanuni wala kifungu chochote cha sheria. Kwa hivyo kusimama kwake kutakuwa batili hapo.(*Makofi*)

KAMATI YA MATUMIZI

Kifungu PK0102 Elimu ya Sekondari	Programu Kuu ya	95,587,550,000

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nimezungumzia kuhusiana na majengo ambayo hayajaezwekwa, nilichangia nikasema kwamba bajeti iliyopita tumeona skuli mbali mbali ambazo hazijaezweka ikiwemo skuli ya Gando. Bajeti hii imeelezea kuezekwa ma madarasa haya ya sekondari. Je, Mhe. Waziri anambie ni lini majengo haya yataezekwa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa minongo'no imezidi hatutoelewana. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi, nakiri kwamba ni kweli tulisema katika ile bajeti ya mwaka 2017/2018 kwamba Skuli ya Gando itaezekwa lakini kupanga ni kuchagua, tuliona skuli nyengine ambazo zilikuwa na matatizo mengine zaidi ya ile nayo ni Skuli ya Uvinje pamoja na Skuli ya Kokota. Kwa hivyo kutokana na kuwa matatizo hayo yalikuwa ni makubwa zaidi, kwa hivyo ile nguvu ambayo ilikuwa imepangwa kwenda katika Skuli ya Gando, ikaenda katika skuli hizo mbili. Lakini naamini kwamba skuli hizo vile vile zimo ndani ya jimbo la Mhe. Mwakilishi ndani ya Jimbo la Gando, hivyo nadhani hatukufanya makosa kuona kwamba labda palikuwa pana uhitaji kuweza kupaweka sawa kulikoni pale ambapo hali ilikuwepo vizuri.

Lakini kama ambavyo tulivyoona katika bejeti hii ya mwaka 2018/2019 pia skuli hiyo imerejeshwa. Kwa hivyo nina maana kwamba ile progamu yake bado itaendelea katika hatua ya uwezekaji.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee nimeridhika.

Mhe. Mwenyekiti: Tumeshamaliza Mhe. Nadir wewe utakuwa mtu wa nne tumeshamaliza

Jumla ya Kifungu 5,057,550,000

Kifungu PK 0103 Programu kuu ya Elimu ya Juu

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na kunipa nafasi hii ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia katika bajeti hii nilizungumzia kuhusu upandishwaji wa ada za skuli bila ya utaratibu maalum, lakini alipokuwa Mhe. Waziri hajalitolea ufafanuzi suala hili kwa kina. Kwa hivyo numuombe sana kwa manufaa ya wanafunzi wetu walikuweko Vyuoni atupe neno angalau moja la kuweza kuwatia moyo na kuona hatma ya masomo yao yanaendaje.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa kukumbushia lakini ni kwamba hatukusahau lakini ningependa sana kumueleza Mheshimiwa ni kwamba hili suala lililokuja la kuongozewa kwa ada kwa kweli tumelisikia ndani ya Baraza hili juzi, mwanzo hatukuwa na taarifa nalo lolote lakini baada ya kulisikia hili suala tumelipokea na tayari tumeshaanza kulifanyia kazi. Kwa hivyo kwa kushirikiana na *TCU* vile vile tutalifuatilia vizuri lakini kuona kwamba vijana wetu hawa wasipandishiwe ada na si jambo sahihi kupandishiwa ada kati kati ya masomo. Kwa hivyo napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi wa Vijana kwamba serikali imelisikia, Wizira imelisikia na suala tutalifanyia kazi vizuri sana Inshaallah.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimeona hatari inasisogelea mbele yangu pamoja na vijana wenzangu kwa kusema kwamba Wizara hawalijui hili na wakati kwenye *semester* iliyopo sasa hivi na waliyokubaliana ilikuwa malipo ni milioni 5. Leo hii mtoto wa wanyonge anaongezewa milioni 2, analipa milioni 7 na mpaka sasa hivi Wizara haijui na hawalitambui. Sasa sijui Wizara inafuatilia vipi katika suala hili la Elimu ya Juu na ukiangalia chombo chetu kinachotunga Sera za Elimu ya Juu ni moja nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, niliposema Wizara hailijui haina maana kwamba hutujui kwamba wanafunzi wanalipa ada, tulichosema kwamba tulikuwa hatuna taarifa rasmi kwamba ada ya Chuo Kikuu cha *ZU* imepandishwa kiholela, hilo ndio ambalo nimelisema na naomba sana niliweke liwe wazi. Ni kwamba hatujapokea taarifa labda ya mamalamiko ya wanafunzi kuja kutwambia kwamda ada imepandishwa kiholela ndani ya chuo na isitoshe Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba sisi kupitia Bodi ya Mikopo tuna wanafunzi ambao tunawalipia ndani ya Chuo cha *ZU*. Malipo ambayo tunayalipa hajabadilika popote.

Kwa hivyo kwa msingi huo hatukuwa na taarifa kwamba kweli kuna ada imepanda kwa sababu kama kungetokea mabadiliko ya ada kwa wale wanafunzi ambao wanalipiwa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo lazima tungejua kwamba kwa nini mabadiliko yaani pesa zibadilike ghafla.

Lakini hakukuwa na mabadiliko hayo lakini kwa sababu tayari wameliwasilisha, tumelisikia vizuri na tumelipokea na nia na madhumuni ya serikali ni kuona kwamba vijana wake wanasoma katika hali iliyokuwa nzuri bila ya kububudhiwa kwa namna yoyote.

Mimi binafsi yangu nimepitia katika mchakato wa kusoma, ninajua shida kwa nini mwanafunzi unapomungezea shilingia 100 tu inavyokuwa ni tatizo. Kwa hivyo kwa hili nimuombe sana Mhe, Mwakilishi ni kwamba tumelisikia na tayari tumeanza kulifanyia kazi juu ya suala hii ahsante sana.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana lakini namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake ambayo yanatua moyo. Ningeomba sana jambo hili lichukuliwe hatua za harahaka ili kuona hatma ya vijana wenzetu na wasomi wenzetu inakwenda vizuri. Ahsante tuendelee.(*Makofi*)

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe.Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana lakini nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kufanikiwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema nimesikitishwa sana na serikali kukiuka sheria zake zenyewe ambazo tunazipitisha hapa Barazani. Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia Chuo cha *SUZA*. Chuo cha *SUZA* kinatakiwa kilete ripoti (*financial report, account report)* na ripoti ya Mkuu wa Chuo hapa Barazani. Na nikawakumbusha kwa Hoja yangu Binafsi taasisi zote zilizokuwa hazileti ripoti hapa Barazani ili wananchi wawe na upana mkubwa sana wakujua mambo yao yanavyoendelea, lakini sikumsikia Mhe. Waziri kusema chochote juu ya hili.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe ni kwamba juzi alisema lakini kwa bahati mbaya katika kusema inawezekana niliyasema mengi labda lake nililiruka, lakini tunamshkuru sana kwa kutuzindua juu ya hili na tunamuahidi kwamba ripoti hizi tutazileta ndani ya Baraza lako tukufu kwa muda muafaka kama ambavyo kiti chako kitatwambia muda gani, ahsante sana Mhe.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wetu wa Zanzibar mpendwa anasema, "*business as usually",* na tunaposali tunapata adhana ni kukumbusha sio kama hatujui wakati, tunakumbushwa. Na mimi kama Mjumbe wa Baraza nilitumia haki yangu kulikumbusha Baraza lako. Sasa inaelekea serikali inaanza kudharau Baraza lako hili. Kwa mantiki hiyo basi wafanye marekebisho wasituletee hizi sheria zisiandikwe zikaletwa Barazani, hazitutia afya sana. Kwa sababu kuendelea kusema mpaka sasa hivi ndio *financial report* ndio mpaka muda mwaka unasema kidogo *SUZA* hutuambii ripoti hizo unasema zitaletwa, lini zitaletwa sisi tunataka zilitwe lini zitaletwa nataka nijue.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu anauliza lini zitaletwa hizo ripoti.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ni kwamba kawaida Baraza huwa linapanga programu zake labda katika kipindi hichi tunajadili

hiki na hiki. Kwa hivyo kama hapo itakuwa Baraza limepanga programu hii basi na sisi tutakuwa tayari kuziwasilisha. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nilimpongeza sana Mheshimiwa mwalimu wangu Mwalimu Haroun Ali Suleiman, lakini nikampongeza sana Mhe. Salama Aboud Talib kwa kuleta ripoti ya *ZAWA* ijapokuwa haikukamilika kidogo ilikuwa na mapungufu ya sheria. Lakini walijua lengo la kuleta sheria hii.

Mhe. tuendelee tukiweza kutanabahishana sheria hizi ziletwe na hapa nina-*beep* na wengine nakuja.

Kifungu PK 0103 Programu kuu ya Elimu ya Juu 26,970,583,000

Kifungu PK 0104

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwanza napongeza kwamba *back benchers* leo wamepa *point* tatu za uhakika, siku nyengine hawa wenzetu huachia 11 hilo la mwanzo ni kwamba serikali, sio kwamba nashindana na nini, ni kwamba serikali tutaikosoa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ndio mara yangu ya mwanzo hii toka kikao cha kwanza kutaka kuzuia shilingi. Mhe. Mwenyekiti, nilichangia na naona tabu kwamba huu ni mwaka wa tatu nachangia kitu hicho hicho, lakini kiu kama haijapata maji inabakia kuwa kiu. (*Makofi*)

Mwenyekiti, kwanza wanasema siku zote msema kweli hukimbiwa na rafiki zake na hupata upekwe wa kitambo, lakini mimi sitauogopa kwa kutegemea kupata furaha milele pale kitu cha ukweli kitakapodhihiri. Mwenyekiti, nimechangia habari ya nyumba huu mwaka wa tatu, naona tabu naona haya lakini napigania vita nilitangaza kwamba kwetu ni Makunduchi, ni raia halali wa Makunduchi na kama hakutatokea mengine sitazikwa Kwarara wala Kibondeni, kama hakutatokea mengine ngoma itakuwa Kumbini.(*Makofi*)

Kwa hivyo nina haki ya kutetea kwetu ingawaje ni Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe. Mhe. Mwenyekiti, siku zote nilikuwa naulizia habari ya nyumba ya Kigaeni. Nyumba ambayo naionea huruma Serikali yangu ya Mapinduzi, serikali ambayo naipenda. Kila nikuuliza suala hili Mhe. Mwenyekiti, majibu yanakuwa ya ajabu sana. Hapa naona tabu. Mawaziri ambao mpo mbele yetu ni kwamba munamsaidia Mhe. Rais. Kwa hivyo mukijubu masuala ambayo hamna uhakika, wakati mwengine munatuumiza sisi huku. Hii serikali yetu, nyie mmetoka huku kuja huko kuisaidia serikali pamoja sisi.

Mhe. Mwenyekiti, niliuliza na baya zaidi *hansard* zipo. Mara ya mwanzo nikajibiwa kile ni Chuo cha Kilimo na Utalii na watu wamesha-*graduate* na wameshaajiriwa, *hansard* zipo nitakuletea Mhe. Mwenyekiti, nitazitoa. Hilo ni jibu la mwanzo la *comrade* Dkt. Khalid mtu ninanyemuheshimu sana humu ndani, baada ya muda akasema aah! ndivyo nilivyopewa. Mimi nimefunga Saumu hapa. Mara ya pili Mhe. Salama Aboud akasema kile...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye suala.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Haya nakuja lakini sisi wengine mpaka tufafanue fafanue, na juzi Mheshimiwa niliyemuuliza Waziri wa Elimu. Je, una habari kama kuna Chuo cha Amali Makunduchi. Akaniambia habari ninanayo na kipo chini Wizara ya Kazi. Hee! Wizara ya Kazi Mhe. Castico yupo, Mhe. Shadya yupo hao ndio Mawaziri wa Wizara hiyo. Kwa hivyo ninachoomba baadae hizi ni taasisi za serikali kunakuwa na mikataba rasmi ya kukabidhiana ili nidhihiri na iwe kweli, nataka baadae nije nione hiyo mikataba ambayo haitaundwa. Leo Mwanasheria Mkuu unanifahamu bwana isije ikaundwa leo hiyo, iliyoundwa ikakabidhiwa Wizara ya Kazi.

Lakini pia kuna *document* hii ya Waziri wa Katiba na Sheria alimpa Mwanasheria wake kwenda kwenye Kamati ya Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), nayo imelalamikiwa kama ni Wizara ya Katiba na Sheria. Ninasema tena nyinyi huko ni Mawaziri, nyinyi huko munamasaidia Rais, sisi huku tanarekebisha serikali yende vizuri, ikiwa majibu yatakuwa na matege. Mhe. Mwenyekiti, hatutaaminika. Kwa hivyo namuomba Waziri wa Elimu pale pale pameandikwa *Inswis Hostel and Vocational Training* palivyoandikwa pale Makunduchi, nadhani sijui kama unakujua au hukujui. Hivyo na hapana SMZ, sijaona kituo cha serikali cha serikali hii ambapo hapana SMZ, chini tu pameandikwa Kamati ya Maendeleo Makunduchi ndio wenye hisa.

Mhe. Mwenyekiti kwa uchungu sana .....

Mhe. Mwenyekiti: Nenda kwenye hoja Mheshimiwa, nenda kwenye hoja moja kwa moja sasa hivi.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Hoja yangu nataka jibu la ukweli Mhe. Waziri ulivyonijibu tumefunga hapa Saumu, wewe mwenyeo umesema tumefunga ni majibu yako au umepewa. Ninataka unijibu na una uhakika na ulivyonijibu kama huna uhakika, sema huna kama una uhakika sema nina uhakika ni chuo...

Mhe. Mwenyekiti: Ameshakuelewa Mheshimiwa, umeeleweka vizuri sana, halafu tuendelee.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mwisho sitaki mengi leo mimi nananchoomba baada ya hayo, sitaki kura maana yake kura haiwasaidii Wamakunduchi, mimi nataka Kamati Teule...

Mhe. Mwenyekiti: Tumekufahamu, subiri majibu Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Nisubiri Mhe. Mwenyekiti, leo zamu yangu miaka mitatu sijatoa hoja hii, miaka mitatu leo niachie kidogo na mimi. Hoja yangu na mimi...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa suala hilo ushalisema.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu na mimi naomba nakuomba kiti chako Mwenyekiti, hebu nawatafutwe watu watano au sita tumalize huu utata iundwe Kamati wakachunguze tuaambiwe ukweli imekwisha.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mheshimiwa subiri majibu kwanza. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na nataka nimtoe wasi wasi Mhe. Abdalla Ali Kombo kwamba asione uchungu na amekuwa akilizungumza jambo hili kwa muda mrefu sana.

Sasa na mimi nitaanza nyuma kidogo Mhe. Mwenyekiti, kusoma barua ambayo ilitoka Wizara ya fedha tarehe 27/11/2013, leo tupo 2018 na barua hiyo ilikuwa ni ya 2013 ambayo alipelekewa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, na ilikuwa inahusu nyumba ya serikali inayomilikiwa na Shirika la Utalii iliyopo Kigaeni Makunduchi.

Sina haja ya kusoma yote aliyoelezwa lakini nataka kusoma *paragraph* ambayo itathibitisha kama hii bado ni nyumba ya serikali, inasema kwa barua hii wizara inakukabidhi, anakabidhiwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, iliyokuwa kipindi hicho, tunakukabidhi rasmi nyumba hiyo kwa madhumuni ya kuwapa taasisi ya *CAAA* kwa masharti kwamba nyumba hiyo itaendelea kuwa ni mali ya serikali kwa muda wote wa matumizi ya taasisi hiyo. Hiyo ndio barua ya mwaka 2013 iliyokwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, wizara hiyo hiyo ikaingia mkataba tarehe 26/6/2014 na kwenye mikataba kuna pande mbili, kuna upande mmoja na upande wa pili. Upande mmoja wa serikali ilitiwa saini na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ya Kazi. Kwa hivyo kwenye mkataba yeye ndiye anayejulikana anasimamia ule mkataba. Nataka nisome Kifungu 0 ambacho kinasema;

"*on termination of this contract all project of hostel and school including improvement and features shall return to the ministry"*

Kwa hivyo hakuna umiliki ulioondoka serikalini kwenda kwa mtu mwengine, nyumba ile inafanywa kazi kwa mujibu wa masharti ya mkataba. Mimi nimuombe sana Mhe. Abdalla Ali Kombo kama ana hoja kwenye mkataba alete hoja yake, kama kuna masharti ya mkataba ambayo ameona yamevunjwa ayalete. Lakini umiliki wa nyumba ile kwa kumbukumbu ambazo zipo, bado miliki ya serikali.

Sasa sina hakika Mhe. Abdalla Ali Kombo amepata wapi taarifa nyingine tofauti na ambazo ziko serikalini, kama anazo taarifa ambazo ni tofauti na sisi atuletee. Lakini barua kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, kuna mkataba tokea 2014 unaoelezea hivyo. Sasa kama kuna hoja ya mkataba labda masharti ya mkataba hayafuatwi *than* alete hoja yake, lakini asiwe na wasi wasi wa kusema nyumba hii ni mali ya nani. Hii nyumba bado ni mali ya serikali na itaendelea kuwa mali ya serikali, hata ikiwepo kwenye wizara gani, bado nyumba hiyo ni mmiliki ya serikali. Kama tunavyojua mmiliki za serikali zote zinakuwa *treasury,* lakini *treasury* inaweza ikaikabidhi taasisi nyengine yoyote ya umma kushughulikia umiliki wa jambo fulani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, bado nyumba hiyo bado upo ndani ya mikono ya serikali. Sasa kama ana hoja kwenye masharti ya mkataba basi alete na sisi tutamsikiliza, lakini kama ana hoja ya umiliki nadhani hoja hiyo haina mashiko na mimi nadhani leo iwe ndio mwisho wake Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Ali Kombo, majibu umepata kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba hiyo nyumba ni ya serikali.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, majibu ya *AG* si ya msahafu, ni majibu ambayo amepanga kuitetea serikali. Nasema hivi Mhe. Mwenyekiti, wakati huo elimu haijulikani katika dunia, watu wenye mvi kama mimi wanahesabika ni wenye akili na watu wenye busara. Lakini elimu ilivyokuja duniani wanachostahiki ni shikamoo, sio kwamba wana akili.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ningemuomba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali afute kwamba haipo Wizara ya Kazi. Halafu nafsi ya binadamu Mhe. Mwenyekiti, mumesema tumefunga Saumu hapa, kila mtu anaijua ndani ya roho yake, nani mwizi, nani kaiba, nani kachukua. Ile ni hoteli.

Mhe. Mwenyekiti, jana nimekwenda Makunduchi kuna mtu ananilalamikia wageni wake 20 hawakuruhusiwa kukaa ananambia serikali sasa hivi ina ugomvi na hii hoteli. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama haitoshi nitakuletea maofisa wa serikali na nitakuweka wewe na Mhe. Mwanasheria Mkuu wazungumze, nasema tena nafsi ya mtu anayo mwenyewe kama kaiba ama hakuiba, kama kafunga kama hakufunga. Lakini wananchi tumesema Shekhe Haji Omar Kheir kaka yangu wa Tumbatu, alisema serikali haimuonei mtu. Nasema watu wa Makunduchi wasionewe. Naomba Kamati Teule kama haiwezekani basi lakini sitaki kura haitotusaidia Makunduchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Ali Kombo umemtaka Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali afute kauli yake kwanza, nafikiri ndio ulichomtaka hicho afanye. Mheshimiwa naomba utowe maelezo kidogo.

Kutokana na kauli yake anayozungumza ulikiri ulisema kwamba hiyo, lakini Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba iko chini ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, ni sawa sawa. Sasa sijui kama kasema yeye kwa nini afute sifahamu Mheshimiwa. *(Makofi)*

Lakini moja ambalo Mhe. Abdalla Ali Kombo amelizungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu amesema kwamba kama una taarifa yoyote basi ushirikiane na serikali kueleza, ili hatua zichukuliwe, kama una taarifa yoyote. Nafikiri Mhe. Mjumbe, una taarifa nzuri sana, pengine unajua zaidi kuliko serikali inavyojua, isaidie serikali Mheshimiwa hiyo ndio kazi yetu, isaidie serikali. Ninaiomba sana serikali, naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu, naomba sana serikali mumsikilize Mjumbe. Kama ikiwa kipindi cha miaka mitatu anazungumzia suala hilo hilo moja basi ina maana ana hoja. *(Mkofi)*

Kwa hivyo, naomba sana serikali ilichukuwe ilifuatilie. Mhe. Mjumbe ana hoja naomba sana serikali ilifuatilie ichunguze kuna tatizo gani. Mhe. Mjumbe mimi namuamini na naona kwamba

ana hoja anayoijenga kule. Tuifanyie hiyo kazi Waheshimwa, naiomba sana serikali, sitaki sasa hivi ya kuzungumza hayo naomba tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) sijakwita mimi. Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Suleman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa Mhe. Ali Khmis Bakar (Doholo) kufanya haraka haraka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nipo kwenye kutoa mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na kuhesabu kupita mafunzo ya elimu ya amali. Mhe. Mwenyekiti, hapa hoja yangu ipo kwenye majengo. Hili Mhe. Waziri alisema kwamba walikose wizara. Lakini mimi nilikuwa nataka kujua baada ya kukosea serikali, Mhe. Waziri alipokuwa akimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema kwamba ataangalia matengenezo ya Skuli ile ya Mtule kwa mujibu wa pesa watakazo pata. Lakini kwenye ujenzi wa skuli hizi za Vyuo vya Amali, serikali imetoa pesa mwaka 2016/2017 asilimia 95 na mwaka huu bajeti tunayokwenda nayo imetoa asilimia 87. Nadhani hata tukifika *quarter* ya mwisho itakuwa asilimia 95 kama awali.
Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Waziri atuambie kwamba ni lini Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, itatekelezwa kujenga majengo yale ili vijana wetu wapate kusoma. Pindipo Mhe. Waziri kwamba wamekosea, lakini sasa lini atuambie Mhe. Waziri kwamba ataanza ujenzi ule, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kumbukumbu zangu ni kwamba juzi nililijibu suala hili na tulielezea kwa nini hali ile imechelewa. Lakini napenda sana kumwambia Mhe. Mwakilishi tunaposema Ilani ya Chama inakuwa miaka mitato, yaani ndivyo invyokuwa, haina maana kwamba Daya na Makunduchi ndani ya miaka mitano hapana. Lakini tunapozungumzia utekelezaji wa Ilani ni kwa muda wa miaka mitano. Kama kwamba kuna programu zimepangwa kutekeleza ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano ina maana zitakuwa ndio zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini juu ya suala lake kwamba lini ujenzi ule utaendelea, baada ya kuelezea yote kuhusiana na matatizo ambayo yalitokezea katika ujenzi wa vituo vile viwili, ni kwamba tayari mambo yote ya sasa yamekaa sawa na tunaamini kwamba kuanzia mwezi ujao basi ujenzi huu utaendelea. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, nililokuwa nikilitaka nimelipata kwa sababu Ilani ndio iliyosema kutengeneza Chuo cha Amali Daya Mtambwe imo kwenye Ilani hii hapa pamoja na Makunduchi. Kwa vile Mhe. Waziri amesema kwamba mwezi ujao. Basi Mhe. Mwenyekiti, tutaona na Inshaallah tutasubiri ili kuona utekelezaji wa majengo haya yanatekelezwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipouliza suala la mwanzo nilipata ki-*memo* kutoka kwa kaka yangu Mhe. Shamata Shaame Khamis. Unajua unapokuwa na

hamu ya jambo unaweza ukasema wakati mwengine ukateleza. Kwa hivyo naomba niweke *Hansard* sawa, wakati nilisema kwamba Mhe. Waziri huko mbele nitakuja mkumbusha, nilisema kwamba nitakuja msokota. Kwa hivyo naomba niweke *Hansard* sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendea hapa katika programu hii nina masuala mawili. Suala langu la mwanzo Mhe. Waziri juzi alikuwa akinijibu vizuri, alinambia kwamba kutoka na Chuo cha Amali kilichopo Wingwi alinambia kuna vifaa vimepelekwa. Nakubalina naye kwa sababu mimi nimekwenda na nimevikuta, lakini nilisema vifaa vile havitoshi kulinganisha na wanafunzi waliopo.

Vile vile suala la umeme hamna kabisa na walimu ambao wanasomesha pale hawajaajiriwa hata mmoja, ni walimu ambao wanajitolea tu. Sasa jawabu la hapa sijalipata. Lakini vile vile niliweka nia ya kuzuwia shilingi katika pesa za suala zima la Elimu ya Watu Wazima. Kwa hivyo kwanza naomba anijibu hilo halafu nitaendelea na jengine.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa umakini wake.

Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane naye kwa kukiri kwamba kweli vifaa kavikuta vipo, aone kwamba kweli serikali inapokuwa inaahidi inatekeleza vizuri. Mhe. Mwenyekiti, suala la umeme tunalifahamu kama katika Kijiji cha Wingwi kuna tatizo la umeme, tatizo hili limetokezea baada kile kituo kuja kwa sababu bado ni kipya ilikuwa kwamba lazima pale pawekwe *transformer* kwa ajili ya matumizi ya kile kituo kutokana na matumizi mengi ya umeme. Kwa hivyo tayari kwa kushirikiana na *ZECO* suala hili tayari tunaanza kulifanyia kazi.

Suala la vifaa kama ambavyo wameeleza kwamba labda havitoshelezi. Kama hivyo tumeanza kupeleka naamini vikiwepo na vyengine tutakuwa tunapeleka ili viweze kuendana na hali halisi ya idadi ya watu ilivyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba atalifanyia kazi suala hilo, hapo mimi sina hoja. Hoja yangu ya pili Mhe. Mwenyekiti, niliweka nia ya kuzuwia shilingi, kwa hivyo hapa naomba anijibu vizuri ili hii shilingi nimrejeshee.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilitaka kujua kwamba pesa za Elimu ya Watu Wazima mara iliyopita katika kitabu hiki kidogo na buku kubwa la bajeti ni kwamba pesa hii haipo sawa kwa mwaka uliopita, lakini hapo sina hoja. Hoja yangu ipo katika pesa wa mara hii kwamba mimi katika Wilaya yangu ya Micheweni hususan kwenye jimbo langu sioni mimi hao wazee ambao wanasomeshwa kwa pesa hizi, wala sioni hayo madarasa ambayo yanajengwa kwa pesa hizi. Kwa hivyo nilitaka kusema nizuwie shilingi pesa hizi kwamba ni nyingi kwa upande wa Elimu ya Watu Wazima, pesa hizi badala ya kutumika hapa basi zigawanywe ama ziondoshwe kabisa na ziende katika sehemu nzima ya kuwasaidia walimu kwa njia ya nauli. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda sana kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba katika fungu hili kama ambavyo ilivyo ni programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali, maana kuna programu mbili ambazo zipo ndani yake. Kuna Idara ya Elimu ya Watu Wazima lakini pia kuna Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.

Kwa hivyo hizi fedha zipo nyingi katika fungu hili kwa sababu fedha hizi bilioni 10 zinakwenda katika ujenzi wa vile vituo ambavyo tunavizungumza, Kituo cha Daya pamoja na Makunduchi na ndio maana akaziona ziko fedha nyingi sana. Hivyo fedha hizi kwa sababu hii yote ni programu moja ndio maana zimewekwa katika fungu moja. Hivyo fedha zilizobakia ndio zinakwenda katika matumizi mengine, lakini hizo bilioni 10 ni kwa ajili ya vituo vya Daya pamoja na Makunduchi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninaamini kwamba karidhika na ile shilingi yake atairuhusu.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu aliyesimama ni dada yangu na kasema maneno mazuri. Kwa hivyo namrejeshea shilingi yake Inshaallah. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu PK0104 Programu Kuu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali 24,540,026,000
Kifungu PK0105

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kuna Wajumbe wengine hapa siwaoni kwenye *list* yangu ambayo inaonesha kwamba watazuwia vifungu, kuna wajumbe hawajatia nia lakini naona wanasimama. Sasa sijui vipi. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf uliweka nia ya kuzuwia kifungu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mimi nimeweka. Hakuna bajeti niliyokuwa sijaweka. Yaani hicho wala si cha kuuliza.

Mhe. Mwenyekiti: Utaratibu wetu mpaka uweke nia ya kuzuwia kifungu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Nimeweka labda kasahau mwandishi. Kwa sababu nina masuala yangu karibu manne nataka nijuwe.

Mhe. Mwenyekiti: Haya tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: La kwanza Mhe. Mwenyekiti, kuna taarifa au kuna malalamiko ambayo baadhi ya walimu hupata barua ya kwenda kuripoti mahala, lakini unaweza kukuta siku ya pili au ya tatu wakapata barua nyengine ya uhamisho. Sasa ningependa kupata jibu kutoka kwa Mhe. Waziri ni nani hasa wenye mamlaka ya kuweza kuhamisha walimu kwa njia kama hizo.

Mhe. Mwenyekiti, naweza kuuliza jengine hapo hapo, maana yake nina hoja nyingi.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea katika kifungu hiki, unahoji kifungu hiki.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ndio

Mhe. Mwenyekiti: Haya.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Lakini jengine vile vile nilizungumza kwamba katika Jimbo langu la Chaani nina walimu waliojitolea zaidi ya 50 ambao wengine wana miaka 15, 9 na 7 ambao wamesomesha bila ya kupata malipo na matokeo yake siku zinapotoka ajira wanachukuliwa watu wengine na wao wanasahaulika. Ningependa kujua sasa, ni lini walimu wale watakuja kuajiriwa ili usumbufu uondoke katika nafasi hizo za walimu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chaani kwa kumpa maelezo yafuatayo.

Suala la uhamisho wa walimu hasa kwamba kama ambavyo nimeeleza kuna matatizo yamejitokeza. Wizara kuona matatizo hayo, kwa hivyo sasa hivi uhamisho hasa anaoufanya ni mkurugenzi. Aidha, wa Maandalizi na Msingi ama wa Sekondari kutegemeana na kiwango cha mwalimu na *level* aliyokuwepo, kwa kuondosha mkaraganyiko kama ambavyo ameelezea. Kwa hivyo mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kumuhamisha mwalimu na atamshushia Afisa Elimu Wilaya pamoja na Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuhusiana na suala la walimu ambao wanajitolea. Nadhani serikali kwa kupitia bajeti ya Wizara ya Utumishi imefafanua vizuri sana masuala yote yanayohusiana na masuala ya ajira. Lakini niseme tu kwamba zinapotokezea ajira zinapotangazwa kila mtu yuko huru na ana haki ya kuomba ajira kwa mujibu wa kiwango chake cha elimu na kwa mujibu wa ajira ambayo inaombewa na nafasi ambayo inaombwa. Kwa hivyo sitosema kwamba kwa nini hawajaajiriwa watu wa Jimbo lale la Chaani, ila naamini kwamba ajira zinapotoka wanaoajiriwa ni vijana wetu wa Kizanzibari. Kwa hivyo naamini kwamba madam Chaani nao vijana wa Kizanzibari bila shaka na wao sifa hiyo wanayo. Kwa hivyo kama hawajaajiriwa labda bado hawajakuwemo, basi zinapotangazwa na Tume wakitangaza basi na wao vile vile wawe tayari katika kuomba ili na wao wawe miongoni mwa ambao wataweza kuajiriwa. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, uhamisho unafanyika hata Afisa wa Wilaya wa Elimu anakuwa hana taarifa. Sasa wizara husika ningependa wanaifafanulie zaidi.

(a) Je, huyo mkurugenzi aliomtaja anaweza kufanya maamuzi bila ya hawa viongozi wa wilaya husika kujua.

(b) Jimbo la Chaani lina Wazanzibari asilimia 99.99.09. Sasa walimu wale watawaahidi vipi kuwachukua, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sio jambo la masihara wamefanyakazi miaka 15, 7, na 5 bila kulipwa bila ya mshahara mpaka leo wanastahamili wanapewa shilingi 2,000 au 5,000. Lakini siku zinapotoka ajira Wallah Laadhim wanasahaulika, ni jambo la kusikitisha sana, walimu wale mtawachukua lini kwa sababu mimi sitaki tubishane, lakini nategemea kwamba haki yao wapewe. Serikali na wizara inawatambua kwamba wale walimu wapo wanasomesha na wanasomesha katika hali ngumu na

mazingira magumu. Kwa nini inapotoka ajira wapewe watu wengine wakati wale wanaweza, wameshasomesha miaka mingi na uzoefu wao mkubwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba vijana wanaojitolea kama hivyo ambavyo Mhe. Mwakilishi ameeleza hawako katika Jimbo la Chaani tu peke yake. Karibuni tunapofanya ziara tunapotembelea maeneo mengi sana tunakutana na tatizo kama hili. Lakini hata ushahidi tu Mhe. Rais alipokuwa akifanya ziara yake katika mwaka 2017 kama anakumbuka tulikutana na tatizo kama hili kwamba kuna vijana ambao wanajitolea. Mhe. Rais pale pale alisema kwamba zinapotoka ajira zichukuliwe kwa mujibu wa maeneo husika, nadhani hili Tume ya Utumishi wanakuwa wanalifanya. Lakini tuseme kwamba zinapotoka ajira Tume ya Utumishi inapotangaza, inasema kwamba ajira zinatangazwa kwa vijana wa Kizanzibari, haisemi kwa vijana wa pahala gani. Kwa hivyo yeyote mwenye sifa hiyo. Kwa maana hiyo zinapokuwa zinatangazwa tunaomba sana wote ambao wana sifa basi wanaweza kuomba.

Vijana hawa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba juzi tulijaribu kuangalia kuna walimu wangapi ambao wanajitolea, basi tulikuta zaidi ya 500 wapo ambao wanajitolea. Kwa hivyo kusema tu kwamba vijana wa Chaani peke yake tutakuwa hatujawatendea haki vijana wengine. Lakini tuseme kwamba Tume ya Utumishi inapokuwa inatangaza basi kila mtu ana haki ya kuomba nafasi hizo na tunaomba sana zinapotangazwa nafasi, wale ambao wote wenye sifa basi tunaomba sana waombe ili waweze kuwa miongoni mwao. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe, Mwenyekiti, Mimi mwakilishi wa Jimbo la Chaani, na siwezi kuongelea Jimbo la Tumbe wala Jimbo la Magomeni, nafahamu wapo walimu majimboni lakini humu mna wawakilishi wao mie siwezi kuongelea kila siku kwenye jimbo la mtu mwengine wakati wenyewe wahai wamo humu, mimi ninachotaka kujua wizara husika, itawasimami vipi wale vijana wangu wa Chaani kwa sababu wakienda huku hawapati kazi, na wao washajitolea muda mrefu. Kwa nini Mhe. waziri asiseme basi atajitahidi katika jimbo atachukua kumi, kwa nini leo walimu wapya hawana *experience* wamemaliza kusoma wanapata ajira wakati wale walokaa *15 years* kusomesha wenye *experience* hawachukuliwi? Hilo ndio suala langu, kwa nini tunachukua wepya wakati wenye uzoefu hawajachukuliwa, mimi natetea Jimbo langu sitetei jimbo la mtu mwengine.

Mhe. Waziri, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake ambayo ameyatoa, lakini pia nataka nimshukuru sana Mhe. Nadir Abulatif Yussuf kwa kutetea wananchi wa jimbo lake.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria yetu ya Utumishi wa Umma inatoa maelekezo ni jinsi gani waajiriwa wapya wataajiriwa, Sheria pamoja na Kanuni zake zinasema hivyo, kwamba serikali kitatangaza na wahusika wataomba, Sheria ile pia inazingatia mazingira ya maeneo hasa maeneo ya *remodel area* kama kokota, uvinje , charawe, uzi, mgonjoni, maeneo yale ambayo yapo katika mazinga ya kidagoni, maeneo yale ya kisiwapanza, tumbatu bahati nzuri tumbatu inajitosheleza kwa walimu, sheria ile inasema itazingatia mazingira kama wapo watu wenye sifa kutoka maeneo hayo basi serikali itatoa kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ili pia inawapa watu wenye ulemavu, kama wapo wenye sifa itawapa kipaumbele, namambo mengine. Kwa sheria ile inawigo mpana sana hata hivyo nataka mthibitishie Mhe. Nadir kwamba serikali imeshatoa maelekezo kwamba wale walimu wote ambao wanajitolea katika maeneo na wana sifa waorodheshwe ili serikali iweze kuona italitatua namna gani hili jambo.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa hivyo hoja yake Mhe. Nadir nadhani asubiri serikali imeshatoa hilo agizo kupitia Wizara ya Elimu kwamba waorodheshwe wale wanajitolea ambao wanasifa waajiriwa katika maeneo hayo. Kwa hivyo nimuombe ndugu yangu Mhe. Nadir akubaliane na hilo wazo la serikali ili avute subira pengine miongoni mwa hao watakao bahatika ni pamoja na walimu wake wa Jimbo la Chaani. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti katika sheria pia na uzoefu imekua *mation* uzoefu na mimi nilikuwa na *point* sana uzoefu nimpokeze wote wawili kwa majibu yao ambayo yanajaribu kuniridhisha lakini ningeomba sasa niipate kauli ya Mhe. Waziri ni lini walimu wa wale wote wa jimbo la Chaani waje wizarani kwako uwaone uwatambue ili ukae nao na uwafahamu, lini waje.

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Ahsante sana , Nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba wa Chaani kwamba katika ajira ambazo zimetoka walimu 6 ni wajimbo lake wameajiriwa. Kwa hiyo naamini kwamba wale walimu wale ni miongoni mwa wale ambao wanaojitolea wako katika ambao waliopata ajira, kama labda hawajamtaarifu hili naomba sana alifuatilie vizuri. Lakini nimwambie kwamba wakati wowote Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali milango yake iko wazi, kwa hivyo wanakaribisha muda wowote kuja ofisini. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nauliza lini waje, tarehe gani?

Mhe. Mwenyekiti: Haa! Lini anasema, Ameuliza suali jengine. Mhe. Waziri kuna suala ameuliza hujalijibu, lini atatembelea?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Hao walimu, Mhe. Naibu Spika, walimu hawajaajiriwa wengi, sasa ninachoomba hawa anaowasema kwamba niwalete lini ofisini kwake? Tarehe gani atakuwepo waje? Wasitoke shamba alafu wakaambiwa waziri hayupo nchini. Lini waende.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo milango ya wizara iko wazi, lakini kwa sababu sasa hivi tupo katika bajeti natunapomaliza hapa tunakuwa pia muda wa ofisi unamalizika itakuwa hawatuwatendei haki vizuri wananchi wake. Kwa hivyo nimuombe sana tutakapomaliza Baraza, tutapomaliza Bajeti basi nawaje ofisini, kama yeye atanambia au yeye atasema siku gani tunakuja wakati wowote, lakini tutawapokea na milango yetu iko wazi. Ahsante sana.

Mhe Zaina Abdalla Salum: Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii adhimu, wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia *program* hii ya uboreshaji wa elimu na nikazungumzia kuhusiana na kifungu kidogo cha Elimu Mjumuisho na nilizungumzia sana elimu hii imekuwa haitolewi kwa walimu ambao wamechukuliwa kwenda kusomea mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Mhe. Waziri yeye katika majibu yake alijibu kwamba kuwa serikali hainyanyasi watu wenyeulemavu, lakini mimi nikawa sikuzungumzia serikali nilizungumzia kuwa walimu hawasomeshi au hawatoi elimu ile stahiki kwa watu hawa wenye ulemavu na nikazungumzia kuwa kifungu kidogo inabidi kwa mujibu wa elimu stahiki watu hawa hawaipati basi tukizuie kifungu hichi na hivi sasa wakati umefika sasa naomba Baraza lako tukufu au wajumbe wa kamati hii ya kupitisha vifungu hadi vifungu tukizuie kifungu ili mpaka watakapoweza watendaji kufata shughuli zao na kutoa elimu kwa watu stahiki hawa nao ili waweze kupata elimu. Mhe. Waziri naomba.

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe, namshukuru Mhe. Mwakilishi wa viti maalum, najua kwamba kweli anawatetea sana kwa sababu yumo katika kundi hilo na ana watetea vizuri sana, nimpongeze sana kwa hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama ukipeleleza kwamba tunafanya kuona kwamba wanafunzi hawa wote bila ya ubaguzi wowote wanapata elimu iliyobora ndani ya nchi yetu. Kwa hivyo nipende sana kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kama kuna walimu hawaajibi ipasavyo, kwa wanafunzi hawa, hawafanyi kazi ambao wametumwa basi sheria ziko wazi.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa hivyo ni muhakikishie sana Mhe. Mwakilishi ni kwamba kama ataniletea labda kama anayo taarifa yoyote, tuweze kuifanyia uchunguzi ili tuone kama kuna walimu hawa hawajibiki, basi kwa mujibu wa sheria tuweze kuwashughulikia kama ambavyo sheria za Utumishi wa Umma zilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Lakini vile vile nimuhakikishie kwamba tunavyo jitahidi sana kufanya ziara za mara kwa mara ndani ya maskuli yetu ili kuona namna ya uwajibikaji wa walimu wetu, lakini wakati mwengine inawezekana wewe unapokwenda unakuta mwalimu anawajibika kama ambavyo ilivyo, inawezekana wakati mwengine wewe hupo, huwezi kujua nini kinaendelea nyuma yake. Lakini yeye kama kalibaini lolote ambalo linakwaza vijana wetu hawa basi tunamuomba sana atupe ushirikiano wa hali ya juu ili kuona kwamba vijana wetu hawa nao wanapata elimu bila ya ubaguzi wa aina yoyote, na walimu hawa nao waweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu Sheria zetu za Utumishi zilivyo. Ahsante Mh. Mwenyekiti.

Mhe Zaina Abdalla Salum: Ahsante, Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kunipa majibu, lakini majibu haya, Mhe. Waziri yamekuwa ya kila siku tumekuwa tunapewa moyo, na hivi sasa kazungumzia sheria ipo, na kama sheria ipo jee, sheria hiyo inasimamiwa vipi? *(Makofi)*

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti, sheria inasimamiwa kwa yule ambaye itakuwa amefanya kosa basi sheria itakuwa inachukua mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, Na kama ambavyo nimetangulia kusema kwamba kama ana taarifa yoyote, kwa sababu inawezekana kuna taarifa yeye anayo lakini hajatupatia hiyo taarifa, nimuombe sana kama kuna taarifa yoyote juu ya walimu wetu, ambao kwa namna moja ama nyengine, wameshindwa kutimiza wajibu wao kwa wanafunzi hao ambao wanaulemavu wa uziwi, atupe taarifa hiyo, ili nasisi tufanye uchunguzi wetu wa kina na tuone kwamba yule mwalimu sheria ina mbana basi sheria iweze kumbana. lakini sheria zipo kwa ajili ya kuwakamata wale ambao watakuwa wanamakosa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa hivyo nimuombe sana kama taarifa hiyo, basi namuomba sana sana sana. Tushirikiane ili kulitatua tatizo hili kuzuia shilingi bado itakuwa hatujaweza kutatua tatizo chochote, tutazidi kuwaengezea mzigo vijana wetu wale watakosa. Kwa sababu tunapozuia inamaana mwaka mzima utapita bila yakuwa ya kuwa na fedha ya aina yoyote. Lakini tukiwapa fedha tunafuatilia kama kuna tatizo yeye kaliona akituambia tutashirikiana kwa pamoja kuona kwamba hiyo sheria basi inafanya kazi yake vizuri. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe Zaina Abdalla Salum: Ahsante, Mhe. Mwenyekiti, Kwa vile Mhe. Waziri kanambia kuna sheri na sisi sote tunaongozwa na sheria, ndio mana tukawa tumefika hapa. Lakini Mhe. Mwenyekiti kwanza nimuombe Mhe. Waziri hii sheria yake aizingatie vizuri, kwa sababu mambo haya yamekuwa yakiendelea siku hadi siku na kila siku yamekuwa ndio ivo ivo. Kwa hivyo mimi nataka nimuhakikishie Mhe. Waziri, mimi nakuwa nafanya ziara ya kushtukiza yeye mwenyewe hajui. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Lakini hii sheria aliyoizungumzia ni muombe sana sana sana, awahimize watendaji wake waweze kuisimamia vizuri ili watu wenye ulemavu wapate elimu yao stahiki, kwa sababu hivi sasa ishakuwa ni tatizo sugu.

Mhe. Mwenyekiti, Watoto wanaacha skuli, wanaacha masomo yao kwa kuwa hawaelewe kitu ambacho wanachofundishwa walimu wanazungumza modomo mitupu.

Mhe. Mwenyekiti, tusipoteze muda. Ahsante sana tuendelee.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nikushukuru sana Mhe. Naibu Spika, namimi kwa sababu maelezo niliyokuwa naeleza wakati wa kuchangia sikupata majibu ningeopmba Mhe. Waziri namimi aniweke vizuri katika masuala yangu katika kifungu hichi ambacho kina kimeanza na SK01- 08, sitaki kuja kwenye fungu jengine.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa hivyo nna masuali yangu nataka anieleze kidogo, moja nilimwambia Mhe. waziri kwamba namuuliza jee ana ofisi ndogo ya *NECTA* ambayo ni elimu ya juu kwa sababu matatizo mengi yanayotokea Zanzibar, unasikia yako *NECTA*. Lazima mtu asafiri kwenda Bara, au tunatumia *NECTA* kwa Wizara ya Elimu Zanzibar, au kuna kifungu maalum cha *NECTA*, ambaco cha Jamhuri ya Muungano hichi sijasikia jibu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili nilimuuliza Mhe. waziri kwamba, elimu yeye ndie msimamizi mkuu wa elimu wa Zanzibar, yeye ndie anayetunga mitaala yote ya elimu, yeye ndie anayetoa vitabu vya elimu, lakini inakuwaje shule za binafsi, na shule zikatafautiana vitabu, lakini wakati

wa mitihani, shule za Serikali zinateremka chini kiwango na shule za binafsi ziko juu, ni sababu gani ambazo kiwango chetu cha elimu kinashuka wakati ambapo serikali inajitahadi kwa asili mia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, Lakini chengine ni kwamba tulikuwa na suala la michezo katika kifungu cha 8.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja zisidi Mheshimiwa zaidi ya mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Sio tatu Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Aa! Hoja ni mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Basi Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Tatu tayari hoja zimeshatolewa na wengine, Kwa hiyo hoja zako wewe ni watatu wa mwisho, hoja ni mbili, funga kwenye hoja zako mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Sawa Mheshimiwa.

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mwakilishi Suleiman Sarahan Said Jembe la Chakechake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kumbu kumbu zangu suala la *NECTA* nakumbuka tulilijibu kwamba ndani ya Zanzibar tunayo ofisi ndogo ya *NECTA*, na tulimtaja mpaka Mwakilishi wake Maalim Kassim kwamba yeye ni mratibu wa *NECTA* kwa upande wa Zanzibar, na ofisi yake ipo. Lakini hata wajumbe wetu wapo katika suala hili. Kwa hivyo nadhani labda kwa wakati ule alitoka nje, inawezekana ilikuwa ni muda wa ibada, kwa hivyo hakunisikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, na kuhusiana na suala la Mitaala nikwamba ilivyo serikali inaandaa mitaala yake kwa elimu ya msingi kwa skuli zote iwe za binafsi iwe za serikali. Skuli za binafsi zote zinatakiwa zifate mitaala ya serikali. Na ndio maana tunaposema kwamba ile kupitia Idara yetu ya ukaguzi wa elimu ni kwamba tunafanya ukaguzi, kuona zile skuli za binafsi jee, zinafata mitaala yetu ama hazifuati. Na tunabaini kwamba kuna skuli hazifuati mitaala yetu kama ambavyo inapaswa kufuatwa, basi sheria kwa mujibu wa sheria ya elimu huwa inafanya kazi yake. Kwa hivyo naomba nimuhakikishia Mhe. ni kwamba hili ndio ambalo linafanyika. Lakini skuli zote za binafsi zinafuata Mitaala ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ambavyo zinatumika ndani ya skuli zetu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, Mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake, lakini tatizo moja ninaloona ni kwamba waziri kwa mwaka huu wa fedha wa 18/19 ana niaahidi nini kwenye shule za serikali kupanda kiwango cha kufaulu.

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nikumbushe Mhe. Mwakilishi kwamba na yeye ni mwakilishi wa wananchi na amechaguliwa na wananchi kuweza kuwakilisha, lakini kuweza kuwasaidia kwa kila ambalo linapaswa kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, suala la elimu si suala la Wizara Elimu peke yake au suala la serikali peke yake ni suala la jamii nzima. Sisi wanafunzi wanapokuwa skuli tunakuwa tunawasomesha vizuri sana, tunawafanyia kila kitu, tutawaweka wakae mpaka jioni wasome, mtoto anaporudi nyumbani ni suala la jamii kuweza kutusaidia sisi wizara, kuona kwamba mtoto yule anapitia masomo yake vizuri sana. Kwa hivyo, Mhe. nimuhakikishie kwamba iwapo tutashirikiana vizuri sana sote kwa pamoja nnaamini elimu yetu itazidi kukuwa kama ambavyo tunapaswa iwe na ubora wa elimu utaweza kuonekana vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa hivyo, tushirikiane kwa hili sote, kwa sababu sote ni masuul wa suala hili kwa hivyo, tushirikiane kuona kwamba elimu yetu inakuw vizuri kwa kuhamasisha na kuwashajihisha vijana wetu, wafanye bidii katika kupitia masomo yao. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti tuendelee, tuendelee.

Kifungu PK0105 Ubora wa Elimu Programu kuu ya Ubora wa Elimu
Jumla Kuu **7,723,628,000**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Kifungu PK0106

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na wajumbe hapa niombe tusaidiane kwa umakini kwenye hoja hii, na niwambie tu mawaziri hamko wakamilifu mnapokosea mkubali kukosolewa, na hatuna nia yetu, nia yetu nikujenga nyumba moja, na hakuna mkamilifu. Hoja yangu maslahi ya walimu kuboresha. Kuna Tume ya Utumishi Serikalini, kuna Tume ya Mahkama, Tume ya Baraza la Wawalishi, kuna Tume ya Vikosi.

Mhe. Mwenyekiti, Walimu hawa wamekuwa wakipata shida kuhusu maslahi yao, shida zao ukweli wao, kilio chao, hawakijui wakipeleke wapi? Waziri na manaibu waziri wanamajukumu mengi, wizara ina majukumu mengi, maslahi yao na kimoja kinacho changia walimu hawa pengine kuto kufeli hawapati kusikilizwa shida zao.

Mhe. Mwenyekiti, Hata Mhe. Rais alisema kama kuna haja ya kuundwa Tume ya Utumishi ya Walimu basi iletwe serikalini. Febuari 2018, katika Baraza la Wawakilishi la zamani kwa hapa nimuombe na wajumbe hapa nakuombeni sana, sana, kama hatukuangalia maslahi ya walimu, Kuundiwa Tume ya Utumishi itakuwa ni mtihani. Ikiwa kuna Tume ya Utumishi ya Serikali, Mahkama, Baraza la Wawakilishi, walimu hawa wanakazi kubwa. Kwa hivyo wajumbe

nikuombeni sana hapa tusaidiane. Silangu mimi tuwasaidi. Nataka ukweli kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa wananchi jimbo la Paje.

Mhe. Mwenyekiti, Ni kweli alizungumza na kama ambavyo hiyo siku anayozungumza ni siku ambayo kuna Mkutano Mkuu wa Walimu na bahati nzuri siku ile alikuwa kaimu waziri wa elimu wakati ule alikuwepo katika ule mkutano, ni kwamba Mhe. Rais pia alizungumzia suala la Tume kama ambavyo walimu waliliwasilisha kupitia Chama cha Walimu, na mamlaka ya kuunda Tume ni malaka yake mwenyewe Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwamba hata yeye mwenyewe katika michango yake alisema kwamba halazimishi ilia ametoa ushauri. Kutokana ametoa ushauri ina maana ushauri wake tumeusikia. Ushauri wake Mhe. Mwakilishi tumeusikia wa Tume ya Utumishi ya Walimu.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya kuunda Tume hayapo chini ya Wizara ya Elimu n Mafunzo ya Amali, ni mamlaka yake mwenyewe Mh.Rais. Kwa hivyo Mhe. Rais amesikia ombi la Mhe. Mwakilishi, na vile vile hata walimu walisikia ombi lao na siku ile pia waliweza kutoa majibu mazuri sana, Mhe. Rais katika ule mkutano wa Chama cha Walimu siku ili ya tarehe 10 Februari, Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi naomba nimwambie kwamba, tumesikia ushauri wake. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana he. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, haya tunayozungumza humu ndani ni kuisaidia serikali yetu, nilipiga kelele hapa Wizara ya Afya, na niwashukuru sana Wizara Afya wakati huo Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, walikuwa wakisema wanaonewa, wanapiga kelele, aliweka pale kitengo cha kulalamika kinafanyakazi masaa 24. Mgonjwa akiwa hakupata matibabu au mahitaji yake huenda katika lile dirisha kwenda kulalamika, sasa hili suala la muda mrefu, kama anataka tupitishe hichi kifungu afungue ofisi ya dharura kwanza ili tupitishe kifungu kama atakubali hivyo, pale pale wizarani kwake *atleast* tuone mwendo wa mwazo hili suala la muda mrefu Mhe. Mwenyekiti kama anataka nipitishe fungu tuunde pale pale afisini kwake kwa dharura kitengo hicho , halafu baadae yatakuja mengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mheshimiwa nimemuelewa sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje hoja yake na hoja hizi za walimu kuomba wawe na Tume yao ya Utumishi ni la siku nyingi sana. Lakini tutizame umuhimu wa kuwa na tume kila taasisi kila wafanyakazi wakitaka kuundiwa itakuwa kazi kubwa sana.

Hivi sasa kuna Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi kuna Tume ya Utumishi Mahakama kuna Tume ya Utumishi ya Vikosi na tuna Tume ya Utumishi Serikalini na walimu ni sehemu ya wafanyakazi wa serikali ndio maana yake serikali tumehisi mpaka hivi sasa bado hakujakuwa na haja ya kuwa na Tume ya Utumishi wa Walimu na hao walimu kama wana matatizo yao yote ya

kiutumishi Afisi ya Tume ya Utumishi Serikalini ipo tayari wende wawasilishe hoja zao tutazisikiliza na tukiona kuwa kuna haja basi tutawasiliana na Kamisheni ya Utumishi ili tuone vipi tunaweza kulifikiria jambo hilo. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri hawa Chama cha Walimu ZATU wamelalamika muda mrefu kama alivyosema Mhe. Waziri hata Mhe. Rais akasema kama ipo haja serikali ichukuwe suala hili na yeye Mhe. Waziri kajibu lakini hapa Dar-es Salaamu tu wanayo tume hiyo ya Utumishi ya Walimu na hichi ndicho chanzo nakihisi kama maoni yangu wanafunzi kutokufanya vizuri walimu wana malalamiko mengi, Mawaziri wanashughuli nyingi sana na Manaibu Waziri. Sasa watakwenda wapi?

Hii tume muhimu ikiwa Vikosi wana tume yao na hawa walimu wengi ninavyoamini kuliko Vikosi walimu ni wengi na hao walimu wote wametokea katika suala la ualimu. Kwa hivyo, hii hoja ni muhimu kuundwa japo kwa dharura tu kwanza pale, wamelalamika muda mrefu hawa ZATU.

Mhe. Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia nashukuru kwa hoja ya Mjumbe aliyoileta katika kifungu hichi. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nitoe tamko rasmi na ni tamko la serikali kwa sababu tamko hilo siku linatokea mie ndie nilikuwa Kaimu Waziri wa Elimu katika ile ghafla ya siku ya walimu.

Naomba nimjulishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Paje kwamba siku ile tamko la serikali lilitoka pale kujuilishwa katika risala ya walimu ambao walisoma walikuja na ombi hilo na Naibu Waziri alikuwepo wizara nzima ya elimu iliyokuweko huko nyuma ilikuwepo na mie ndie nilikuwa Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nikiwa namuwakilisha Mhe. Riziki Pembe Juma. (*Makofi*)

Tamko lilitoka kwamba haitoundwa tume nyengine ya Utumishi ya Walimu maalum kwa ajili ya walimu. Tume hiyo hiyo ya Utumishi ya Serikali ndiyo itakuwa inashughulikia masuala yote na bado tume hiyo haikushindwa na kazi hiyo. Hilo ndilo tamko rasmi na ipo katika hotuba ambayo Mhe. Rais Dr. Ali Mohamed Shein aliitoa pale. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya mawaziri karibu watatu. Sasa kuomba si kosa kuiba ndio kosa, katika hii Tume ya Utumishi hawa walimu ni wengi niiombe serikali kuwe na kitengo chao maalum basi katika Afisi ya Tume ya Utumishi wakifika pale angalau anayetoka Pemba kuja pale asije kaa siku tatu au nne apate kumuona Mhe. Waziri au Naibu Waziri.

Kwa hivyo, niombe Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman pawe na kitengo maalum pale cha walimu na yeye alitokea hii Wizara ya Elimu na hili ni ombi. Nataka kauli ya serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, Tume yetu ya Utumishi Serikalini ni Tume ya Watumishi wote Serikalini ukiacha

zile taasisi ambazo zina Tume zao vile vile. Kwa hivyo kuweka tu kuwa na *desk* maalum la walimu tu tutakuwa tunafanya ubaguzi. Tume ile ipo kisheria kwa watumishi wote serikali.

Mimi nawaomba walimu kama wapo wana matatizo haya basi waende tu kwa Mkurgenzi wa Kamisheni wa Utumishi wa Umma watashughulikiwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nafikiri umesikia serikali inavyozungumza. Serikali wanasema kwamba hao walimu wanaweza kuitumia Tume ya Utumishi kama wafanyakazi wengine wote. Mimi nafikiri muhimu ni kwamba walimu watambue haki zao katika suala zima la utumishi na wana haki ya kuitumia Tume hiyo hiyo ya Utumishi ya Serikali. Kwa hivyo mimi nafikiri zaidi ni kwamba uwape taarifa hao ambao walimu wanahisi kwamba hawapati haki kutokana na kwamba hawana Tume. Tume ipo na wao wanaweza kuitumia hiyo.

Nafikiri hilo ndio kubwa Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kidogo tu kuweka sawa. Hii wizara ni kubwa sana kuna Katiba na Sheria tulitoa ushauri utumishi wote Unguja na Pemba Mheshimiwa tuendelee. (*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nilisimama mafungu mengine sikupata nafasi. Lakini mimi sina nia kabisa ya kuzuia fungu nipo katika fungu hili la Uratibu ya Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, niliandika mimi mchango wangu kwa sababu hatukupata nafasi maelekezo yako, ulitwambia tuandike kwa maandishi na nilifanya hivyo na nikawa naizungumzia Skuli ya Muembemakumbi ambayo nashukuru pia Mhe. Waziri kasoma skuli hiyo na jengo ambalo nilililokuwa nalizungumzia ni jengo lile la kabla ya Mapinduzi kwa muda mrefu limekuwa halitumiki.

Sasa nikataka kujua tu ule mpango wa serikali katika kulitengeneza lile jengo. Lakini na kama serikali haina mpango kwa sababu tumeunda Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa sababu na lile linaingia kwenye utaratibu huo huo basi tulitangaze ili tuweze kupokea watalii baada ya yale matumizi ya skuli yaliyokuwa ya awali. Mimi sina tatizo nilikuwa nasubiri majibu ya Mhe. Waziri atakavyonijibu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi wangu ndani ya Jimbo langu nakukiri kwamba ile skuli hata na mimi nilipitia. Mheshimiwa alichokichangia ni kwamba aliuliza katika utaratibu wa ukarabati wa majengo serikali imeanza mfumo wa ukarabati wa majengo kwa skuli tatu kama ambavyo tumeeleza. Tumeanza na skuli ya Lumumba, Haile Salassie pamoja na Ben Bella.

Kwa hivyo na utaratibu midamu umeanza bila shaka utaendelea na majengo mengine namuomba Mhe. Mwakilishi kwamba aiachie serikali iangalie mfuko, unazidi kutononoka baada ya kuanza kufanyiwa kukarabati majengo matatu haya ni lipi jengine litaingia. Lakini na hili lake yeye ni

kipaumbele kwa sababu kama ambavyo anasema hata mimi ile skuli ndiyo ambayo nimesoma naiona na natamani siku moja nione lile jengo linaendelea kusomewa kama ambavyo sisi tulipokuwa tunasoma katika miaka ile ya nyuma. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi tukuombe sana kwamba serikali imeanza ukarabati basi kadri ambavyo tutakuwa tunapata pesa tutaongeza na majengo mengine, lakini na hili nalo litakuwa ni kipaumbele. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti namshukuru sana Mhe. Waziri, ilikuwa mimi hamu yangu kujua tu maana aidha tunapeleka mambo ya kale au tunaingia kwenye ukatabati lakini nimemfahamu sana Mhe. Waziri tunaendelea kukusubiri. Ahsante tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: *Wallah Laadhim* nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kuweza kunipa hii nafasi nikaweza kutetea maslahi ya walimu hasa katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikijenga hoja zangu nilikumbushia wizara na nilimuomba Mhe. Waziri wa Fedha ili aje amsaidie Mhe. Waziri kujibu suala hili. Pamoja na kuwa Mhe. Waziri wa Fedha hayupo lakini naamini serikali ipo itaweza kunisaidia au kumsaidia Mhe. Waziri kujibu suala hili. Hoja yangu ilikuwa malimbikizo ya maslahi mbali mbali ya walimu ikiwemo viinua mgongo, marekebisho ya mishahara lakini vile vile na pesa nyingine za likizo.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilikuja na hoja, walimu walikuwa wanadai malimbikizo yao bilioni 5. na nilimuomba Mhe. Waziri wa Fedha, fedha hizi kwa kutegemea bajeti ya wizara ya Elimu kwa mujibu wa bajeti tunazowapitishia tutawakwaza na watashindwa kufanya shughuli nyingine kwa sababu pesa ni nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, bado leo nakuja katika Baraza hili zaidi ya mwaka mmoja, bado madai ya malimbikizo ya walimu ni mengi sana hapa nna barua zaidi ya kumi waliyokuwa wanakumbushia wizarani na wengine wakaona wizarani hawapati jawabu wamefika hadi kumuandikia mpaka Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe. Mwenyekiti hata ukiona hali hiyo ujue hali ishakuwa tete, kuna walimu wamestaafu toka mwaka 2015/16 mpaka leo bado viinua mgongo hawajapata na ndiyo pale niliposema huu ubora wa elimu tutakuwa tunauzugumza mdomoni tu kwa sababu walimu kaka hawajapewa maslahi yao wakatulia ndani ya nafsi zao kwa kweli itakuwa ni shida. Mheshimiwa mpaka sasa hivi bado malimbikizo ya walimu ni mengi na nimejaribu kuangalia bajeti ya mwaka huu Mhe. Mwenyekiti kwa kweli zile fedha ambazo walizoongezewa yaani hapa bajeti ya mwaka jana ukiangalia karibu bilioni 7 safari hii ni bilioni 8 bilioni 1 tu wakati huo walimu wanadai bilioni 5 malimbikizo na haya malimbikizo kwa kuwa walimu wanastaafu na walimu wanaendelea kusoma yataendelea sasa leo Mhe. Waziri wa Fedha hayupo nilimuomba Mhe. Waziri wa Fedha hili deni liwe ni deni la serikali lilipwe aidha moja kwa moja katika mfuko mkuu wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika hili hakuwahi kunipa jawabu la kutosha najua mambo yalikuwa mengi lakini naamini atanieleza kama serikali imeshawalipa kiasi gani lakini bado mimi ninaavyojua bado walimu ni wenngi wamo mitaani mungu apishie mbali sijui wangine

sijui kama wengine sijui kama hawajatangulia mbele ya haki lakini mpaka leo bado wanadai stahiki zao. Naomba jawabu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi Mwenyeviti wa Wenyeviti kwa kujali sana walimu naamini hata nyumbani kwake itakuwa anae mwalimu ndani ya nyumba yake.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba serikali kwa hili tayari imejitahidi sana katika kulipa malimbikizo ya walimu labda hili nimwambie kwamba binafsi sisi tulipoingia katika ofisi zetu tulikuta madeni walimu yakiwemo ya likizo na madeni mengineyo, na hivi tunavyozungumza mpaka sasa kwa mfano kwa madeni ya likizo mpaka 2016 tumeshamaliza kulipa, 2017 kwa sababu likizo za walimu mara nyingi wanakwenda mwisho wa mwaka Disemba kwa hivyo disemba wanakwenda likizo baada ya kwenda likizo wanaandaliwa utaratibu wao na fedha hizi tayari katika hii kota ambayo inamalizia wanamaliziwa wale ambao wa 2017 lakini waliobakia wote wanaodai pesa za likizo basi tayari wameshalipwa na kama binaadamu pengine kuna mwalimu kwa bahati mbaya sana inawezekana labda hajaja mwenyewe wizarani kuchukua basi huyu tunamuomba aje ili achukue fedha zake.

Na malimbikizo mengineyo, binafsi Mhe. Waziri wa Fedha kweli hayupo lakini hayupo kwa sababu ya dharura za kikazi lakini aliniambia suala hili kwamba tayari kupitia yeye kwenye meza yake weshalipa mpaka mwezi wa Februari mwaka 2018 malimbikizo yote ambayo yalikuwa yanadaiwa kwa serikali kwa sababu utaratibu uliopo ni kwamba yanapokwenda maombi yanakwenda maombi ya wafanyakazi wa serikali hayendi labda kama huyu peke yake Mwalimu, huyu Daktari huyu labda kada nyengine, yanakuwa maombi kwa ujumla wake. Na wao wanachofanya wanakusanya yale maombi kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu wanakuwa wanalipa kwa hivyo mpaka februari 2018 tayari wameshalipa na sasa hivi wanaendelea katika miezi ambayo imebakia mpaka kumalizika mwezi wa juni. Kwa hivyo naamini kwamba kama kuna walimu ambao nao watakuwa ni watumishi wa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kama wapo ambao katika msururu huu wa kusubiri katika miezi mitatu hii hapa basi naamini na wao watamaliziwa. lakini Mhe. Mwakilishi namwambia kwamba sisi binafsi wizara kwa sasa hivi kwa kesi hizi tunapokwenda katika *field* zetu basi hatukuti tena tatizo hili na walimu wanaatushukuru sana wanaishukuru serikali kwa kuweza kulipwa madeni yao. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyonishuru mimi Mhe. Waziri na mimi namshukuru sana kwa sababu ni mtu ambae anasikiliza hoja na anazifanyia kazi. Mhe. Mwenyekiti ameeleza kwamba ameambiwa na Mhe. Waziri wa Fedha katika meza yake tayari kuna malimbikizo mpaka Februari 2018 lakini mimi nataka nimthibitishie. Na kwa bahati nzuri Mhe. Waziri alisema malimbikizo haya siyo kwa wizara ya elimu tu ni serikali nzima nataka nikuthibitishie. Mhe. Mwenyekiti kwamba malimbikizo bado yapo mimi nina watu amabao wamefanya kazi Manispaa katika marekebisho ya mishahara mpaka leo hawakurekebishiwa lakini vile vile huko wizara ya elimu wao wanasema wameshalipa mpaka mwaka 2016 lakini kuna walimu waliostaafu mwaka 2016 mpaka leo wapo nyumbani hawajalipwa viinua mgongo kwa hivyo bado hili tatizo lipo kubwa. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani kwa sababu Mhe. Waziri ameshaipata hoja yangu sasa basi labda sitaki niwe *agency* lakini kwa wale ambao

hawakuridhika na kuambiwa kwamba mpaka mwaka 2016 wameshalipwa ambao bado hawajalipwa basi nitaomba kwa sababu mimi ndo mwenye hoja basi wanitafute ili niwawasilishe mimi mwenyewe au wao waende wenyewe wameshindwa basi warudi tena kwangu ili niweze kukamilisha hizi hoja zao lakini bado nataka nimwambie Mheshimiwa walimu wengi ambao wamebadilisha kada yaani waliobadilisha mishahara baada ya kurudi masomoni wengi wao mpaka sasa hivi hawajalipwa stahiki zao na ndiyo maana wameandika barua mpaka kwa Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kuona wizara ya elimu hawajalipwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri akubali tu kwamba hiyo takwimu aliyopewa bado haijawa sahihi lakini usahihi bado kuna walimu wengine bado hawajalipwa malimbikizo yao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba ambao anawaelezea kwamba kuna wengine hawajalipwa, kuna walimu ambao watalipwa ndani ya mwaka mpya wa fedha utakaoanza mwezi wa julai kuna walimu ambao watamalizia kulipwa *area* kama alivyozungumza wale ambao wamerudi masomoni. Lakini kwa yale mengine ambayo ameyazungumzia malimbikizo ya wale walimu wengine waliokuwa miaka thelathini ambao walikuwa hawajalipwa , walimu walioanza likizo na nyenginezo zile ambazo kama tumeeleza kwamba tayari zimeshalipwa . Lakini kwa hizi kwa wale ambao wametoka kusoma kwa mfano mtu karudi kusoma mwezi wa julai lakini kwa bahati mbaya sana hata kurekerbishiwa muda kwa hivyo wale ndiyo majani yao watalipwa kipindi cha julai mwaka mpya wa fedha ambao utaanza.

Mhe. Mwenyekiti, Lakini jengine naomba sana nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba walimu wanapokuwa na matatizo yao wengi wao wanakuja wizarani wanasilizwa na wanatatuliwa shida zao. Lakini kuna baadhi yao kwa sababu mimi namjua Mhe. Hamza nahisi ni njia rahisi kwenda kwa Mhe. Hamza ili kwenda kupeleka lalamiko langu lakini hata na yeye Mhe. Mwakilishi anapokuwa anaambiwa ile kesi ni vizuri kwa sababu wizara ipo kila siku wizara haipo kwa kipindi cha bajeti peke yake ni vizuri kama kuna malalamiko ambayo yeye kwa namna moja ama nyengine kapelekewa basi si vibaya na ni busara sana akaja nayo wizarani ili yaweze kufanyiwa kazi kulikoni kusubiri mpaka kipindi cha bajeti kwa sababu ule muda nao unaweza kuona unazidi kuwa umekaa yule mwalimu kule atakuwa anadhani kwamba lalamiko lake limeshafika kumbe Mhe. Mwakilishi ameliweka anasubiri muda wa bajeti ndo aje aliseme hapa. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Mwakilishi makini sana Mwenyeviti wa wenye viti wanapokuja walimu wetu basi washauri waje wizarani ili tuweze kuwatatulia matatizo yao. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti ndiyo yale niliyoyasema mwanzo unajua tatizo la kuisimamia serikali sisi mwaka mara moja kwa hivyo ina maana wengi wale wenye matatizo yao wanasubiri wakisikia tu bajeti imeanza ndo wanakuja na zile shida zao kwa sababu wanajua kile kipindi chengine chochote hata wakija mambo yanakuwa ni hivyo, lakini kimsingi Mheshimiwa nakushukuru na hii kwa sababu hawa wengine ndo kama hivyo wamekuja wizara ya elimu mpaka wameshindwa wakaamua kumuandikia barua mpaka Katibu Mkuu Kiongozi na kopi za barua zao ninazo. Sasa hili ndiyo nikasema kwamba wajitahidi *at least* kumalizana nao ili suala likae sawa, lakini nafirkiri kwa kuwa hii hoja si yangu ni hoja ya wananchi wenyewe walimu wameshasikia ambao wana malimbikizo basi waende kwenye wizara zao na wakiona kule wamekwama basi warudi kwa mtumishi wao wa umma ambae nimejitolea nafsi yangu

kuwatetea ili niweze kwamba tunasaidia kuzitetea haki zao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tayari wajumbe wameshatimia kwa hivyo hatuwezi tena kuongeza, kanuni zinasema ni wajumbe watatu kusimamia hoja.

Kifungu PK0106 Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Elimu	13,902,013,000
Jumla kuu	**179,605,900,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za Wizara yangu bila ya mabadiliko yoyote, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa naomba utoe hoja au umetoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante nyongeza haigombi. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka Fedha 2018
Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Mhe. Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Kipondi cha pili ni ndua na naomba maelezo yangu yatiwe kwenye Hansard kama yalivyo katika hotuba yangu kwenye maandishi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutanguliza shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa wenye afya njema, uwezo na nguvu za kuwatumikia wananchi wa Zanzibar katika hali ya amani, umoja na mshikamano. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe hekma, busara, uadilifu na mafanikio katika kujadili mambo muhimu ya Maendeleo ya Taifa letu na kusimamia utekelezaji pamoja na kuwatumikia wananchi wote.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake imara wenye busara na hekima ambao chini ya uongozi wake, Serikali inaendelea kutekeleza Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira 2020, *MKUZA III* na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020. Kupitia Mipango hiyo, Serikali inaendelea kuleta maendeleo makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa wananchi wa Zanzibar. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumjaalia afya, hekma na busara katika kuitumikia Zanzibar na watu wake.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuniteua kuwa Waziri katika Wizara mpya ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naahidi kwa kushirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa Lulu Msham Abdulla na watendaji wote tutahakikisha tunatekeleza kwa ufanisi malengo tuliojiwekea ili wananchi wa Zanzibar hasa vijana, wasanii na wanamichezo waendelee kunufaika na maendeleo yanayoletwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Chama Tawala Chama Cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii maalum kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kumsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kuiongoza nchi na kuleta manufaa kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kukupongeza na kukushukuru wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza Baraza lako Tukufu kwa mujibu wa sheria, taratibu, hekima, busara, uadilifu na uvumilivu mkubwa bila ya kuyumba katika kusimamia kanuni tulizojiwekea. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (Shihata) ambae

pia ni Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi wa jimbo la Kijitoupele pamoja na Makamo Mwenyekiti Mheshimiwa Salha Mwinjuma kupitia nafasi za vijana kwa kuisimamia Kamati hii kwa umahiri mkubwa. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hii, nawaahidi kwamba mimi binafsi, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na watendaji wangu wote tutaendelea kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwao kwa kipindi chote cha utekelezaji wa utendaji wa majukumu yetu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mabadiliko yaliyofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo inaundwa na Sekta kuu nne ambazo ni Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo zilizo chini ya taasisi 11 kama zifuatazo:-

i. Idara ya Utumishi na Uendeshaji;
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
iii. Ofisi Kuu Pemba;
iv. Idara ya Maendeleo ya Vijana;
v. Baraza la Vijana Zanzibar;
vi. Idara ya Utamaduni na Sanaa;
vii. Baraza la Kiswahili Zanzibar *(BAKIZA)* ;
viii. Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni *(BASSFU)* ;
ix. Afisi ya Msajili wa Hakimiliki *(COSOZA)* ;
x. Idara ya Michezo; na
xi. Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar *(BTMZ).*

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuchukua nafasi hii kutoa maelezo kuhusu bajeti ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Katika maelezo hayo nitaeleza uchambuzi wa mapato, matumizi, utekelezaji wa programu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na mwelekeo wa bajeti, vipaumbele na makadirio ya fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya Wizara yaliyofanyika hivi karibuni, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilibidi kutekeleza programu kuu tatu kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kama ifuatavyo:-

i. Programu ya Maendeleo ya Vijana;
ii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

iii. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikadiriwa kupata jumla ya shilingi 8,437,415,000/= kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tatu na miradi ya maendeleo ya Wizara. Kati ya hizo shilingi 2,339,915,000/= kwa kazi za kawaida na *shilingi* 6,097,500,000/= kwa kazi za maendeleo. Katika fedha za miradi ya maendeleo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikadiriwa kutoa shilingi 500,000,000 /= kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya na shilingi 5, 597,500,000/= kwaajili ya Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa China. Kwa upande wa mapato, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shillingi 124,303,000/= zinazo kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 80,000,000/= ni makusanyo ya mirabaha kwa ajili ya wasanii na wabunifu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha miezi tisa Julai - Machi 2018, jumla ya shilingi 1,831,745,797/= zilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 78 ya lengo la shilingi 2,339,915,000 /=. Aidha, Wizara ilikusanya kupitia Baraza la Sanaa ya Filamu na Utamaduni *(BASSFU)* na Baraza la Kiswahili *(BAKIZA)* shilingi 56,851,500/= sawa na asilimia 46 zilizoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikilinganishwa na lengo la shilingi 124,303,000/=. Vile vile, shilingi 75,496,565/= sawa na asilimia 94 ambazo ni makusanyo ya mirabaha ya wasanii na wabunifu ikilinganishwa na lengo la shilingi 80,000,000/=.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mishahara ya Idara zilizomo ndani ya Wizara jumla shillingi 1,035,075,290/= sawa na asilimia 86 ya lengo la shilingi 1,206,015,000/=. Taasisi zinazopokea ruzuku zilipata jumla ya shilingi 74,925,675/= ikiwa ni malipo ya mishahara ambapo ni sawa na asilimia 75 ya lengo la shilingi 100,000,000 /=.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa matumizi mengineyo jumla ya shilingi 419,200,424/= zilipatikana kwa Idara zilizomo ndani ya Wizara sawa na asilimia 70 ya lengo la shilingi 600,000,000/=. Vile vile, kwa taasisi zinazopata ruzuku zilipata jumla ya shilingi 302,544,408 sawa na asilimia 70 ya lengo la shilingi 433,900,000.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo zinazotokana na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jumla ya shilingi 500,000,000/= zimeshapatikana sawa na asilimia 100. Aidha, kwa upande wa msaada wa Ujenzi wa Uwanja wa Mao-Tse-Tung kutoka kwa ndugu zetu

wa Jamuhuri ya Watu wa China wenye jumla ya shilingi 5,597,500,000/= hadi kufikia Machi 2018, jumla ya shilingi 3,400,000,000/= sawa na asilimia 61 zilipatikana ambapo ujenzi wa uwanja huo unaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, uchambuzi zaidi wa fedha zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambazo ni shilingi 8,437,415,000 na zilizopatikana hadi kufikia Machi 2018 jumla ya shilingi 5,731,745,797 sawa na asilimlia 68 zimeainishwa katika **kiambatisho namba 1A hadi 1B.**

MAFANIKIO YA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.
Programu ya Maendeleo ya Vijana.

Mhe. Naibu Spika, program hii ilikuwa inapatikana katika Programu Kuu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi ndani ya Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana iliyokuwa ikitekelezwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii ilidhinishiwa jumla ya shilingi 427,363,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2018, imefanikiwa kupata shilingi 321,840,140/= sawa na asilimia 75 **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).**

Mhe. Naibu Spika, kifungu nambari 18 naomba kitiwe kwenye Hansard kama nilivyoleta kwa maandishi katika hotuba yangu.

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu hii ni kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana ikiwa ni pamoja na kuwawezesha vijana ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia programu mbali mbali. Programu hii inaundwa na programu ndogo moja nayo ni Maendeleo ya Vijana. Programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana pamoja na Baraza la Vijana Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kupitia program hii mafaniko yaliyopatikana ni kuendesha mafunzo ya stadi za maisha yaliyotolewa kwa vijana walio nje ya skuli. Vijana 2,053 kutoka Wilaya zote za Zanzibar walipatiwa mafunzo ya stadi za maisha. Pia, jamii imeelimishwa kupitia Vyombo vya Habari 17 juu ya umuhimu wa stadi za maisha kwa vijana 1,547 na washiriki 26 kutoka NGO's za Vijana.

Mhe. Naibu Spika**,** jumla ya vikundi 100 vya vijana (50 Unguja na 50 Pemba) wanaojishughulisha na shughuli za kiuchumi na kimaendeleo kwa Mikoa yote ya Zanzibar vimefuatiliwa kwa lengo la kufahamu mafanikio, fursa na changamoto zinazowakabili vijana katika shughuli zao za kila siku ili kuimarisha shughuli hizo. Miongoni mwa changamoto iliobainika ni kukosekana kwa vyanzo vya kudumu vya maji na maeneo ya kudumu kwa

shughuli za kilimo. Aidha, Idara imesaidia vikundi tisa vya vijana Unguja na Pemba kwa kuvipatia vifaa ikiwemo mashine za maji, vyerahani, mipira ya maji na vifaa vya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na Shirika la *Eqwip Hubs* Idara ya Maendeleo ya Vijana, iliadhimisha Siku ya Kimataifa ya Vijana tarehe 12/8/2017 kwa kufanya program mbali mbali ikiwemo siku ya mazoezi kwa vijana, usafi wa mazingira kwa kila Wilaya pamoja na kongamano siku ya kilele lilozungumzia ujumbe wa mwaka 2017 ambao ni *"Vijana ni Wajenzi wa Amani".*

Mhe. Naibu Spika, Idara imefanikiwa kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017 ambapo kilele kilifanyika Mkoa wa Mjini Magharibi; Mgeni Rasmi alikua Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania **Dkt. John Pombe Magufuli.** Aidha, kwa mwaka 2018, Uzinduzi wa Mwenge ulifanyika Mkoa wa Geita ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa **Kassim Majaliwa.** Ujumbe wa Mwenge kwa mwaka 2018 ni **"Elimu ni Ufunguo wa Maisha Wekeza sasa kwa Maendeleo ya Taifa Letu".**

Mhe. Naibu Spika, Bonanza la Vijana la kupaza sauti zao kupinga vitendo vya Ukatili na Unyanyasaji wa Wanawake, Wasichana, Watoto na siku 16 za Uwanaharakati limefanyika. Vile vile, Vijana wameelimishwa juu ya madhara ya Mimba za Umri Mdogo na Ndoa za Mapema kupitia kampeni ya kuwaepusha vijana wakike na mimba za umri mdogo kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba na jumla ya vijana 2,000 walifikiwa na kampeni hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mikutano ya uratibu ya kila robo mwaka imefanyika na wadau wa Vijana kwa lengo la kutoa fursa ya kutathmini shughuli za maendeleo ya Vijana na kuangalia huduma wanazotoa, walengwa wanaofikiwa pamoja na fursa zilizopo na changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa utoaji wa huduma na kupeana hatua za baadae.

Mhe. Spika, Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kuunda Sekretarieti ya Baraza la Vijana Zanzibar kwa kuajiri maafisa sita ambao watarahisisha utendaji kazi wa shughuli za Baraza. Aidha, kwa kushirikiana na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Baraza la Vijana Zanzibar limeweza kusimamia uendeshaji wa Mabunge ya Vijana ya Nchi za Jumuiya ya Madola ***"Common Wealth Parliamentary Association"*** *(CPA)* ambayo yalifanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi hapa Chukwani tarehe 12/3/2018.

Mhe. Naibu Spika, vifaa mbali mbali vimetolewa kwa Mabaraza ya Vijana ya Wilaya na Taifa katika kuyaimairisha ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi. Mabaraza ya Vijana ya Wilaya ambayo yamepatiwa vifaa hivyo ni Baraza la Vijana Wilaya ya Wete, Micheweni, Chake Chake

na Mkoani kwa Pemba. Kwa Unguja ni Wilaya ya Kati, Kaskazini "A", Kaskazini "B" na Magharibi "A".

Mhe. Naibu Spika, katika kuwajengea uwezo Vijana wa Zanzibar, jumla ya Vijana 2,549 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, stadi za maisha, uongozi, kilimo, uandishi wa habari, utunzaji fedha, elimu ya biashara, utalii, uibuaji wa fursa za kiuchumi na uendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Vijana Zanzibar limefanikiwa kuyaunganisha Mabaraza ya Vijana ya Wilaya saba na fursa mbali mbali kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Mabaraza yenyewe ni Baraza la Vijana Shehia ya Kiuyu Minungwini, Mgogoni, Pandani, Kiuyu Kigongoni na Kangani tayari wameshapatiwa mashamba na Serikali kwa ajili ya kilimo. Shughuli za kilimo wanazofanya ni kilimo cha mikaratusi, migomba, kilimo cha mboga mboga na mchai chai. Aidha, kikao cha pamoja kati ya Wizara, Wakuu wa Wilaya zote za Zanzibar, Wenyeviti wa Mabaraza ya Vijana Wilaya na Viongozi wa Baraza la Vijana Taifa kimefanyika ili kujenga ushirikiano wa pamoja kati ya taasisi hizi.

ii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utamaduni, Ubunifu na Sanaa ya Zanzibar inawainua wasanii kiuchumi na kupunguza umasikini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shillingi bilioni 1,912,552,000/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2018, jumla ya **shillingi bilioni 1,509,905,657/=** sawa na asilimia 79 zilipatikana. Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa pamoja na Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo.

Programu Ndogo 1: Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa inatekelezwa na taasisi zifuatazo: Idara ya Utamaduni na Sanaa, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 1,549,032,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2018, imefanikiwa kupata **shilingi bilioni 1,280,271,573/=** sawa na asilimia 83 na kutakiwa kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 204,303,000/=.** Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya **shilingi**

bilioni 132,348,065/= zimekusanywa sawa na asilimia 65 **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1Dna 1E).**

Mhe. Naibu Spika, kupitia programu ndogo hii, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kufanikisha Tamasha la 22 la Utamaduni wa Mzanzibari kwa ufanisi mkubwa ambapo shughuli za kiutamaduni kama hasa ngoma za asili, maonesho ya fensi, michezo ya watoto, mchezo wa ng'ombe, taarabu asilia na maonyesho ya wajasiriamali wa kazi za sanaa yalifanyika.

Mhe. Naibu Spika, katika kuutangaza utamaduni wa Zanzibar nje ya nchi, vikundi vitatu vya utamaduni vya taarab, ngoma na wajasiriamali vimefanikiwa kushiriki katika Tamasha la *JAMAFEST* nchini Uganda, Chama cha Waigizaji cha Zanzibar kimeshiriki katika Tamasha la 10 la Filamu Muscat Oman na wasanii 10 wa ngoma asilia wameshiriki katika Tamasha la Utamaduni nchini India.

Mhe. Naibu Spika, katika kuiendeleza na kuimarisha Nyumba ya Sanaa, wafanyakazi wamepatiwa vifaa vya uchongaji, uchoraji, mashine ya kuchapishia fulana na kofia. Pia vijana 4 wa fani ya uchapishaji wamepatiwa mafunzo ili kuwajengea uwezo juu ya kazi za sanaa na kuweza kujiajiri wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni kwa kushirikiana na Idara ya Michezo na Utamaduni ya Wizara ya Elimu limefanikiwa kuandaa programu ya uibuaji na uendelezaji wa vipaji kwa kuwashindanisha wanafunzi wa elimu ya msingi katika sanaa za maigizo na uchoraji ambapo skuli 18 za msingi, katika Wilaya tatu ambazo ni Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharib "A" na Wilaya ya Magharib "B" zimeshiriki katika mashindano hayo kwa awamu ya kwanza. Aidha, mafunzo kwa walimu wakuu na wale wanaofundisha somo la utamaduni na sanaa katika skuli teule za msingi kwa Unguja na Pemba yametolewa.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya wasanii 50 wa filamu na maigizo wamepatiwa mafunzo ya wiki mbili kwa kushirikiana na Chuo Cha Uandishi wa Habari Zanzibar kwa lengo la kuwajengea uwezo wasanii wa filamu katika mbinu za uandishi wa *"script",* ujengaji na ubunifu wa wahusika, ubunifu wa mandhari pamoja na kujifunza historia ya chimbuko la uigizaji na maendeleo yake. Vile vile Kikundi cha Taifa cha Taarabu kiliwezeshwa kuandaa onyesho la taarab kwa lengo la kujitangaza.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya wasanii 14 wa sanaa ya maigizo wa zamani wametembelewa, wamehojiwa na kuwekewa taarifa zao kwa utaratibu maalum. Miongoni mwa wasanii hao ni Bi. Khadija Ibrahim (Bi Hawa), Bi. Asha Khatib Hassan, Bi. Mwema Kh. Omar ambaye pia anaitwa (Bi njiwa), Bw. Khamis Mikidadi, Bw. Makame K. Mtwana (Mfupa), Bw. Juma Haji Khamis

(Halikuniki) na Bi Fatma Mlenge (Shangazi). Taarifa hizo zitahifadhiwa na kutumika kwa maendeleo ya sanaa na wasanii nchini na kuwaenzi wasanii hao.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya vipindi 12 vya sanaa vimefanikiwa kurushwa hewani kupitia ZBC Redio, Chuchu FM, na Zenj FM kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sanaa za asili na utamaduni wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya vikundi 23 vya sanaa na utamaduni vimesajiliwa upya kwa ajili ya kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za BASSFU, aidha jumla ya filamu 344 za maonyesho zimekaguliwa kwa lengo la kuhakikisha haziendi kinyume na maadili ya Zanzibar. Vile vile, kazi za sanaa 40 zimerikodiwa kupitia Studio ya Filamu na Mziki iliyopo Rahaleo zikiwemo vikundi vya ngoma za asili, kizazi kipya, kasida, mashairi pamoja na nyimbo za taarab.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa jumla ya filamu 150 za nchi Wanachama wa Afrika Mashariki zilihakikiwa ambazo ziliingia katika mashindano ya **"FILAMU ZETU"** yaliyofanyika Dar-es-Salaam, katika tunzo 10 zilizokuwa zikiwaniwa tunzo nne zilichukuliwa na filamu zetu za Zanzibar na filamu iliyofanya vizuri zaidi ni **"Binti wa Zanzibar"**. Wizara inapenda kuwapongeza wasanii kwa kazi nzuri wanazozifanya hadi kupelekea kupatikana kwa tunzo hizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Kiswahili Zanzibar limefanikiwa kusambaza jumla ya Makamusi 7,548 katika skuli zote za Serikali za Unguja na Pemba, pamoja na taasisi za Serikali ili kusaidia jamii kutumia Kiswahili kwa ufasaha na usanifu.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya vipindi 51 vimerushwa hewani kupitia ZBC TV na Redio, Zanzibar Cable 2 TV, Hits FM, Bomba FM, Chuchu FM, na Swahiba FM. Miongoni mwa mada zilizojadiliwa ni: Uundaji wa Maneno na Istilahi za Kiswahili, Utandawazi unavyokuza Kiswahili na Mchango wa Vyombo vya Habari, katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Vile vile, Baraza linaendelea kutoa huduma za Maktaba kwa wanafunzi kutoka skuli na Vyuo Vikuu vya Zanzibar na Tanzania Bara. Jumla ya wanafunzi 193 walihudhuria wakiwemo wanawake 116 na wanaume 77. Aidha, mafunzo kwa Waandishi wa Habari juu ya Matumizi Sanifu na Fasaha ya Lugha ya Kiswahili yametolewa.

Mhe. Naibu Spika, Baraza limeendelea kutangaza na kuuza machapisho ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar ambapo jumla ya machapisho 140 yameuzwa yakiwemo Machapisho ya Kamusi la Kiswahili fasaha, Kamusi la Lahaja ya Kipemba, Kamusi la Lahaja ya Kimakunduchi,

Kamusi la Lahaja ya Kitumbatu, Kitabu cha Kiswahili kwa Wageni na Kitabu cha Utamaduni wa Mzanzibari.

Mhe. Naibu Spika, Baraza limefanikiwa kuandaa Kongamano la Kimataifa la Kiswahili lililofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdul wakil ambalo lilihusisha wataalamu wa Kiswahili kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Zimbabwe, Marekani, Uganda, Kenya na Tanzania Bara. Katika kuadhimisha Siku ya Kiswahili Zanzibar, Baraza limefanikiwa kutekeleza shughuli mbali mbali zikiwemo kutoa mafunzo kwa walimu wa Somo la Kiswahili. Jumla ya walimu 120 walishiriki kutoka skuli mbalimbali za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Baraza limeshiriki katikaTamasha la Utamaduni wa Mzanzibari na Tamasha la Biashara lililofanyika Zanzibar kwa lengo la kutangaza na kuuza vitabu vya BAKIZA. Katika makongamano hayo, Baraza limeshiriki katika uwasilishaji wa makala na mijadala ya taaluma za Kiswahili, kuuza machapisho pamoja na kulitangaza Baraza na kazi zake. Pia Baraza linaendeleza kuandika jarida la BAKIZA ambalo huhusisha makala za taaluma ya Kiswahili katika Isimu na Fasihi.

Mhe. Naibu Spika, katika kukuza na kusambaza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar, Baraza la Kiswahili Zanzibar limeshiriki katika matamasha na makongamano mbali mbali, miongoni mwao ni Kongamano la Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA), Kongamano la Kimataifa la Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki pamoja na Kongamano la Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA). **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 4).**

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki imefanikiwa kusajili jumla ya kazi za hakimiliki 511 na kuingizwa katika mfumo wa kielekroniki kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na kuwa na takwimu ya kazi zilizosajiliwa na takwimu ya wafaidikaji wa mirabaha. Aidha, kanuni tatu za usimamizi wa masuala ya Hakimiliki zimekwishaandaliwa. Kanuni hizo ni Kanuni ya Usimamizi wa Kazi za Maandishi, Kanuni ya Usajili wa Kazi na Wanachama na Kanuni na Utaratibu Maalum wa Usuluhishaji au Usuluhishi wa Masuala ya Hakimiliki. Kanuni hizo zinatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji, mirabaha yenye thamani ya **Shilingi milioni 75,496,565/=** ilikusanywa kutoka kwa watumiaji mbali mbali wa kazi za hakimiliki kibiashara na utaratibu wa kuzigawa kwa wenye hakimiliki wapatao 1,237 umeanza kufanyika ambapo kwa wastani kikundi au msanii anapata wastani wa chini **shilingi elfu 50,000/=** na wastani wa juu zaidi **Shilingi milioni 2,000,000/=.**

Mhe. Naibu Spika, wabunifu na wasanii wagonjwa 33 wamefikiwa katika maeneo yao kwa Unguja na Pemba, na kuwapatia kiasi cha fedha kinachotokana na eneo maalum la mirabaha ambapo jumla ya **Shilingi milioni 3,300,000/=** zilitumika kwa shughuli hiyo. Hata hivyo bado kuna changamoto ya mwitikio mdogo wa ulipaji mirabaha na kuheshimu haki za matumizi ya hakimiliki kibiashara kwa baadhi ya watumiaji hasa vituo vya Utangazaji. Kuna jumla ya wastani wa **shilingi milioni 105,000,000/=** hazijawasilishwa na taasisi zikiwemo ZBC TV na Redio TV, Coconut Redio na TV, Zenj FM, Bomba FM, Bahari FM pamoja na Marashi TV. Hatua zilizochukuliwa ni kuiandikia barua Tume ya Utangazaji, ikiwa ndio msimamizi wa vyombo vya habari Zanzibar ili wafanye malipo.

Mhe. Naibu Spika, katika kupunguza uharamia wa hakimiliki, Afisi imefanikiwa kufanya ukaguzi katika maeneo mbali mbali ya wauzaji kazi za hakimiliki. Watumiaji 80 wa kazi za Hakimiliki kibiashara wamekaguliwa wakiwemo wenye maduka ya kuuza na kukodisha kazi za vinasa sauti vya kusikia na kuonekana.

Mhe. Naibu Spika, mikutano minne ya mafunzo kwa wahusika mbali mbali wa Hakimiliki ilifanyika, ambapo jumla ya wadau 300 wakiwemo wasanii na wabunifu walihudhuria ikiwemo mkutano wa mafunzo juu ya mikataba kwa wasanii na wabunifu kwa Unguja na Pemba. Mkutano wa mafunzo juu ya uharamia wa hakimiliki. Aidha, Afisi kwa kushirikiana na Shirika la Milki Bunifu Ulimwenguni *(World Intellectual Property Organisation - WIPO)* walifanya mafunzo juu Usimamizi wa hakimiliki katika mazingira ya kidijitali. Mafunzo hayo ni kwa ajili ya kuwaelewesha wamiliki na watumiaji wa kazi za hakimiliki athari za mazingira ya kidijitali kwa matumizi ya hakimiliki.

Mhe. Naibu Spika, vipindi 22 vya elimu juu ya masuala ya Hakimiliki vilirushwa hewani kupitia televisheni ya Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), televisheni ya “Zanzibar Cable” na kituo cha redio cha “HITS FM”, kwa lengo la kuwaelimisha watumiaji wa kazi za hakimiliki, wamiliki na jamii kwa jumla juu ya haki za wabunifu na wasanii pamoja na umuhimu wa kulipia Mirabaha kwa matumizi ya hakimiliki kwa lengo la kuinua kipato cha wabunifu, wasanii na Taifa kwa ujumla.

Programu Ndogo 2: Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa michezo inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo: Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ). Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, iliidhinishiwa jumla ya shillingi 363, 520,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2018, imefanikiwa kupata shilingi 229,634,084/= sawa na asilimia 63.

(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).

Mhe. Naibu Spika, Wizara imefanikiwa kuiwezesha Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Zanzibar *(Zanzibar Heroes)* kushiriki mashindano ya CECAFA nchini Kenya nakupata nafasi ya pili. Aidha, Timu ya Taifa ya *Zanzibar Beach Soccer* imeshiriki katika mashindano ya *Beach Soccer* ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Dar – es – Salam na timu hiyo ilipata ushindi wa kwanza.

Mhe. Naibu Spika, Chama cha Watu Wenye Ulemavu wa Uziwi kimefanikiwa kushiriki katika mkutano wa Kimataifa kwa nchi za Afrika Mashariki nchini Kenya na kwa upande wa mchezo wa riadha wachezaji 20 wameshiriki mashindano ya kimataifa ya *Youth East and Central Africa Championship* yaliyofanyika Dar es saalam.

(Tafadhali angalia kiambatisho namba 3).

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mafunzo ya kimataifa, Idara imewasaidia makocha watatu wa Chama cha *Base Ball* kushiriki mafunzo ya mchezo wa *Baseball* yaliyotolewa na wataalamu wa shirikisho la michezo ya *Baseball* na *Softball l*a Dunia yaliyofanyika Mwanza. Pia wanamichezo wawili wa mchezo wa Taekwondo wameshiriki semina ya mchezo huo iliyofanyika nchini Uganda. Vile vile, mchezaji mmoja wa riadha amewezeshwa kushiriki mafunzo ya mchezo wa riadha yaliyofanyika nchini Brunei.

Mhe. Naibu Spika, katika uimarishaji wa viwanja vya michezo, Uwanja wa Amani umewekewa uzio wa matofali na kuufanyia matengenezo madogo madogo. Aidha, ujenzi wa kiwanja cha Kitogani umekamilika kwa hatua ya awali na wananchi wa Kitogani na Mkoa wa Kusini kwa ujumla wanakitumia kiwanja hicho katika shughuli za michezo. Vile vile, kwa kushirikiana na wadau wa michezo Idara imefanikiwa kuandaa Tamasha la Siku ya Mazoezi ya Viungo lililofanyika tarehe 01/01/2018 katika Uwanja wa Amaan na mgeni Rasmi alikuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kuviwezesha vyama tisa vya michezo kushiriki na kuandaa mashindano mbali mbali ya ndani na ya kimataifa. Miongoni mwa vyama hivyo ni Chama cha Mchezo wa Netiboli kimefanikiwa kundaa mashindano ya ligi kuu ya Muungano. Chama cha Judo kimeweza kushiriki mashindano ya *Tanzania Budokan Cup* yaliyofanyika Dar es salam sambamba na kuandaa mashindano ya Zanzibar Budokan yaliyofanyika Zanzibar.

(Tafadhali angalia kiambatisho namba 3).

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mafunzo, Baraza limeweza kusaidia vyama sita vya michezo kuandaa na kushiriki katika mafunzo ya uamuzi na ukocha katika mchezo wa Netiboli, *Basketball, Volleyball*, Riadha, *Baseball* na Kuogelea.

Mhe. Naibu Spika, katika kusimamia utekelezaji wa Sheria Namba 5 ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ya mwaka 2010, Baraza limeviwezesha vyama vitano vya michezo *ya*

Basketball, Netiboli, Squash, Table tennis na Handball kufanya uchaguzi wa kuwapata viongozi watakaoviongoza vyama hivyo kwa mujibu wa katiba za vyama vyao.

Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, programu ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu imeundwa na programu ndogo tatu nazo ni programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara na programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya kiwizara, fedha za programu kuu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo sambamba na fedha za programu ndogo tatu zilizoidhinishwa na Baraza lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 zinasomeka katika programu kuu na ndogo katika kitabu cha Hotuba ya Bajeti cha Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale cha mwaka wa fedha 2018/2019.

Programu ndogo 1: Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, katika kusimamia majukumu ya kiutendaji ya kuratibu na kusimamia utawala na uendeshaji, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imefanikiwa kufanya ziara za kikazi katika taasisi zilizopo chini ya Wizara na kushiriki katika uzinduzi wa Mwenge kitaifa uliofanyika Geita. Aidha, viongozi na watendaji wameshiriki katika makongamano, mikutano na warsha tofauti nchini Afrika Kusini na Comoro.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya wafanyakazi sita katika ngazi na fani tofauti wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa lengo la kukuza, kuongeza ufanisi na utendaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku.

(Tafadhali angalia kiambatisho namba 2).

Mhe. Naibu Spika, Idara katika kuimarisha mazingira mazuri ya kazi imeweza kuzipatia Ofisi zake vitendea kazi na vifaa mbali mbali kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika kazi. Aidha, Kitengo cha Ukaguzi wa hesabu za Ndani kimetayarisha ripoti za fedha na ukaguzi kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha. Pia, Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kimeanza utayarishaji wa Mpango wa Manunuzi wa mwaka pamoja na Mpango wa Matumizi ya Fedha kwa ajili ya kuwa na utaratibu wa manunuzi ambao utafatwa na taasisi zote zilizo chini ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, Idara imeweza kutayarisha na kusimamia vikao vya Kamati Tendaji ya Wizara kwa ajili ya kujadili shughuli mbali mbali za Wizara ikiwemo matayarisho ya bajeti mpya ya mwaka 2018/2019.

Programu Ndogo 3: Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini mipango, sera, tafiti na miradi ya maendeleo ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, Rasimu ya Sera ya Utamaduni na Sera Filamu imeshawasilishwa kwa wadau na kujadiliwa ili kupata maoni kuhusiana na sera hizo. Sera hizo zinatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Kamati Tendaji ya Wizara kwa ajili ya kujadiliwa na kupatiwa michango ya kuimarisha rasimu hizo kabla ya kuendelea na utaratibu wa kuziwasilisha katika ngazi husika ili ziweze kupitishwa.

Mhe. Naibu Spika, Idara kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) imefanya uchambuzi yakinifu wa uanzishwaji wa Sera ya Lugha, uchambuzi huo umesaidia kujua maeneo ambayo yatakuwepo kwenye sera na kuwekewa mikakati ya kiutekelezaji. Ripoti ya Utafiti huo imekamilika. Aidha, ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara ili kujua utekelezaji halisi wa miradi hiyo umefanyika. Miradi iliyokaguliwa na ripoti zake za utekelezaji kuwasilishwa Tume ya Mipango katika kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini ni Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Michezo cha Mao-Tse-Tung kilichopo Mpirani na Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Wilaya Kitogani.

Mhe. Naibu Spika, taarifa za utekelezaji wa shughuli za Wizara pamoja na miradi ya maendeleo zimetayarishwa na kuwasilishwa kwa wakati. Aidha, Idara ipo katika hatua ya utaarishaji wa Mpango Mkakati wa Kitakwimu kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji takwimu katika maeneo ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara *(Strategic Plan).*

Programu Ndogo 3: Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba ambayo inajukumu la kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kuratibu ziara za wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, walipotembelea maeneo ya miradi na taasisi mbali mbali za Wizara kwa upande wa Pemba pamoja na kuwatembelea wanamichezo na Wasanii Wakongwe. Aidha, imeweza kuratibu kikao cha wadau cha kujadili Sera ya Utamaduni na Filamu, Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari pamoja na kuratibu mkutano wa wadau wa Utamaduni. Vikao na mikutano ya kiutendaji

imefanyika ya kuibua vipaji vya michezo na sanaa katika skuli teule. Vile vile, Kamati za Sanaa za Wilaya na maafisa mbali mbali wa michezo wamepatiwa mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana wanafunzi 30 na wasiokuwa wanafunzi 200 na mafunzo ya kiuchumi pamoja na kusaidia wajasiriamali wanane yamefanyika sambamba na ufuatiliaji na usimamizi wa Ujenzi wa Viwanja vipya vya Michezo vya Wilaya kwa Pemba. Kwa upande wa Uwanja wa Gombani, marekebisho yamefanyika kwa kutengeneza na kutia rangi majukwaa pamoja na maeneo ya ndani na nje ya jukwaa la Wageni Mashuhuri (VIP).

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imefanikiwa kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung na Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung ulipangiwa jumla ya shilingi 5,597,500,000/= ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Hadi kufikia Machi, 2018, mradi huu umeshaingiziwa jumla ya shilingi 3,400,000,000/= sawa na asilimia 61 ya fedha zilizotengwa

(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1A).

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu ulipangiwa jumla ya shilingi 500,000,000/= na hadi kufikia Machi, 2018 mradi huu umeshaingiziwa jumla ya shilingi 500,000,000/= sawa na asilimia 100.

(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1A).

Mhe. Naibu Spika, hatua za ujenzi wa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung unaendelea vizuri kwa kushirikiana na Mkandarasi wa Kampuni ya Zhengtai Group Co, Ltd kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Shughuli ambazo zimeshatekelezwa hadi sasa ni kukamilisha kiwanja kimoja kwa uwekaji wa nyasi bandia katika kiwanja cha kuchezea mpira wa miguu, ukamilishaji wa kiwanja cha michezo mchanganyiko na michezo ya ndani *(Indoors game)*, kiwanja kwa ajili ya mazoezi ya viungo *(gym)*, ujenzi wa vyoo 48, majukwaa ya Wageni Mashuhuri (VIP) na yawatizamaji wa kawaida pamoja na Ofisi mbili. Maeneo yote hayo yameshajengwa na hatua iliyobaki ni upakaji wa rangi na ufungaji wa vifaa. Aidha, kazi ya ukamilishaji wa kiwanja cha pili cha kuchezea mpira wa miguu umeshaanza na umefikia katika hatua nzuri. Vile vile, ujenzi wa sehemu za pembezoni mwa uwanja “edges” pamoja na ukuta unaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mradi huu wa Ujenzi wa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung unatarajiwa kukamilika mwezi wa Oktoba mwaka huu pamoja na changamoto za ukosefu wa mchanga uliojitokeza awali ambapo kazi zilisimama kwa miezi miwili na mvua kubwa iliyonyesha mwaka huu.

Wakandarasi wetu wanaendelea na jitihada ili kukamilisha kazi hizo kabla ya mwisho wa mwezi Oktoba, 2018.

Mhe. Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya vinatarajiwa kujengwa Kishindeni Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kangani Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba. Shughuli ambazo zimefanyika hadi sasa ni kufanyika kwa upembuzi yakinifu wa mradi huo na utayarishaji wa makisio ya Ujenzi (BOQ) ya viwanja hivyo, kwa sasa Wizara ipo katika hatua ya kutafuta wakandarasi. Kuchelewa kuanza ujenzi wa viwanja hivi kulisababishwa na kutopatikana kwa wakati maeneo husika.

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo imepangiwa jumla ya shilingi 7,411,600,000/= Kati ya fedha hizo shilingi 3,611,600,000/= kwa matumizi ya kawaida na shilingi 3,800,000,000/= kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa fedha za matumizi ya kazi za kawaida jumla ya shillingi 1,582,800,000/= ni mishahara ambapo shillingi 1,480,900,000/= ni mishahara ya Idara za ndani ya Wizara na shillingi 101,900,000/= ni mshahara kwa taasisi zinazopokea ruzuku. Kwa upande wa matumizi mengineyo jumla ya shillingi 2,028,800,000/=, kati ya hizo matumizi mengineyo kwa Idara za Wizara ni jumla ya shillingi 1,462,000,000/= na kwa taasisi zinazopokea ruzuku ni jumla ya shillingi 566,800,000/=

Mhe. Naibu Spika, katika fedha za miradi ya maendeleo Wizara imepangiwa jumla ya shilingi 3,800,000,000/= kwa ajili ya Programu ya Ajira kwa Vijana ambayo ni shillingi 3,000,000,000/= na Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya shillingi 800,000,000/= .

Mhe. Naibu Spika, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shillingi 187,670,000/= kati ya hizo jumla ya shillingi 97,670,000/= kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ni makusanyo yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na jumla ya shillingi 90,000,000/= ni makusanyo ya mirabaha.

(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F, 1H, 1I).

MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA FEDHA 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, Wizara imejipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:-

i. Kuandaa programu za kuwawezesha vijana kiuchumi na kujiajiri,
ii. Kufanya tafiti katika maeneo ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo,
iii. Kuandaa matamasha ya utamaduni na michezo na kuviwezesha vikundi kushiriki matamasha ya kitaifa na kimataifa,

iv. Kuibua, kuendeleza na kusimamia sanaa, wasanii na wabunifu,
v. Ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya na kuziwezesha timu kushiriki na kuandaa mashindano, na
vi. Kukamilisha Sera ya Filamu na Sera ya Utamaduni na kutayarisha Sera ya Lugha.

5.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUBWA NA NDOGO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo tunaomba tuidhinishe tutumie jumla ya **shilingi 7,411,600,000/=** kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu tatu ambazo ni:-

i. Programu ya Maendeleo ya Vijana **(Shilingi 457,448,000/=);**

ii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo **(Shilingi 2,049,626,000 /=);** na

iii. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni Sanaa na Michezo tutahitaji **(Shilingi 4,904,526,000/=). (Tafadhali angalia kiambatisho namba 1G, 1H na 1I).**

1. Programu Kuu: S0101 Maendeleo ya Vijana.

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu hii, ni kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana ikiwa ni pamoja na kuwawezesha vijana ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia programu mbali mbali. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuengeza idadi ya ajira kwa vijana kwa kuwawezesha ikiwemo kuwajengea uwezo kupitia programu mbali mbali. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 457,448,000/=** na imepangiwa kusimamia programu ndogo moja:-

i. Programu Ndogo: SS010101 Maendeleo ya Vijana (Shilingi 457,448,000/=).

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana itatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:-

Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana Zanzibar ambapo jukumu la msingi katika Programu ndogo ni kuwawezesha Vijana ili kujenga uchumi na maendeleo ya jamii. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia shughuli za Maendeleo

ya Vijana, kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, kusimamia uendeshaji wa Mabaraza ya Vijana katika ngazi zote, kuyawezesha Mabaraza ya Vijana kiuchumi ili yajiendeleze na kukuza ajira kwa Vijana.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia malengo ya programu hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kutoa mafunzo na kusaidia makundi ya Vijana katika shughuli za Kilimo, Uvuvi, Biashara, Elimu ya stadi za hasa stadi za maisha na amali ili kuwawezesha kiuchumi na kijamii;
ii. Kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru kitaifa;
iii. Kuyawezesha Mabaraza ya Vijana kuwa na Ofisi, Wafanyakazi na vifaa;
iv. Kuwezesha kufanyika mikutano yote ya Mabaraza ya Vijana kwa mujibu wa sheria iliopo pamoja na kuwajengea uwezo Vijana ili waweze kushiriki katika ngazi za kutoa maamuzi Serikalini na katika Sekta binafsi; na
v. Kuimarisha huduma, vifaa, Elimu na mazingira bora ya kazi kwa Taasisi zinazotekeleza programu hii.

Mhe. Naibu Spika, ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 457,448,000/=** kwa kazi za kawaida.

2. Programu Kuu: S0102 Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa utamaduni na Sanaa ya Zanzibar inawaendeleza wasanii kiuchumi ili kupunguza umasikini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa, uhifadhi wa utamaduni na kukuza michezo. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 2,049,626,000 /=** na itakuwa na programu ndogo mbili.

i. Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu utahitaji **(shilingi 1,681,226,000/=);** na
ii. Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo **(shilingi 368,400,000 /=).**

Programu Ndogo: SS010201 Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa itatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo: Idara ya Utamaduni, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki. Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kusimamia, kuratibu, kuimarisha, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za utamaduni na sanaa Zanzibar.

Kwa ruhusa yako na kuomba Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 93 ambacho nimekwisha kukueleza kitiwe kwenye *Hansard* kama kwenye Hotuba yangu ya maandishi.

Mhe. Naibu Spika, huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za sanaa na wasanii, kurikodi kazi za sanaa kupitia Studio ya Filamu na Muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi fasaha ya Kiswahili, usimamizi wa hakimiliki pamoja na ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wenye hakimiliki.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia malengo ya programu ndogo hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuandaa, kusimamia na kuratibu matamasha yote ya kiutamaduni pamoja na kulinda mila, desturi na silka za Wazanzibari, kwa kushirikiana na jamii;
ii. Kusimamia, kuhamasisha pamoja na kutoa elimu kuhusiana na matumizi bora ya lugha ya Kiswahili na lahaja zilizopo;
iii. Kukiimarisha kikundi cha Taarabu cha Taifa pamoja na vikundi vya Sanaa;
iv. Kuwasaidia wasanii kwa kuwapa mafunzo, kuwaendeleza kiuchumi, kuendelea kuitumia Studio ya Mziki na Filamu pamoja na kuwawekea mazingira bora ya kukuza sanaa zao;
v. Kusajili, kusimamia pamoja na kulinda kazi na haki za wasanii na wabunifu wa kazi mbali mbali pamoja na kuwapatia mirabaha yao; na
vi. Kuimarisha huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa taasisi zinazotekeleza programu ndogo hii.

Mhe. Naibu Spika, ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 1,681,226,000/=** kwa kazi za kawaida na makusanyo jumla ya **shilingi 97,670,000/=** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia, makusanyo ya **shilingi 90,000,000/=** ambazo hukusanywa na taasisi ya Hakimiliki kwa ajili ya Mirabaha ya wasanii na wabunifu.

Programu Ndogo: SS010202 Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya ukuzaji na uendelezaji wa michezo itatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo:-

Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo. Jukumu la msingi katika programu ndogo ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa nchini. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo kupitia Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza programu ndogo hii kwa ufanisi, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuendeleza michezo kwa kuziwezesha timu kushiriki na kuandaa mashindano ya kitaifa na kimataifa pamoja na kuvisaidia vyama vyote vya michezo;
ii. Kuimarisha miundombinu ya michezo kwa kufanya ukarabati wa Uwanja wa Amani, Gombani pamoja na kuandaa bonanza ya siku ya mazoezi ya viungo;
iii. Kuandaa mafunzo ya kitaifa na kimataifa kwa waamuzi, makocha, viongozi na wanamichezo; na
iv. Kuimarisha huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa taasisi zinazotekeleza programu hii ndogo.

Mhe. Naibu Spika, ili programu ndogo iweze kufanya kazi zake katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 368,400,000 /=** kwa kazi za kawaida.

3. Programu Kuu: S0103 Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na kuratibu na kusimamia utawala na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa usimamizi bora wa mipango na uendeshaji wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 4,904,526,000/=** na itasimamia programu ndogo tatu.

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. **(shilingi 3,952,000,000/=);**
ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo **(Shilingi 842,526,000/=);** na
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. **(Shilingi 110,000,000 /=).**

Programu Ndogo: SS010301 Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya Wizara kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika nataka kifungu namba 100 kwa kujitosheleza kitiwe kwenye Hansard kama kilivyo katika Hotuba yangu ya maandishi, ambayo itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kuratibu, kufuatilia na kutathmini mipango, sera, tafiti na miradi ya maendeleo ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni utaratibu au uratibu wa sera na tafiti, kuratibu na kuandaa bajeti ya Wizara na kuratibu mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia malengo ya programu ndogo hii shughuli zifuatazo zimepangiwa kutekelezwa:-

i. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Vijana, Sera ya Utamaduni, Sera ya Filamu pamoja na kutayarisha Sera ya Lugha;
ii. Kuratibu na kusimamia tafiti za Wizara katika maeneo ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
iii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Wilaya na Programu ya Ajira kwa Vijana;
iv. Kuandaa Bajeti, mipango ya Wizara pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi, programu na shughuli za Wizara; na
v. Kuimarisha huduma, vifaa, elimu na mazingira bora ya kazi kwa taasisi zinazotekeleza programu ndogo hii.

Mhe. Naibu Spika, ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 3,952,000,000/=,** ikiwa **shillingi 152,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilling 3,800,000,000/=** kwa kazi za maendeleo, ambapo jumla ya **shilling 3,000,000,000/=** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Ajira kwa Vijana na **shillingi 800,000,000/=** ni za Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya.

Programu Ndogo: SS010302 Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo itatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za Utumishi na Uendeshaji wa Wizara.

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali Watu. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia malengo ya programu ndogo hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia vifaa, huduma muhimu pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao;
ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa mujibu wa kada zao ili kufanya kazi kwa ufanisi;
iii. Kuratibu shughuli na ziara za kikazi za viongozi Kitaifa na Kimataifa;
iv. Kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya Mkakati Wakupambana na Rushwa hapa Zanzibar; na
v. Kuandaa na kusimamia Mpango wa Manunuzi wa Wizara.

Mhe. Naibu Spika, ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 842,526,000/=** kwa kazi za kawaida.

Programu Ndogo SS010302: Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango itatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Programu ndogo hii ina jukumu la kuhakikisha mipango, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zitatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kifungu 109, naomba kiingie katika Hansard kama kilivyo katika Hotuba yangu ya maandishi, lengo kuu la programu ndogo ni kusimamia na kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera, tafiti na mipango mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba, kuratibu miradi ya maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia malengo ya programu ndogo hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia vifaa, huduma muhimu pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa Ofisi Kuu Pemba;
ii. Kuratibu shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba;
iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi;
iv. Kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya Masuala Mtambuka;
v. Kuwapatia mafunzo viongozi wakuu wa Idara za Pemba kuhusu Sera na Mipango mikuu ya Wizara; na
vi. Kusimamia shughuli za miradi inayotekelezwa huko Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 110,000,000/=** kwa ajili ya kazi za kawaida.

SHUKRANI

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalumu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Bi. Lulu Msham Abdalla, Katibu Mkuu Nd. Omar Hassan Omar, Naibu Katibu Mkuu Nd. Amour Hamil Bakari, Makatibu Watendaji, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Wakuu wengine wa Taasisi za Wizara na wasaidizi wao pamoja na wafanyakazi wote kwa kufanyakazi kwa juhudi, maarifa, uadilifu na umakini mkubwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nakuomba kifungu cha 113, kuruhusu kiingie kwenye Hansard kama nilivyoandika kwenye Hotuba yangu kwa sababu hizi ni shukurani tu ambazo nazitoa kwa watu mbali mbali na Taifa na Kimataifa, naomba kuwashukuru Vijana wote, wanamichezo, wasanii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za Wizara yangu. Pia shukurani za pekee ziende kwa Vyombo vya Habari vya Serikali na Binafsi kwa kufanikisha kurusha vipindi mbali mbali vya kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Vijana, Utamaduni na Sanaa na habari za michezo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa kwa mahitaji ya fedha na ushauri katika kurahisisha utekelezaji wa mipango ya Wizara. Vile vile, ninazishukuru Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mashirika, Taasisi binafsi kwa mashirikiano makubwa waliotupatia.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu pia nizishukuru nchi mbali mbali na Mashirika kadhaa ya kimaendeleo ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Comoro, Afrika ya Kusini, Uganda, Ubalozi mdogo wa India, Ubalozi mdogo wa Oman, Shirika la Idadi ya Watu na

Maendeleo (*UNFPA*), Shirika la Eqwip Hubs, Shirika la Milki Bunifu Ulimwenguni yaani *(World Intellectual Property Organisation – WIPO),* na Washirika wote wa Maendeleo tunaoshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kukushukuru tena wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini mkubwa. Ni ukweli usiopingika kwamba mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii yamewezekana kutokana na ushirikiano wenu.

Naomba kuleta kwa kibali chzako Mhe. Naibu Spika maombi ya fedha kwa utekelezaji wa programu za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, naliomba Baraza lako Tukufu kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya shilingi 7,411,600,000/=. Kati ya hizo shilingi 3,611,600,000/= kwa Kazi za Kawaida, shilingi 3,800,000,000/= kwa Utekelezaji Miradi ya Maendeleo ya Wizara ambapo na shilingi 3,000,000,000/= kwa Programu ya Ajira kwa Vijana na shilingi 800,000,000/= kwa Ujenzi wa Viwanja vya Wilaya. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya mapato ya shilingi 97,670,000/= kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia, makusanyo ya mirabaha shilingi 90,000,000/=.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie bajeti hii ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

VIAMBATANISHO

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe Mheshimiwa ametoa hoja wale wanaokubaliana na hoja, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Naibu Spika naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba nitampisha Mwenyekiti aendelee na shughuli yetu hii ya leo lakini kabla ya kuendelea kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwanza kupitisha bajeti yake lakini vile vile kwa kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe vizuri sana na kuweza kutupa matumaini katika mwaka 2018/2019 wa utekelezaji wa bajeti yake. Mhe. Waziri hongera sana.(*Makofi*).

Lakini niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mijadala yenu ambayo mumeitoa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali lakini kwa hoja zenu ambazo mumezileta hapa mbele na naamini sisi sote tunajenga nyumba moja, yale ambayo yanajitokeza kwa kweli ni kwa sababu tunataka kujenga na kuona wananchi wetu tunaweza kuwatumikia vizuri na kuleta maendeleo ya taifa letu.

Kwa hivyo niwapongeze nyote vile vile kwa shughuli ambayo mumeifanya kwa ajili ya kupitisha bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa kabla ya kumalizia na kumpisha Mhe. Mwenyekiti naomba niwakaribishe wageni wa Mhe. Suleiman Makame Ali Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani ambao wageni wenyewe ni wanatoka katika Kikundi cha *Jufe Film Production* kutoka Wete Pemba ambao ni:

1. Ndg. Mohamed Kombo Hamad (Mwinyimpeku) huyu umaarufu wake anaitwa Mwinyipeku simama wakuone pamoja na

2. Ndg. Mohamed Yussuf Hemed na yeye huyu vile vile anatoka katika Kikundi cha *Jufe Film Production* karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema hayo sasa nimkaribishe Mwenyekiti kuja kuendelea na shughuli yetu. Mwenyekiti karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) Alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana.

Mhe. Mussa Foum Mussa (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, habari na Utalii): Mhe. Mwenyekiti, Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti naomba kutowa hotuba ya Maoni ya Kamati ya maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii

kuhusiana na Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye rehema kubwa kubwa na ndogo ndogo, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kushiriki kikamilifu katika Mkutano huu wa Bajeti.

Aidha nakushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa, na Michezo mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inaunga mkono mabadiliko yaliyofanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuunda Wizara hii mpya, tukiamini utendaji na ufanisi mkubwa zaidi kwa sekta zote zilizohamishiwa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, Sina budi pia kumshukuru Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa, na Michezo Mhe. Balozi Ali Karume, Naibu wake Mhe. Lulu Mshamu Abdullah pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii.

Lakini pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya. Kwa hakika wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	Mwenyekiti
2.	Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
4.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
5.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
6.	Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe
7.	Ndg. Himid Haji Choko	Katibu
8.	Ndg. Mussa Issa Mussa	Katibu
9.	Ndg. Amina Abeid Hemedi	Mkalimani

Mhe. Mwenyekiti,Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 7,411,600,000/= *(Bilioni saba, Milioni Mia Nne na Kumi na Moja na Laki Sita)* kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu Tatu (3) kama ifuatavyo:-

1. Programu ya Maendeleo ya Vijana
2. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni , Sanaa na Michezo na
3. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni , Sanaa na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inaipongeza Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa kuendesha mafunzo ya Stadi za maisha kwa vijana walioko nje ya skuli katika wilaya zote hapa nchini, tunaamini kwamba elimu hiyo itawasaidia katika kupambana na hali ngumu ya maisha na ukosefu wa ajira.

Aidha tunapongeza jinsi wanavyofuatilia maendeleo ya vijana hao na tunahimiza kupatiwa ufumbuzi wa haraka changamoto inayowakabili ambayo ni kukosekana kwa vyanzo vya kudumu vya maji na maeneo ya kudumu kwa shughuli zao za kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inapongeza juhudi zinazochukuliwa na Baraza la Vijana Zanzibar kwa kuyaunganisha na fursa mbali mbali za kiuchumi Mabaraza ya Vijana ya Wilaya. Kamati tunazidi kuishauri Idara kuongeza juhudi hizo, ili iweze kuyaunganisha zaidi mabaraza hayo ili Vijana wetu waweze kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Kamati kuridhika na juhudi zinazofanywa na Idara ya Vijana bado Kamati hairidhiki na kiwango cha fedha zinazotengwa kwa Idara hii, kulingana na Idadi ya Mabaraza ya Vijana yaliyopo hapa nchini kutokana na kuhamasika pamoja na uchakarikaji wa vijana hao.

Tunashauri Bajeti hii ikaongezwa kwa kiwango kikubwa zaidi katika miaka ya usoni ili Idara iweze kuendesha Mabaraza mengi zaidi pamoja na miradi ya maendeleo inayoanzishwa kupitia mabaraza hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inathamini juhudi zinazochukuliwa na Serikali pamoja na Jumuiya mbali mbali katika kuendesha matamasha mbali mbali yanayolenga kukuza shughuli za Utamaduni, Sanaa na Michezo yetu hapa nchini.

Kamati inasisitiza haja ya kuendelezwa kwa Matamasha hayo na kila inapowezekana Serikali haina budi kuyaunga mkono na kuingiza nguvu zake, kwani tunaamini kwamba matamasha hayo ni njia moja wapo ya kutangaza Utalii kitaifa na kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, inasikitishwa na tabia ya mwitikio mdogo wa ulipaji mirahaba na kuheshimu haki za matumizi ya haki miliki kibiashara kwa baadhi ya watumiaji hasa vituo vya utangazaji, pamoja na uharamia wa haki miliki. Tunachukua fursa hii kuiomba Wizara kulisimamia ipasavyo suala hili ili mirahaba hiyo iweze kupatikana na hatimae wasanii wetu waweze kufaidika na kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inapongeza juhudi zinazochukuliwa kutekeleza azma ya Serikali ya Kujenga Viwanja vya Michezo kila Wilaya. Tunahimizi juhudi hizo ziongezwe ili kuhakikisha azma hiyo inafikiwa ifikapo 2020. Aidha Kamati inapongeza sana hatua nzuri iliyofikiwa ya ujenzi wa viwanja wa Mao-Tse-Tung na tunahimiza kuongeza kasi ili ukamilike kwa muda uliopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu bado inasikitishwa tena na bajeti inayotengwa katika kuendeleza michezo hapa nchini. Tunazidi kuiomba serikali kuongeza bajeti ya Michezo, ili kuondokana na

tabia ya kuomba omba hasa pale timu zetu zinaposhiriki na kushindana mashindano ya Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti,Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii imehuzunishwa sana na taarifa za kuondolewa timu yetu ya Taifa ya Vijana ya Zanzibar chini ya Umri wa miaka 17 *(Karume Boys)*, katika mashindano ya *CECAFA* na hatimae kufungiwa na Kupingwa faini katika Mashindano hayo mwezi wa Aprili mwaka huu huko Rwanda, kutokana na tuhuma za kupeleka wachezaji waliozidi umri kinyume na utaratibu wa mashindano hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inahoji kwanini *ZFA* isizingatiae Kanuni za mashindano hayo, na kwanini ***ZFA*** itoe nafasi na ikaribishe viashiria vinavyoweza kurejesha nyuma timu zetu. Aidha Kamati inaendelea kuhoji kwanini *ZFA* isifuatilie kwa karibu Sheria, Kanuni na matakwa ya mashindano hayo hadi kufikia timu yetu ikaadhirishwa kwa tuhuma kama hizi?

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kwamba Masuala ya Michezo yanasimamiwa na Chama cha Soka Zanzibar yaani *ZFA*, ambayo haipaswi kuuingiliwa na serikali, lakini Ushiriki wa timu zetu kwa mashindano kama haya huwa zinabeba dhima ya ushiriki wa Taifa , hivyo Kamati inaomba Serikali kutoa taarifa ya kina kuhusiana na kadhiya hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Katika suala zima la kukuza na kuimarisha michezo hapa Zanzibar, Kamati yetu inaishauri Wizara, kukaa pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kuangalia namna bora ya kufufua Mashindano ya Tamasha la Michezo ya Elimu Bila ya Malipo pamoja na ile ya UMISETA kwani tunaamini kwamba, Matamasha hayo yalikua na mchango mkubwa wa kuibua vipaji vya wanamichezo na wasanii pamoja na kukuza Michezo na sanaa hapa nchini.

Aidha, Kamati inashauri kuwa, wakati umefika wa Kurejesha Mashindano ya Muungano, Kupunguza Idadi ya Timu zinazoshiriki Ligi kuu ya Zanzibar, pamoja na kupunguza Bei na Ushuru wa Vifaa vya Michezo na Sanaa, ikiwa ni njia moja wapo ya kuimarisha na kufufua michezo.

Mhe. Mwenyekiti,Kamati yetu pia inapongeza uamuzi wa Wizara wa kuwakumbuka Wasanii, wanariadha na wanamichezo wakongwe angalau kwa kuwatembelea na kurikodi taarifa za kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuona umuhimu wa suala hili la kuwajali hazina hii ya taifa, Kamati yetu pia iliwatembelea baadhi ya wanamichezo na wasanii wakongwe Unguja na Pemba na kusikitishwa na hali zao za maisha walizonazo hivi sasa kulingana na mchango wao mkubwa walioutoa kwa taifa letu enzi zao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inashauri kutizamwa kwa jicho la huruma zaidi wanamichezo, wasanii na wanariadha hawa, ili kuwapa moyo na wale waliopo hivi sasa na wanaokuja, kwamba taifa linathamini kazi muda wote

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaridhika na juhudi zinazochukuliwa za ukarabati wa Uwanja wa Gombani hasa katika eneo la *VIP* na kupaka rangi eneo lote la Uwanja nje na Ndani. Hata hivyo

Kamati inashauri Kiwanja hicho kiwekewe taa zenye mwangaza Mkubwa zaidi ili uweze kukidhi haja iliyokusudiwa pamoja na kufanyiwa matengenezo ubao wa kuoneshea matokeo ya mpira (*Score board*), ili kukipa hadhi zaidi kiwanja hicho na hatimae kiweze kuhudumia mashindano ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamalizia hotuba yangu napenda sasa kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa. Pia napenda kukushukuru wewe binafsi kwa mara nyengine tena kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na bajeti ya wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wajadili, wachangie na hatimae waunge mkono Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo waliyojipangia**.**

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mussa Foum Mussa, Mwakilishi wa Kiwani kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo, Wanawake, Habati na Utalii. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Simai Mohamed Said atafuatiwa na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Awali ya yote nianze kwa kutanguliza shukurani zangu kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwa kupitia wizara hii ambayo ni muhimu Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa maneno mazuri na hotuba yake alivyoisoma, tulikuwa tunamsikia kwa ukaribu kabisa na alikuwa anasoma kwa uzoefu. Vile vile nichukue nafasi kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ambaye hotuba yake imesomwa hapa leo na kamati yote kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kufanya masahihisho kidogo katika kitabu hiki kwenye ukurasa nambari 12 na 13, naomba nisome kwenye nambari 25. Mhe. Mwenyekiti, hapa inasema kwamba, "Baraza la Vijana la Zanzibar limefanikiwa kuunda sekretarieti ya Baraza la Vijana Zanzibar na kuajiri maafisa sita ambao watarahisisha kazi ya utendaji kazi wa shughuli za Baraza".

Aidha, wanasema kwamba, "Baraza la Vijana la Zanzibar limeweza kusimamia uendeshaji wa Mabunge ya Vijana wa nchi za Jumuiya za Madola (*Commonwealth Parliamentary Association)*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ndiye mwenyekiti wa *Commonwealth Parliamentary Association* na sifa hii ambayo imechukuliwa na Wizara husika inawezekana katika wakati wizara zinabadilishwa hasa limewekwa hili neno la 'kusimamia'. Kusimamia ilikuwa ni kazi ya Kamati

ya Baraza ambayo nimesimamia mimi kwa niaba ya Spika. Kwa hivyo hapa inatakiwa iwekwe kwamba Baraza la Vijana walishiriki kwa kupokea mwaliko wa Baraza la Wawakilishi wakaja hapa. Kwa sababu ukisema wamesimamia maana yake walilipia lakini gharama zote kwa kweli zilisimamiwa na Baraza la Wawakilishi chini ya kamati na chini ya mwenyewe Spika. Kwa hivyo mimi niseme tu baada ya masahihisho hayo ikiwa Waziri atayakubali ndio nitakuja kuunga mkono hoja, *otherwise* itabidi ametupokonya keki ambayo hii ilikuwa ni mafanikio ya Baraza la Wawakilishi na tuliwaalika hawa Baraza la Vijana kutokana na mahusiano yaliyokuwepo na Baraza.

Sasa baada ya hapo niende katika mchango wangu kwa vitu viwili. Kwanza nipongeze maendeleo mengi nimeona kwa sababu nina muda ni mchache, lakini nimeona vijana wetu katika vyama tofauti wameweza kufanya kazi nzuri. Kwa hivyo nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza sana katika vyama vyote vya mipira ya miguu nimeona, nimeona Zimamoto, nimeona walemavu, Chama cha Riadha, *Baseball*, vikapu, Pete, judo, kuogelea pamoja na mbio za baiskeli. Wote hao tunawapongeza sana.

Mhe Mwenyekiti, lakini moja nataka niseme ambapo kamati pia wameliona ni *issue* ya *Karume Boys*. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nawapongeza kazi nzuri wanayoifanya *ZFA* na kwa kweli uhuru ambao serikali imekuwa inawaachia waweze kufanya maamuzi yao. Lakini katika ile kadhia ya vijana wetu walipokwenda Rwanda mwezi wa Aprili na kuweza kuondolewa katika mashindano hasa kwa udanganyifu. Kwa kweli mimi binafsi ile aibu sikuipenda na imenitia huzuni sana. Kwa sababu kwanza ilienea katika mitandao kote, tumeandikwa sisi kwamba Zanzibar wadanganyifu. hata ndugu zetu wa Tanzania Bara walishindwa kutufahamu na unapoonekana mdanganyifu hasa katika michezo inatuondolea umakini wetu sisi wenyewe pamoja na serikali yetu. Kwa hivyo, mimi niombe sana udanganyifu huu na yale machafu ambayo yalitokea wayabebe wenyewe *ZFA*.

Mimi naipongeza wizara sana hasa nimpongeze Katibu Mkuu alipotoa Kauli ya Serikali kwa upande wao ili kuweza kufuata utaratibu kujua limeanzia wapi. Na ni kama vile kuweza kwenda kuwasaidia lakini kimsingi aibu ile ibakie nao wenyewe *ZFA* na serikali itoe *statement* ambayo inayostahiki. Kwa sababu kama unajua pahala unahitaji kutokana na umri wako unapeleka kijana unasema wewe, ukiona ile *e-mail* ambayo ilienea katika mitandao ya kijamii inasema kabisa kwamba mtu ambaye yuko chini ya umri wa miaka iliyotajwa. Sasa unapopeleka mtu ambaye ni baba anakuwa huyo tayari umri umeshazidi na katika mashindano ya vijana tafauti ya mwaka mmoja ni tofauti kubwa sana, tafauti ya miezi sita tayari utakuwa umeshakua kwa sababu bado unaendelea kukuani kijana. Kwa hivyo, mimi niombe wajitahidi sana katika hili

Pia nataka niwapongeze katika kitabu hiki. Mheshimiwa mimi pia ni mwenyekiti wa lile tamasha la Sauti za Busara na nitoe masikitiko yangu kwamba sijaona hata sehemu moja ambayo wamelizungumza, ambapo kwa kweli tumekuwa tuna mahusiano mazuri sana pamoja na wizara na wizara pia imekuwa wanatia mkono wao kwa niaba ya serikali kuwasaidia na pengine vizuri Baraza hili likajua kwamba, katika wale wasanii wa kimataifa wanapokuja kila mwaka wanatakiwa pale wanapopanda kwenye *stage* wawe wanalipa ada wanaita ni *business visa* ninafikiri zaidi ya dola 250. Sasa tayari serikali inakuwa inatoa unafuu kwa kutoa barua ya msamaha, wale wenyewe taasisi wasingeweza hata kulipa zile fedha, lakini serikali inatia mkono

wake na inakuwa ni sehemu ya wadhamini. Kwa hivyo, serikali isiache kwamba mafanikio yanayotokana na matamasha kama haya ambayo yanasimamiwa nje ni sehemu yao kwa sababu yanafanyika Zanzibar. Matamasha kama *ZIFF*, Sauti za Busara na mengine yote yameleta muamko mzuri. Tamasha la Sauti za Busara sasa limekuwa Tamasha la Saba Bora Afrika. Kwa hivyo, sifa hii inakwenda kwa Zanzibar. Sasa serikali nao waitambue na wao wachukue huo ujiko ambao Zanzibar inaupata. Sasa nataka nizungumze kuhusu masuala ya *studio* pamoja na masuala ya fedha mimi nitashughlika wa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tumetengeneza *studio* lakini vijana wetu bado uwezo wao ni mdogo wa kifedha. Sasa lazima tuzingatie haya, kama tunataka hii tasnia ya filamu ikue lazima tuangalie ada tunazoziweka. Sasa mimi nashauri katika hii *studio* vijana wetu katika kuwashajihisha kwa ujumla tuangalie kwa ukubwa na tuwe tunawasikiliza wao wenyewe. Kwa sababu tasnia ya muziki, filamu, sanaa ni ubunifu, anayejua ni yule mwenyewe ambaye anabuni lile jambo. Sasa kama unataka umratibu na umsimamie umsikilize uwezo wake, kwa sababu ufahamu wote mwisho wa siku upo kwao wao wenyewe. Kwa hivyo, mimi niombe tu kwamba leo tunajua hapa tunae msanii wetu mmoja yupo juu ndugu yetu Issa Mussa maarufu ni *cloud*, ni *actor* maafuru kutoka *Bongo Flavor* yupo kaja kuunga mkono na tuwapongeze sana ni mgeni wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf amekuwa anakuja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu, watu kama hawa ambao wanajitolea tuwasikilize na tuzidi kuwafahamu hasa kile wanachokitaka wao. Naamini anapokuja Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma atayakazia haya ninayozungumza kwa sababu yeye ni Mwakilishi wa vijana.

Jengine pia nataka nizungumze suala la ajira katika masuala mazima haya ya vijana. Mheshimiwa mwaka juzi nilipokuwa nachangia bajeti nilishauri utaratibu gani unatumika kuwatambua vijana wenye uwezo na sifa ambazo wanaweza kufanya kazi. Sasa mimi nashauri tena kwa kupitia Wizara inayohusu masuala ya Utumishi pamoja na Wizara hii yetu ya Vijana, waweke *database* ya vijana kwa kupitia Halmashauri zetu pamoja na *CV* wale vijana wote ambao tayari wameshamaliza kusoma tayari wameshajijengea *experience*, ina maana kama mtu ana uwezo wa *mechanical engineer* tayari kama kuna hoteli au sehemu kuna ajira katika mikoa yetu unakuwa tayari unamsaidia. Lakini na hizi ajira zinapotoka fursa zake katika mikoa na wilaya ziangaliwe sio zinaishia pahala pamoja. *(Makofi)*

Sasa hivi pia utaona kuna muamko mzuri sana wa kuhakikisha kwamba ajira zinakwenda maeneo tofauti. Mimi kwa mfano natoka Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kati hizi ajira mimi kila nikiomba tangu siku hizo hakuna hata moja niliyoipata. Sasa naomba hawa vijana wetu waliokuwepo wenyewe wasaidiwe lakini wawajue pia. Zinapkuja ajira zile mimi niseme za serikalini lakini tuwaangalie katika kuwasaidia kuweka kumbukumbu zao katika sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunatumia serikali zetu za mkoa kwa sababu sasa hivi tumeamua au tumeazimia kwamba tunapeleka madaraka mikoani kwa njia ya ugatuzi ambayo ni *devolution of power*. Sasa lazima taarifa zao tuwaangalie, kama unaangalia Mkoa wa Kusini mimi Wilaya ya Kati jimboni kwangu sina hoteli hata moja, lakini ukiangalia jimbo la Mhe. Jaku Hashim Ayoub jimbo la Paje, ana hoteli kutoka Paje, Michamvi mpaka Makunduchi wana hoteli nyingi. Sasa zile ajira zote zinapotokezea nafasi Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini zile Halmashauri

zisimamie kuwajua vijana wao ili waweze kuwasukuma katika nafasi ambazo tayari wana uwezo nazo na hili halihitaji ubunifu mkubwa, ni Mkuu wa Mkoa tu kujenga mahusiano mazuri pamoja na watu husika. Mimi naamini hili likifanyika tutaweza kuwakomboa vijana wetu wengi sana. Kwa sababu hao watu waliokuwepo katika mahoteli wanatafuta vijana ambao wanaishi katika maeneo husika wanashindwa kuwafikia kwa sababu hakuna mahusiano ya karibu, kutenga utaratibu mzuri baina ya Serikali Kuu pamoja na Serikali zetu za Wilaya na Mkoa ili kuweza kuwasaidia vijana wetu. Sio vibaya katika fani zetu ambazo tunajua tuna uwezo nazo tuweze kuwasaidia, mimi nitafurahi sana ikiwa tutaweza kuwasaidia. Pia natala nizungumze jambo ambalo limezungumzwa kwenye suala la filamu. Mheshimiwa katika kila wizara ukiangalia wanahitajika waweke vipaumbele kwenye sekta ya utalii. Ukisoma kwenye bajeti wakiulizwa kila wizara wanaema kwamba utalii. Sasa mimi naona katika suala hili wizara hii kuna sehemu moja ambayo tunaisahau ni suala la *film industry*.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka juzi nilizungumza hapa naendelea kurudia tena, pale Kenya kuna *move* inaitwa *Auto of Africa* imefanywa mwaka 1984, ilipeleka umaarufu sana kwa Kenya kila mmoja ukienda Ulaya ukimwambia Kenya anakwamba *Auto of Africa,* tutengeneze filamu. Sisi kwa mfano tuna *venue* nzuri zenye mvuto, tuna bahari, tuna fukwe, tuna mashamba, tumejaaliwa na kila kitu lakini hakuna hata sinema moja ya kimataifa inafanyiwa Zanzibar. Sinema moja ikija Zanzibar kutoka *Hollywood* itatupa jina kubwa sana na kuweza ku-*promote* nchi yetu lakini pia italeta fedha kubwa sana.

Kwa mfano, Mji Mkongwe ukiugeuza kuwa ni sehemu ya *venue* ya *film industry,* tufanye filamu moja tu ya James Bond i-*act* kwa dakika tatu tu pale, mimi nakwambia watu wote Mji Mkongwe watavaa suti, wote watakuwa mwaka mzima wanakula raha kwa sababu pesa itakayoingia na kulipa wanakuja watu 400 na 500 kwa filamu ya dakika tatu, lakini *promotion* yake itajulikana duniani kote. Kwa hivyo, tuangalie sana *opportunity* zilizokuwepo kwenye *film industry* na kuifanya Zanzibar katika juhudi na kuiunganisha katika utalii, sio tunaimba utalii lakini wana wajibu wa kila wizara kuwaangalia wao wanaweza ku-*take opportunity* katika sehemu fulani.

Pia niwaombe watu katika wizara husika washiriki katika matamasha ya kimataifa ambayo yanahusiana na *films,* waende na Mhe. Waziri ikiwezekana kwa sababu yeye ni muelewa na yeye mwenyewe afuatane nao azunguke nao duniani huko, tukuone usiwe unabakia hapa Zanzibar Mji Mkongwe na hapa mjini unasema kwamba unalinda utamaduni. Utamaduni pia lazima tujifunze kwa kuangalia huo utamaduni wenyewe kuugeuza kuwa ni sehemu ya uchumi wetu, ikiwa utamaduni wako hawakuletei fedha basi itakuwa kuna sehemu moja umekosea, tutumie utamaduni wetu kama wenzetu wanavyofanya tuangalie Wagiriki, Waingereza. Juzi tumeangalia ndoa ya mtoto wa Malkia basi duniani kote imegeuzwa kuwa kama sasa kila mmoja asimamieshe kazi zake, aangalie televisheni afuatilie matangazo. Kwa hivyo, lazima na sisi tutumie utamaduni wetu ambao tunao ni urithi mkubwa kufanya ni sehemu ya uchumi na itatusaidia sana na tuna nafasi sisi pia kuwasaidia ndugu zetu Tanzania Bara na wao pia wakajifunza kwetu sisi. Kwa hivyo, mimi naomba suala hili tulikalie sana kwa nguvu zote.

Chengine kuhusu Uwanja wa *Mao-tse-Tung.* Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nijue Uwanja wa *Mao-tse-Tung* kiingilio kitakuwa bure. Mbona ukuta ni mfupi sana na ndugu zetu tunawajua sisi Wazanzibari kwa tabia tuliyonayo ya kuruka ukuta. Kwa hivyo, Mhe. Waziri

atakapokuja atueleze kwamba kiingilio kitakuwa bure au kutakuwa kunalipiwa. Lakini pia hapana *parking* pale *Mao-tse-Tung* na uwanja ni mzuri na nimpongeze sana Mhe. Waziri. Sasa zile *parking* za magari amejipangia utaratibu gani.

Vile vile katika uwanja kutakuwa kuna *cafeteria* au mkahawa pamoja na vyoo, ili kuhakikisha vile vyoo vinakuwa endelevu haviharibiwi pamoja na mikahawa. Je, amepanga kuikodisha ili ile fedha iingie wizarani, ulinzi wake na usalama utakuwaje. Mimi nashauri ukodishe mpaka vyoo iwe ni shilingi 500 au 200 mtu kuingia kujisaidia lakini ziwe zile fedha zinaingia katika kuweka hali ya usafi na usalama.

Kuhusu kikundi chetu cha Taarab cha Mataifa. Mheshimiwa mimi napongeza kwamba kikundi cha taarabu kimekuwa kinashiriki katika matamasha ya kimataifa. Lakini naomba kikundi cha taarabu wafunguliwe *website* yao wenyewe wawe na mtandao wao wenyewe, wawe wanajulikana duniani kote na wawe na sehemu tatu. Kwa sababu kama unataka kuwaalika kushiriki katika matamasha ya kimataifa kuwalipia tiketi wanakuwa wako wengi 30 pamoja na meneja na watu wa serikali wakifuatana. Wapungue wawe wana vikundi wachache wawe wanaweza kufanya kama vile '*bashrafu'* kumi, lakini pia iwe watu wanafahamu. Kama unaweza kwenda ku-*perform* kwa watu kumi hata Dar es Salaam nchi zetu za jirani wawe pia wana uwezo wa ku-*promote,* hata hao nchi zetu za jirani wawatambue kwamba wao hata kumi wanaweza kufanya *performance* nzuri na wakatoa burudani ambayo itaendana na taarabu.

Nina dakika ngapi Mhe. Mwenyekiti naona unaangalia.

Mhe. Mwenyekiti: Dakika mbili.

Mhe. Simai Mohamed Said: Dakika mbili, haya ahsante. Sasa mimi naomba katika kikundi cha taarabu kama wako 30 wa *breakdown* watu 15 mpaka kumi na walitumie lile *Ganun* pamoja na zile *instruments* zao zote za kizamani na za kisasa ambazo wanazo ili unapotoka ule mziki uwe ni mzuri kabisa na waweze ku-*perform* ndani ya Bara la Afrika, wawe wanapata fedha nzuri na serikali iwe nyuma yao pia katika kuwanyanyua katika mazingira yao.

Jengine nataka nizungumze suala la wasanii wetu. Kwanza nataka niipongeze kamati kwa kuwatembelea wazee na kuweza kuwatambua. Pia nataka nizungumze lakini kwanza nimpongeze Mhe. Rais kuwa ule Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi sasa umepatiwa jina rasmi la Rais wetu Mstaafu mpenzi wetu, Dkt. Idrissa Abdul-Wakil. Lakini mimi nataka nizungumzie juu ya wasanii wetu wengi tuliokuwanao ambao ni maarufu. Kwa mfano Mhe. Bakari Abeid, Bi. Kidude. Mwapombe Hiari, hao wote wamefanya kazi nzuri. Sasa hakuna maeneo pia tukaweza kuwatambua, kuna barabara zetu za ndani, tuna maeneo huko mitaani pia, kuna majengo ya kihistoria basi na wao kumbukumbu zao waweze kutambulika.

Kwa mfano, Bi. Kidude amechangia sana katika sanaa Zanzibar hasa kunyanyua wasanii wetu. Kwa hivyo, tusisubiri mpaka wanapoondoka duniani tuwathamini pia wakati kwenye uhai wao ili maisha yao na mchango wao kwenye familia zao wawe wanaweza kuutambua. Sisemi kwamba ni kosa kuweza kutambua au sio jambo jema wakati tayari wao wameshatangulia mbele ya haki, lakini ni vizuri pia kuwathamini watu mchango wao wakati wako hai. Mimi niipongeze

sana serikali hasa Ofisi ya Makamu wa Pili kwa kuuita ule ukumbi uliokuwepo katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwamba ni Dkt. Ali Mohamed Shein, kuwa mwenyewe yupo ni Rais na kaujenga yeye. Kwa hivyo, inakuwa ni jambo zuri sana kuweza kulifanya.(*Makofi*)

Baada ya hapo nilikuwa naangalia bajeti, ukiangalia mwaka 2017/2018 ilikuwa shilingi 1.5 bilioni ambapo ilikuwa karibu na shilingi 1.2 na ushei. Sasa mimi niombe ikiwa tunataka kuendeleza suala zima la masuala ya sanaa na filamu. Sina uhakika nadhani niwe mkweli ni njia gani kwamba tubakie kwenye mfumo wa Baraza au tugeuze idara. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja atatueleza sisi wapi tunaweza kupata bajeti kubwa tukaongeza bajeti na tukapata usimamizi mzuri ili katika kuendeleza masuala mazima ya filamu na sanaa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tu nimeona vitu vizuri ambavyo masomo madarasa wamepatiwa kwenye masuala ya *script,* wamefundishwa vijana mengi ambayo masuala ya masomo ambayo wameshiriki. Lakini pia katika maeneo ambayo wameshiriki katika makongomano ya kimataifa ya masuala ya lugha yetu ya kiswahili. Kwa hivyo, ni jambo zuri ziendelezwe pia kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu katika wizara zote husika tumeoma karibuni pia Wizara ya Elimu imeandaa pia suala la Insha. Kwa hivyo, si vibaya pia BAKIZA wakashirikiana pia na Wizara ya Elimu katika kufanya makongamano pia ya kutunga lugha ya kiswahili hasa katika kuibua vipaji vya ngonjera, mashairi na maeneo tofauti ambayo haya maanini anapokuja Mhe. Rashid Makame Shamsi ambaye ni Mwakilishi makini ataweza kutusaiadia sisi katika masuala haya.

Sasa baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa muda na nijipongeze mwenyewe kwa kutumia muda wangu vizuri naamini michango yangu ilikuwa mizuri na nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Mimi niseme tu naunga mkono hoja kwa kuzingatia kwamba nikiamini kwamba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho ataweza kufanya *summary* nzuri na yale yote ambayo nimeyagusa ataweza kuyataja.

Nakushukuru sana na nawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi kwa kunisikiliza na niwapongeze kamati. Naunga mkono hoja na kama nilivyosema mapema kwamba Waziri atakujua kufanya majumuisho ipasavyo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Simai Mohammed Said Mwakilishi wa Tunguu kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Nassor Salim Jazira ajiandae.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji ya Bajeti ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutanguliza shukurani zetu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Shukurani hizi zinaambatana kwa kutuletea na kutuwekea Wizara maalum inayohusiana na Vijana moja kwa moja na sio mambo mengine.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye wizara, niishukuru wizara yote na watendaji wake wote akiwemo Katibu Mkuu kwa kuweza kushauriana, kupeana maamuzi mazuri na kuweza kushirikiana na sisi katika kuiandaa ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kuipongeza sana kabla ya kuendelea kwenye michango yangu, nianze kwa kuipongeza sana timu ya Taifa ya Zanzibar, (*Zanzibar Heroes)* kwa ushindi na sifa nzuri waliotuletea nchi yetu na kutuvisha taji la michezo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi naomba nianze katika ukurasa namba 40 kwenye Maendeleo ya Vijana kwenye Programu ndogo ya tatu.

Kwanza niishukuru serikali na wizara yao hii kwa kuona kwamba vijana wanawajali na kuwathamini, lakini vile vile kuwaweka katika vipaumbele vyao walivyoweka wizara. Niende kwenye Programu ya tatu inayosema kuyawezesha Mabaraza ya Vijana kuwa na afisi wafanyakazi na vifaa. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba niipongeze sana serikali kwa kuliona hili, lakini niipongeze wizara ambayo iliyotangulia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wanawake, Vijana iliyokuwa mwanzoni na watoto kwa kuweza kutufanikisha robo ya majukumu yetu na malengo yetu ambayo tulijiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye bajeti iliyopita tulitengewa shilingi milioni mia moja. Bajeti ambayo haijaweza hata kutusaidia kuweza kununua kifaa ambacho kitaonekana na kutusaidia katika afisi zetu. Lakini katika utekelezaji halisi tulikuwa tunaona kwamba kulikuwa kuna makosa na baadhi ya udanyanyifu kutoka wizara ile kwa kutwambia wametununulia vifaa vya kuweza kutusambazia katika maeneo yetu. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo lilikuwepo lakini kwa baadhi ya wilaya na wilaya hizo ni chache kutokana na wingi wa mabaraza haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo niiombe wizara hii mpya na niishauri sana kwenye haya malengo ambayo wamejiwekea kwa Baraza la Vijana ya kuwapatia afisi na ukiangalia Mabaraza ya Vijana yapo mengi, kuanzia Taifa mpaka kwenye Mashehia. Lakini kizuri zaidi au kibaya zaidi hata hilo Baraza lenyewe la Vijana Taifa afisi hawana. Kwa hiyo, tungeanza na kuwaona vijana wetu hawa tuwatafutie majengo yaliyokuwa mazuri na tukiamini kwamba majengo bado yapo serikalini ili na wao waweze kujihifadhi na kuweza kupata sehemu ya kufanya vikao vyao na kutoa maamuzi.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niende kwenye Serikali zetu za Mitaa lakini na Manispaa zetu ambazo zipo hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba niwaombe sana Serikali zetu za Mitaa, Halmashauri zetu, lakini na Manispaa zetu zote ambazo tunashirikiana nazo kwa namna mmoja au nyengine. Niwashauri kwanza wakae na vijana hasa hawa Mabaraza ya Vijana, lakini pia kwenye sheria zao ambazo wanatunga *atleat* basi na wao waweze kutugaia angalau asilimia chache ya kuweza kujiendesha sisi wenyewe, asilimia hizo naamini kwamba tukipata asilimia kidogo na serikali tukipata kidogo nahisi vijana tutafikia mbali na kuweza kwenda katika programu zetu ambazo tumejipangia.

Lakini sio asilimia tu Mhe. Mwenyekiti, na miradi midogo midogo ambayo inaingia kwenye Halmashuari zetu ikiwemo makampuni mbali mbali yalitoka kuendelezwa basi miradi hiyo vijana wanaiweza na tuziombe Halmashauri zetu watupe sisi vijana kwa kuweza kuifanyia kazi.
Mhe. Mwenyekiti, natambua bajeti ya safari hii imeongezwa kwa kesi za vijana. Lakini kuongezwa kwake sitegemei kama itatosha kwa masuala yote ya vijana. Kwa hivyo, niiombe serikali kwenye bajeti inayofuata ituongezee bajeti ili vijana sisi ambao ni wengi kutokana na tathmini ambayo inafanywa asilimia kubwa ya wakaazi na wananchi wa Zanzibar ni vijana basi tuombe sisi vijana ambayo tumejitoa na pale tunapothubutu basi tupewe nyenzo muhimu na za wakati ili tufikie malengo yetu.

Niipongeze serikali kwa dhati kabisa, lakini kwenye bajeti hii ambayo tumewekewa Mhe. Waziri hapa amesoma ripoti ametueleweshа tuna bajeti ya shilingi bilioni tatu kwa mwaka huu wa fedha 2018-19 kwa ajili ya vijana pekee. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hii ni kamati yangu na wizara yangu niendelee kuishauri wizara hii sikivu ya kwamba fedha hizi ambazo zimetengwa kwa ajili ya vijana tujaribu kutafuta namna ya kuweza kuzitumia vizuri, lakini sio vizuri kwa kuwagaiya tu vijana watafute namna ya kuweza kuwashauri wao wenyewe na kuweza kukaa nao kitako ili tuone vijana wanataka nini na ili tuone malengo yao ambayo wamejiekea. Kwa hivyo niwaombe ili tuende sambamba na Sera ya Tanzania ya Viwanda basi waanzishe viwanda vidogo vidogo ambavyo vitakavyowasaidia vijana hasa wa Zanzibar katika tatizo la uhaba wa ajira.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hilo kwenye maendeleo ya vijana naomba nirudi kwenye ukurasa wa 38 inayohusu vipaumbele vya wizara. Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu namba 4 wanatwambia kuibua na kuendeleza kusimamia, sanaa, wasanii na ubunifu. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana serikali kwa kuona kwamba kuna haja sasa ya kusimamia na kuibua sanaa zetu hapa Zanzibar. Kwani tukiangalia sanaa hizi zilikuwa bado ziko nyuma lakini na wasanii wetu hali zao sio nzuri sana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kupitia hili nimepata faraja kwa kuona wasanii wetu hasa hawa ambao wanachipukia na hata wale wakongwe watapata kujaaliwa na kuona wanafikia malengo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi niiombe wizara sana isichoke kuwaunga mkono lakini sio kuwaunga mkono tu na kuwashika mkono ili kuweza kufikia malengo yao waliojiwekea. Mhe. Mwenyekiti, kwa namna nyengine ya pekee niseme kwamba serikali kupitia wizara hii tujaribu kushirikiana na wasanii wetu hawa, ili na wao wanyanyuliwe soko lao la kazi zao kuona kwamba soko hili linakwenda na wakati lakini sio wakati tu kulingana na mazingira ambayo yanatukabili nchi yetu. Mfano mdogo soko la sanaa kule Tanzania Bara.

Tanzania Bara wenzetu wana soko zuri lakini kuna vipaji ambavyo vinaibuliwa kutoka Zanzibar vinakwenda kutumika Tanzania Bara. Kwa hiyo, kama wizara ichukuwe jitihada ya hali ya juu ili kuona vipaji vyetu ambavyo vipo hapa Zanzibar vitumike hapa hapa, lakini na vijana wenzetu nao wafaidike kutokana na kazi ile ambayo waliojiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwenye hao wasanii wana changamoto nyingi sana. Lakini changamoto hizo hasa ukiangalia katika kizazi kipya changamoto kubwa ambazo walizokuwa nazo kwanza kutopewa vipaumbele kwa kazi zao ambazo wanazifanya. Mhe. Mwenyekiti, hili niliseme kwamba tumekuwa mashahidi hata katika sherehe zetu za kitaifa wasanii wetu ambao

tunawachukua hapa Wazanzibari tunawapa kipao cha nyuma sio kipaumbele kama tunavyowachukua wenzetu kutoka Bara.

Vikundi vya sanaa vipi vingi lakini kuna wasanii wengi ndani ya nchi yetu lakini kuna vijana ambao wanajitolea kwa taifa lao wanachukuliwa wanakwenda kwenye sherehe za kitaifa na baada yake wanapewa ahsante na sio ahsante sana kama ilivyo kwa wenzetu. Kwa hivyo, niiombe sana serikali iwaangalie kwa jicho la tatu hawa wasanii wetu ili na wao kuwaibuwa na kuweza kupiga hatua zile ambazo tunazihitaji. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninachoamini mimi kwamba tukiwapa vipaumbele na wao watakuwa na hamu watakuwa na busara, watakuwa na huruma ya nchi yao na kafanyakazi kwa maslahi ya taifa letu. Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto nyengine ya kutopewa ruzuku kwa baadhi ya Vyama vya Sanaa. Mhe. Mwenyekiti, hili niliombe sana Mhe. Waziri anatambua na Mhe. Naibu Waziri kwa bahati nzuri anatokea miongoni mwa vijana tujaribu kuwaona vijana wenzetu, tujaribu kuwaona wasanii wenzetu hasa vijana tuwapatie alau ruzuku na wao kwenye vyama vya *atleast* waweze kukopesheka katika Taasisi za Kifedha, kwa sababu wasipokuwa na fedha wao wenyewe, wasipokuwa na chanzo chao wenyewe cha kutoa fedha hawatapata fursa alau ya kupata mkopo wakaaminika katika nchi yao. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, waandae programu, waandae utaratibu mzuri ili tuone na wao wanatapata ruzuku kama vilivyo vyama vyengine vya Mpira wa Miguu na vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye wasanii wakongwe. Niendee kuwamwagia sifa za dhati kabisa wizara ikisimamiwa na Katibu Mkuu kaka yangu, mwenzetu Omar King kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Lakini na jitihada zake zote ambazo anashirikiana na wizara ili kuona mambo yakwenda vizuri. Mhe. Mwenyekiti, wasanii hawa nitangulie kusema kwamba wameifanyia kazi sana nchi yetu, wameshamwaga jasho jingi na wanajitolea kwa kuweza kutusaidia na kutupelekea *message* kwa jamii yetu.

Kwa hiyo, mie niombe kama tunavyoweza kuwathamini na kuwajali baadhi ya wanasiasa wakongwe basi niombe na hawa wasanii wakongwe nao tuwajali, tuwathamini na tuwape vipaumbele kwa kuona kwamba kazi walioifanya ni kubwa, lakini bado tunahitaji vitu vizuri kutoka kwao na vitu vizuri hivyo hatutovipa kama tukiwa nao mbali. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, niseme sana kwamba hawa wazee wetu hawa akina Profesa Moh'd Elias na wengine basi tuwaone nao ili tuone tunafanyaje katika kukuza na kuhifadhi sanaa yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niwazungumzie hawa hawa wasanii wakongwe kwa bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa kamati. Mhe. Mwenyekiti, kwenye ziara zetu ambazo tumekwenda kwa bahati mbaya sana tuliwakuta baadhi ya wasanii hawa hususan wanamuziki na michezo ya mpra wa miguu, wenzetu au wazee wetu wako vibaya sana na wapo vibaya mpaka inafika wakati wanakataka tama kwa sababu walishapoteza nguvu zao sana kwa kulitumikia taifa letu, lakini wameshatumia ujuzi wao mkubwa sana kwenye kuijenga nchi yetu. Lakini kwa masikitiko inafika wakati wana vikundi vyao ambavyo wanavianzisha ili kuweza kuwazaa hawa akina Mohd Elias baadae lakini kuna na kuwazaa kina Profesa Gogo wa baadae hawana *support* kupitia kwenye serikali. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tukae nao vizuri tujaribu kushauriana nao tuwape ushirikiano kama serikali tuwa-*support* ili na wao waone wanafaidika katika kulimwaga jasho lao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii sina nia ya kuzuiana kifungu, mambo mema na mazuri tumeshaishauri kamati kupitia vijana wenzangu Wazanzibar hasa wa Mkoa wa Kusini Unguja niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Mwakilishi wa Vijana kutoka Kusini Unguja kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi atafuatiwa na Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza alau na mimi kuichangia hotuba hii ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kuipongeza wizara na hususan waziri makini Mhe. Ali Karume na Naibu wake na watendaji wote wa taasisi za wizara hii.

Nichukuwe fursa hii vile vile kuwapongeza vijana wote wa Zanzibar niwapongeze wana michezo wote wa Zanzibar na wasanii ambao wengine katika ukumbi huu sehemu ya juu kwa kazi zao nzuri ambazo wanalinyanyua taifa hili katika medani mbali mbali. Lakini niipongeze kamati husika ambayo imewasilisha ripoti yake katika ku-*support* hotuba hii na nimpongeze sana Mhe. Mussa Foum Mussa Mwakilishi makini kwa uwasilishaji wake. Lakini niwapongeze pia Wajumbe wenzangu walionitangulia kwa michango yao fasaha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana kwa upekee kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuwajali vijana, lakini vile vile kujali sekta za sanaa na michezo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika michango yangu sasa. Nije katika mafungu pamoja na ruzuku. Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia kitabu hichi katika mafungu ya baadhi ya taasisi au ruzuku kwa kweli hatukuwatendea haki. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Sanaa, Sensa, Filamu na Utamaduni. Mwaka jana wenzetu hawa ambao ndio tunawaamini katika kukuza sanaa, sensa za filamu pamoja na utamaduni tuliwapangia na kuwapitishia shilingi milioni thamanini na nne. Lakini la kusikitisha sana mwaka huu bajeti yao ruzuku ni shilingi sabini na nane nukta nne milioni.

Sasa tujiulize lakini na Baraza la Michezo vile vile pamoja na kila mwaka kuweza kuliombea kwamba ruzuku yake hii ni ndogo sana. Mwaka jana nao walipangiwa shilingi milioni thamanini na nne. Lakini la kusikitisha sana mwaka huu wamepangiwa shilingi sabini na nane milioni nukta nne. Sasa ukitizama watu wetu wa sanaa na watu wa michezo vifungu vyao vinalingana lakini majukumu yao nina hakika yana tofautiana. Inaonekana kama *copy and paste*, hawa tuwape tuliwatoa thamanini na nne basi wote tuwape sabini na nane, kwa kweli sio haki. Hizi taasisi bila kuweza kuziendeleza kibajeti kwa kweli suala zima la maendeleo katika sanaa na michezo haliwezi kupiga hatua.

Baraza la Michezo lina vyama visivyopungua thalathini vyote vinataka kuendelezwa kukuzwa. Kwa kweli kila mwaka tukiendelea kuwapunguzia bajeti sidhani kama tutagipa hatua katika hizi nyanja itakuwa tunawalaumu wenzetu lakini kama hatujawaingizia fedha za kutosha kwa kweli hatuwezi kupiga hatua.

Lakini nende katika wenzetu hawa wa Utawala na Uendeshaji Pemba wamepangiwa shughuli karibu ya sita na hii ndio taasisi ambayo inaendesha shughuli zote kule Pemba. Kwa kweli kwa shilingi milioni mia moja na kumi, kwa kweli wenzetu hawa Pemba hawawezi kumudu kutekeleza majukumu yote kwa sababu kule inakuwa kama wizara, taasisi zote hizi maan yake kule wao ndio wasimamizi.

Mhe. Mwenyekiti, hatuja watendea haki hawa watu tutakuja walaumu baadae hawa kwamba hawakufikia yale malengo na shughuli ambazo wamejipangia. Lakini nije katika maendeleo ya vijana ambayo Mhe. Salha ameeleza kwa ufasaha sana, maendeleo ya vijana wamepangiwa shilingi milioni 457 katika shughuli sita ambazo zimepangwa, lakini kwa shughuli zile ambazo zimepangwa zikiwepo za kuwawezesha kiuchumi hizi pesa ni kidogo sana.

Lakini Mhe. Waziri atakapokuja nataka ufafanuzi na kama haujaridhisha basi natishia katika hili. Kuna bilioni 3 zimewekwa lakini hazikuwekwa hapa zimewekwa mwisho zimeombewa kwa ajili ya ajira kwa vijana kwa nini zisiweke katika programu ya vijana, kwa nini ziwekwe mwisho ziombewe kule, kuna siri gani za kuwekwa kule, zisiwekwe hapa zingechanganywa hapa zikawa shs.3,457,000 tukasema na ile ajira ya vijana iko hapa tungeweza kujiridhisha. Haya mambo ya kutenga fungu mbali halafu mwisho wa siku tunakuja kushindwa kupima utekelezaji wake. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja tunaomba ufafanuzi kwa nini zile Bilioni 3 za ajira ka vijana zikawekwa pembeni kule.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika maendeleo ya michezo. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze kwa juhudi za serikali zinazochukuliwa katika kuendeleza michezo na hususan Mhe. Rais, lakini bado juhudi za kuendeleleza michezo hazijatosha bado, tunapaswa kuwa juhudi za kuwa juhudi za kipao mbele kabisa katika michezo. Na hii yote inakuja kutokana na bajeti kama nilivyotangulia kusema, hapa imezungumziwa michezo kwa mfano *baseball* lakini imezunguziwa Mwanakwerekwe tu, *baseball* iko Mwanakwerekwe tu. Maan yake bado hatujapiga hatua. Hii ni picha kwamba baadhi ya vyama vya michezo havijapewa kipaumbele katika kuendeleza michezo na ni vingi sana. Kwa hivyo tuangalie tusiangalie *footbal*l tu tuna vyama vingi ambavyo vilikuwa vinailetea sifa Zanzibar katika michezo ya kimataifa.

Kwa hivyo ni wakati sasa umefika wa kuweza kuvitazama vyama mbali mbali na sio kukazia zaidi katika *footbal*l, tuna vyama vilikuwa vinafanya vizuri kwa mfano katika *badminton* katika *table tennis*, vilikuwa vinafanya vizuri lakini hivi sasa utakuta vimelala na hii yote ni kutokana na kwamba hakuna msukumo, hakuna miundo mbinu mizuri katika hivi vyama. Hivyo hili nalo nilisisitize sana wizara ilichukue ili kuongeza juhudi zaidi katika masuala haya ya michezo.

Lakini nije katika michezo ya kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, tumeona hapa kuna vyama hususan *footbal*l na vyengine vimeweza kushiriki katika michezo ya kimataifa. Kwa mfano kwenye *footbal*l vilabu kama JKU, Zimamoto vilishiriki katika klabu bingwa ya Afrika na ile ya

Shirikisho, lakini vimefanya nini nafkiri tukae tuweze kujiuliza. Ukweli Mhe. Mwenyekiti, maandalizi ya michezo kimataifa bado, ule ushindi wa *heroes* unakuja kwa bahati mbaya kwa maana nyengine. Wenzetu wale walikuwa na juhudi, walikuwa na uzalendo ndio maana walikuja na ushindi wa pili. Lakini ukitaza uhalisia wa programu za maandalizi kimataifa bado Zanzibar tunahitaji kuweza kujipanga.

Timu hizi kwa mfano ya JKU na Zimamoto hakuna timu hata moja iliyocheza mchezo wa kimataifa kwa kujiandaa kwenda katika mashindano unatarajia nini, utacheza na KMKM utacheza na Pemba sijui Jamhuri, huwezu kujipima nguvu katika michezo ya kimataifa na wala hatuwezi kushinda kirahisi katika michezo ya kimataifa kama hatuna program maalum ya kuweza kuziandaa timu zetu kimaataifa. Mhe. Mwenyekiti, vile vile huduma ni duni sana kwa hivi vilabu wakati wa kujiandaa, vifaa wakati mwengine tunatoa misaada lakini hiyo misaada tunayotoa vile viatu vikipindwa vinakatika sasa umewasaidia vipi, ushahifadhi vifaa *store* miaka 10 huko vishakuchachia ndio unakwenda kuwasaidia wana michezo. Kwa hivyo sote tuna wajibu wa kuvisadia hivi vilabu katika maandalizi ya kimataifa ili Zanzibar iendelee kupata ushindi katika madali mbali mbali za michezo hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika sasa suala zima la motisha kwa wana michezo. Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuwa mstari wa mbele katika kutoa motisha kwa vilabu au kwa wanamichezo ambao wanafanya vizuri. Lakini nina masikitiko sana Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hichi kuna baadhi ya vilabu au baadhi ya vyama vimefanya vizuri, lakini mimi sijasika kupongezwa. Wenzetu wa Judo mimi sijawasikia kupongewa na humu wenzetu wa judo walipata medali nyingi vile vile katika kipindi hichi. Kuna medali tatu za dhahabu, medali tatu za fedha, medali sita za shaba lakini sijaskia kupongezwa kama wengine.(*Makofi*)

Lakustusha zaidi linauloudhi zaidi wenzetu wa chama cha michezo ya watu wenye ulemavu wa akili yalifanyika mashindano hapa Mhe. Mwenyekiti, mwezi Disemba 2017, wenzetu hawa walipata medali 38, walemavu wa akili, walipata medali 19 za dhahabu, medali 9 fedha na medali 10 za shaba. Mhe. Mwenyekiti, niambie wamepongozwa lini na taifa hili. Hawa ni walemavu wa akili kwa nini tusiwape moyo, wenzetu wametetea kila pahala hawajapongezwa tena yalikuwa ni mashindano ya kitaifa timu mbali mbali zimetoka Tanzania Bara zimekuja hapa, wenzetu wamefanya vizuri tena hawa ni watu wenye mahitaji maalumu maana yake hii inaonekana wenzetu tunawatenga hata kama wakifanya vizuri. Hili sio jambo zuri sana mimi naomba sana hawa waitwe wapongezwe na kama sikupata maelezo mazuri ya Mhe. Waziri juu ya kupongezwa hawa wanamichezo wenye ulemavu wa akili basi mimi natishia kwenye fungu hili, kama hawajapongezwa hawa kama walivyopongezwa *Zanzibar Heroes* basi hatujatenda haki kwa wenzetu walemavu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika kulinda haki za wasanii. Wenzetu wamezungumza sana hapa juu ya wasanii wa zamani na mimi ninakiri sana hawa watu wanapaswa kuendelezwa, lakini nakuja katika kulinda kazi zao wasanii. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninajua kwamba kuna kitengo kichohusiana na hakimiliki lakini kuna wasanii ambao ni wa zamani, wengine wameshafariki wameshatangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awalaze pahala pema lakini wengine bado wapo. Lakini wengine bado hawajakuwa na uwelewa wa kuweza kuzisajili kazi zao na wengine

waliofariki hawakuwahi kuzisajili kazi zao. Kazi zao zinalindwa vipi. Ninataka Mhe. Waziri atueleze utaratibu unaotumika kuweza kulinda haki za wasanii.(*Makofi*)

Kwa mfano mimi nasikia sijui kama angalau huyu mwenzetu amepata chochote. Kuna nyimbo ile inayoitwa Subalkheri Mpenzi. Subalkheri Mpenzi ni nyimbo ambayo hivi sasa imepatia sana umaarufu sana Nandy na mwenyewe yupo nakumbuka mwenyewe nafikiri ni Mwapombe Khiyari. Sasa sijui kama kanufaika, natoa hiyo mifano labda Waziri aje atwambie sijui kama kanufaika, kwa sababu yule yeye imempamba jina na inampatia fedha nyingi. Sasa pamoja na haya kuna kikundi cha saana cha taifa, kuna kikundi cha *Culture*, tuna nyimbo zetu za asili ambazo wasanii waliimba mimi naomba tuwe na utaratibu wa kuwalindia kazi zao ili wasanii wasiweze kuzichukua kirahisi na wao zikawaopandishia chati. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie sasa katika suala zima la suala la kuendeleza na kukuza michezo na nije katika hivi viwanja vya wilaya. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana serikali na nimpongeze sana Mhe. Rais kuweza kufikiria kuweza kujenga viwanja vya michezo katika Wilaya na hivi sasa tayari Kiwanja cha Kitogani tunaambiwa katika awamu ya kwanza kiko tayari, wasi wasi wangu ni mmoja tu kwamba kile ni kiwanja cha *football*, sijui katika mipango ya kujenga viwanja vya Wilaya imeweza kuzingatia na michezo mengine kama iwe ipo pale, ingekuwa vizuri kama hiyo mipango haipo tukaona kwamba viwanja vile vya michezo vya Wilaya vinawekewa njia ya kukimbilia ili kuweza kukuza mchezo wa riadha katika Wilaya mbali mbali.

Lakini vile vile pembeni yake kuwa viwanja vya michezo mengine kama *volleyball*, *basketball*, pamoja na michezo kama ile midogo kama *netball* ambayo ni mchezo maarufu sana, kama vile viwanja vya michezo mengine havitoweka katika maeneo haya tunayosema viwanja vya Wilaya, itakuwa bado tuna pengo Fulani. Kwa hivyo kwa kile ambacho kiko awamu ya kwanza lakini hata na vyengine vitakavyojengwa kuweza kufikiria kuwa na eneo kubwa zaidi tusiwe na kiwanja cha *footbal*l tu, lakini pale pale pawe na kiwanja *volleyball, netball* pamoja na *basketball* ili kuweza kuhamasisha na vile vile vitasaidia Wizara ya Elimu pale wanapokuwa na mashindano ya kiwilaya.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikushukuru kwa nafasi uliyonipa hii na mimi kuweza kutoa michango yangu na kwa uwelewa wangu katika fani hizi za sanaa na michezo na niiombe sana serikali iweze kuyapokea yale ya ripoti ya kamati yote ni mazuri na ya wenzangu waliochangia na watakaochangia na niwaombe wengine wachangie na tuinge mkono. Lakini mimi ninaunga mkono kwa asilimia thamanini mpaka pale nitakapopata maelezo sahihi juu ya yale ambayo nimeyachangia.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana ahsante.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nassor Salim Jazira atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajiandae.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Vijana Utamaduni, Sanaa na Michezo na kwa kweli Mhe. ni hotuba nzuri nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hutuba yake nzuri na nimpongeze pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya katika kipindi kifupi hichi ambacho wamepewa jukumu hili. Lakini vile vile nimpongeze pia Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi ambayo kuwasaidia mawaziri wetu katika kutekeleza kazi za kila siku katika wizara hii.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kweli nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kazi nzuri anayoifanya katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kuinua sekta hii ya michezo kwa Zanzibar. Mhe. Rais wetu amefanya kazi kubwa sana. Mambo aliyofanya katika kipindi hichi cha kutekeleza ilani 2015/2020 ni kazi kubwa sana ni mambo mazuri sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wetu ameweza kutujengea upya uwanja wetu wa michezo wa *Mao tse Tung*. Kwa kweli ni faraja kubwa sana kwa Wazanzibari na Watanzania kwa jumla katika kuujenga upya uwanja ule ambao umo katika Jimbo la Kikwajuni. Mhe. Mwenyekiti, Jimbo la Kikwajuni unajua ni jimbo la asumini, kwa hivyo mambo mazuri mazuri yanakuja Kikwajuni na hata viongozi wazuri na mahahiri wako katika Jimbo la Kikwajuni. Lakini mbali na kujenga uwanja ule wa *Mao tse Tung* lakini Rais wetu ameweza kutujengea viwanja na mikakati mizuri ya kujenga viwanja kwa kila Wilaya. Kwa hivyo hii ni kazi nzuri ambayo anayoifanya Mheshimiwa wetu na tuna imani nae na tuna imani kwamba ifikapo 2020 viwanja vyote ambavyo vipo wilaya ambavyo vilipangwa kujengwa vitakuwa vimemalizika.

Lakini mbali na pongezi hizo Mhe. Mwenyekiti, na kazi nzuri uliyoifanya lakini tukumbuke kuwa katika vile vile Rais wetu huyo amefanya kazi kubwa katika kuboredha viwanja vyengine ambayo kuna kiwanja chetu cha michezo pale katika maeneo ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mwenyekiti, viwanja vile vilikuwa katika kipindi hichi cha masika ulikuwa huwezi kufanya shughuli zozote za machezo. Lakini sasa hivi, leo hivi nanavyozungumza hata mashindano ambayo yameandaliwa na Mhe. Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, leo yanaendelea katika viwanja vile vya Mnazi Mmoja, haya ndio mazuri ambayo Mheshimiwa kwa kweli tunastahili kumpa pongezi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mbali na kufanyia ukarabati nzuri ambao maji pale hayakai sasa hivi, niiombe serikali kupitia wizara husika na ninamuomba na nina imani sana na Mhe. Waziri ili kwamba katika viwanja vile vya Mnazi Mmoja kunajengwa viwanja japo viwili vya kisasa vya nyasi bandia. Mhe. Mwenyekiti, unapokwenda katika nchi za wenzetu wanakuwa wana viwanja vingi vya michezo na hasa unapoaanda mashindano ya kimataifa, timu zinapokuja hapa tunakuwa na mashindano makubwa ambayo yaandaliwa kila mwaka, mashindano ya *Mapinduzi Cup* ambayo kwa kweli mashindano yamekuwa na yamekuwa makubwa sana katika ukanda huu wa nchi za Afrika Mashariki.

Kwa hivyo inakuwa timu zetu zinapokuja katika mashindano yale wanakosa viwanja vya kufanyia mazoezi, lakini mbali na uwanja ule wa *Mao tse Tung,* lakini kama tutajenga viwanja viwili pale katika maeneo ya Mnazi Mmoja, uwanja ambao umetumia fedha nyingi katika

kuuboresha uwanja ule wa Mnazi Mmoja, tukajenga viwanja viwili tukajenga viwanja viwili. Nina imani kwamba soka la Zanzibar litazidi kukua na uwanja ule ni historia kwa sababu wana michezo wingi wakongwe wametumia uwanja ule wa Mnazi Mmoja, hata Dkt Shein Rais wetu mpendwa ametumia uwanja ule. Kwa hivyo nina imani kwamba Mhe. Waziri basi katika kipindi kitakachokuja tunajenga viwanja viwili vya nyasi bandia katika uwanja ule.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije katika sakata hili ambalo imeikumba nchi yetu ni kubwa la vijana wetu wa *Karume* B*oys.* Lakini kabla ya hapo Mhe. Mwenyekiti, mambo mazuri ambayo ameyafanya Mhe. Rais na ndio ikafika wakati vijana wetu wa *Zanzibar* Heroes walifanya vizuri kule mjini Nairobi katika mashindano yale ya Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika Nairobi. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mnadhimu wangu Mhe. Ali Salim pamoja na Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa kazi kubwa waliyoifanya kipindi kile, wakati timu yetu ile inakwenda katika mashindano kule nchini Nairobi, na nimpongeze sana Katibu wa Baraza la Michezo kaka yangu, mzee wangu maalim Khamis, kwa kweli anafanya kazi nzuri, anavyofanya jambo zuri mtu mpe ukweli.(*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mbali ya hao kuna wafadhili mbali mbali wamesaidia timu ile ya *Zanzibar Heroes* ikafanya vizuri, makampuni, serikali imefanya kazi nzuri. Jambo ambalo wamefanya vijana wale ni jambo kubwa tumpongeze sana Mhe. Rais kwa zawadi kubwa waliyoipa vijana wale, ni jambo la historia alilolifanya Mhe. Rais ni jambo kubwa na sisi ni wajibu wetu kulipongeza lile. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka katika uzuri ule ambao umeiletea sifa Zanzibar, tumepata aibu kubwa sana Zanzibar kupitia vijana wetu wa *Karume Boys.* Mhe. Mwenyekiti, jina la *Karume Boys* ni jina kubwa, ni jina ambalo lina historia kubwa na Mhe. Waziri jina hili limo katika damu yako na nina imani utalibeba hili utalifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba ile aibu tuliyoipata vijana wetu nchi yetu kupitia vijana hawa wa *Karume boys*,kupitia viongozi wao basi zinachukuliwa hatua ili kuona kwamba iwe fundisho kwa viongozi wengine wa vyama michezo ili kuondokana na aibu kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wa *Karume* B*oys* ambao walishiriki mashindano yale nchini Burundi, wa *under seventeen.* Mimi ninavyofahamu kwamba *under seventeen* ni *sixteen* kuja chini, hata unapokuwa unashiriki katika mashindano *under twenty o*ne inakuwa ni *under twenty* kuja chini. Sasa sakata hili ambalo limeikumba Zanzibar na Tanzania kwa jumla ni sakata kubwa na la aibu. Niombe serikali kwa kweli *ZFA* wametuia aibu kubwa. Kwa hivyo kwa yule ambaye amehusika naiomba serikali imchukulie hatua.

Mhe. Mwenyekiit, mimi nina imani kubwa wale ambao wamefanya kadhia hii mpaka ikafikia aibu, nadhani imetokana na tamaa zao kwa sababu Mhe. Rais ameyafanya mazuri. Sasa ninadhani ule uzuri ambao Mhe. Rais na zawadi kubwa alizozitoa kwa vijana wetu *Zanzibar* Heroes, basi pengine kuna wawili, watatu walifanya tamaa wakaingiza watu ambao hawastahiki kwenda katika safari ile. Lakin nina imani Mhe. Miraji Khamis Mussa ni kiongozi ambaye anapenda michezo, Mhe. Ali Salim ni kiongozi wetu Mnadhim katika Baraza hili kwa wana CCM, ni kiongozi ambaye anajitolea lakini Juzi tulizungumza na Mhe. Miraji Khamis Mussa,

nikamuuliza Mhe. Miraji Khamis kadhia ile vipi, akaniambia sina hata la kusema. Sasa Wazanzibari na Watanzania kwa jumla wanataka kujua kadhia ya tukio hili.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni baada ya kutokea tukio hilo Katibu Mkuu wa Wizara alitoa mwezi mmoja na akasema kwamba baada ya mwezi mmoja *ZFA* walete ripoti, lakini mpaka nazungumza leo mimi sijasikia ripoti ya *ZFA* kuhusiana na kadhia ile. Nasikia sijui wamekata rufaa sijui *CECAFA* sijui wapi. Sasa kama kuna rufaa au kama kuna majibu yoyote, basi naiomba wizara itupe majibu kuhusiana na kadhia hii. Nina imani sana na Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, lakini hili lazima mtupe majibu ambayo tutaridhika na tutaona kwamba kweli wale ambao wamehusika na kadhia hii wanachukuliwa hatua.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye wasanii. Wasanii wanafanyakazi kubwa na kazi kubwa wanayoifanya wenzangu wamezungumza Mhe. Salha Mohamed kazungumza na Mhe. Rashid Makame Shamsi kazungumza na ndio ikamfanya Mhe. Rais akamteuwa msani mkongwe mwenye hadhi kubwa, mzee wangu Mzee Chimbeni Kheir kuwa mshauri wa Rais katika masuala ya wasanii. Hongera sana Mzee Chimbeni. Lakini haya yote ya Mhe. Chimbeni yamezaa matunda mazuri zaidi kwa juhudi zake Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, kuna wasanii ambao wanaojengea sifa na wanatuletea sifa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna wasanii kina Issa Mussa ambaye kwa jina jengine anaitwa *Cloud*, ni msanii mzuri na ni msanii ambaye anaitangaza Tanzania na Zanzibar kwa jumla. Kuna msanii anaitwa Rashid Spider ni wasanii vijana ambao wanaitangaza Zanzibar, kuna msanii Abdalla Rahmim na yule anayeitwa Ray ni msanii mkubwa mbaye anaitangaza Zanzibar, kuna msanii Ussi Haji ni kijana mdogo. Kwa kweli nichukuwe fursa hii pia kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kumuwezesha kijana huyo kwa kushirikiana na viongozi wengine, ili kukuza kipaji chake, ni kijana ambaye ana kipaji kikubwa na nina imani kwamba atazidi kuitangaza Zanzibar kupitia sanaa.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna msanii anaitwa Mwinyimpeku. Mhe. Mwenyekiti, Mwinyimpeku amefanya usanii nje ya Baraza lako hili. Nilitoka hapo nje basi usanii alioufanya nikajua kweli huyu ni msanii, hongera sana Mwinyimpeku.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wasanii wana haki zao wanafanyakazi nzuri na wanaleta sifa kwa taifa. Lakini nichukuwe fursa hii kutoa pongezi kubwa sana kwa taasisi ya Hakimiliki kwa kulinda haki za wasanii. Nina ombi kupitia Wizara husika ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na wizara hii kulinda haki za wasanii. Mhe. Mwenyekiti, wasanii wetu wa Zanzibar wanafanyakazi nzuri, wanajenga heshima na yote haya kazi hii inatokana na uongozi bora wenye hekma, busara, mapenzi ya Rais wetu na viongozi wetu wa serikali. Chama cha Mapinduzi ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ipo katika kuwasaidia na kuwaendeleza wasanii. Kwa hivyo ni wajibu wetu sisi kuhakikisha tunalinda haki za wasanii.(*Makofi*)

Lakini pamoja na pongezi hizo Mhe. Mwenyekiti, naomba kugusia suala ambalo kwa kweli wasanii wetu wakongwe Mhe. Rashid Makame Shamsi kazungumza na Mhe. Salha Mohamed kazungumza. Kuna msanii Mhe. Mwenyekiti, alizungumza Mhe. Rashid Makame Shamsi hapa, wasanii wenzetu wa Tanzania Bara wanatumia sana nyimbo au sanaa za Wazanzibari au nyimbo

za Wazanzibari. Taarabu ya zamani kuna nyimbo ile inaitwa Subalkheir Mpenzi, pengine naweza nikazungumza hilo sio kwa nia nyengine, pengine salamu za Subalkheir Mpenzi naweza kumpa hata mke wangu aliyeko nyumbani. Kwa hivyo hata wewe Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo unaweza ukaitumia nyimbo ile ya kumsifu mke wako, ni nyimbo nzuri yenye mahaba na yenye hadhi nzuri. Nyimbo ile Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni nyimbo ambayo ina hadhi nzuri, inaleta hisia nyengine nzuri kwa kweli. Hata unapokuwepo nyumbani baada ya futari ukiisikiliza nyimbo ile baada ya kwisha kusali Tarawehe basi usingizi mnono unaupata.

Mhe. Mwenyekiti, sasa lakini msanii aliyeimba nyimbo ile au aliyeitunga nyimbo ile hajafaidika, wanaofaidika ni hao wengine. Kwa hivyo niombe wizara kuhakikisha kwamba je, kwa kupitia wimbo ule ambao umeimbwa upya, wasanii wetu ambao wameimba kwa kupitia *Club* ya *Culture Music Club* je, wamefaidika na nini. Nadhni Mhe. Waziri atakapokuja atatupa jibu hilo

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakukumbusha una dakika tano.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa wasanii hawa wa maigizo ambao kwa kweli niwapongeze na niwapongeze kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kukuza sanaa hii ya maigizo. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda unakwenda na wakati unakwisha, basi niseme tu bila ya kuwasahau wasanii wetu hawa ambao nimewataja mwanzo na itakuwa kosa kama kweli hatutawashukuru wasanii hawa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika hotuba hii kitabu hiki kimewataja wasanii wote, lakini wasanii wa kizazi kipya tumewasahau, na wasanii wa kizazi kipya kwa kweli tunawatumia katika nyanja mbali mbali. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri basi awaalike wasanii wa kizazi kipya wa Zanzibar ili aje akae nao ili kuweza kuendeleza sanaa yetu ya kizazi kipya kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Lakini vile vile yale mawili au matatu ambayo nimeyazungumza kwa sababu mimi ni mdau utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na nina imani na Mhe. Waziri. Kutokana na uongozi bora wa Mhe. Rais, nina imani kwamba Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri wake haya yote wanayafanya yale ya *Karume Boys* watayatolea majibu, ili kuhakikisha kwamba Wazanzibari wanapata jibu, na Mhe. Rashid Makame yupo atawasaidia ili kuweka mambo sawa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Nassor Salim Ali Jazira kwa mchango wako, Mwakilishi wa Kikwajuni, mwakilishi wa asumini. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kama muda utaruhusu basi Mhe. Hidaya Ali Makame ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuichangia bajeti ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi kidogo nacheka kwa sababu mwenyekiti ananichekesha yuko karibu. Najua hapa kama kutakuwa kuna makoseo makoseo kidogo ya mambo ya hesabu anaweza akaniwekea sawa.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataallah* aliyenijaalia uzima na afya na akatuwezesha kukutana hapa leo, ikiwa ni mara ya kwanza kuichangia wizara hii mpya. Pia sina budi kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuona kwamba upo umuhimu wa kuunda wizara mpya ya vijana, wizara ambayo aliitoa sehemu mbili kwa umahiri wake akachukua sehemu Wizara ya Kazi na Vijana, akachukua na kwenye michezo akaitengeneza ikawa ni wizara. Hili alilifanya akiamini kwamba Wizara hii ya Vijana ilikuwa ni kilio cha vijana kwa siku nyingi kwamba vijana ndio nguvu kazi ya taifa lolote ulimwenguni, akatilia maanani akaona sasa bora aanzishe hiyo wizara, na akampa Mhe. Balozi Ali Karume.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kumpongeza sana Rais kwa kumpa Mhe. Balozi Ali Karume kuwa Waziri wa wizara hii. Kwa hivyo ni imani yetu kwamba kwa mashirikiano yake ya karibu yaliopo na uzoefu alioupata Mhe. Naibu Waziri kwenye Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi basi wizara itakwenda kwa kasi sana. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba vijana wategemee mazuri ambayo walikuwa wakiyaomba kwa siku nyingi na dalili ya haya nimeyaona kwamba kwa upande wa bajeti wamewatengea karibu shilingi bilioni tatu, vijana washindwe wenyewe. Sasa mambo mazuri hayo yanakuja.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nizungumze sana michango yangu kwenye utekelezaji wa bajeti. Tuliona katika ukurasa wa 6 kwamba hawa wametenga shilingi milioni 500 mwaka jana kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya wilaya. Sasa mimi ningeomba sana aniambie atakapokuja waziri kwenye majumuisho yake kwamba na mara hii nimeona kidogo hizi pesa. Viwanja viliopo na idadi ya pesa zenyewe hazitoshi. Sasa sijui ana mkakati gani wa kuhakikisha angalau tunapata hivyo viwanja kwenye wilaya zetu, kwani vijana tunapojenga viwanja hivi katika wilaya basi ni moja katika jambo litakalotusaidia sisi kuendeleza michezo na kuibua vipaji mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, pia wenzangu wamechangia kwa kusema kwamba viwanja vinavyojengwa ni vya mchezo wa mpira wa miguu tu, hebu tujiulize hatuna michezo mengine. Kwa hivyo nitowe wito kwa wizara, kama ilivyoweka kipaumbele kwa mchezo wa mpira wa miguu, utowe pia kipaumbele kwa michezo mengine kama vile *netball*, *basketball*, *handball* na mengine *cricket*, ili vijana wetu waweze kuburudika zaidi na kuweza kushiriki kwenye michezo ya kimataifa na kuweza kutuletea heshima ya aina yake taifa letu. Kwa hivyo niliombe sana jambo hili kwamba pamoja na mambo mazuri, lakini bajeti hii ya shilingi milioni 500 iliyopatikana mwaka jana waje wanieleze Mhe. Mwenyekiti, kwamba ni viwanja gani na gani vimeanza kupata hizi pesa na hatua ya ujengaji wao umefikia wapi.

Pia Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima ambalo ningependa nilielezee na wenzangu wamelielezea kwa kina la usanii wetu. Wasanii popote wanajumuisha utamaduni wa nchi. Kwa hivyo ningeomba sana Mhe. Waziri utakapokuja uniambie mipango yako hasa uliyonayo, kwa sababu ya kurudisha ule utamaduni wetu wa Kizanzibari. Leo tulikuwa tumezowea wazee wetu waliotangulia tuliokuwa tunawaona sisi, walikuwa wewe mwenyewe huwezi kumuona mzee

anapita usiweze kumfuata ukampokea, ukamsalimia na mambo mengine, lakini leo tabia ile imepotea kabisa. Nataka uniambie kwa kupitia hili Baraza lako la Vijana, hawa vijina wamejipangaje kurudisha mila na silka za Uzanzibari hasa kwa kizazi chetu kipya kinachokuja, jambo ambalo linaonekana kwa sasa linapotea siku hadi siku. Jambo hili lilikuwa linatupa sisi utambulisho, ilikuwa ni utamaduni lakini pia ulikuwa ni utambulisho wetu. Popote mtoto wa Kizanzibari anapokwenda akionekana anajua kama hawezi kumpisha mzee hata awe wa mwenzake ni lazima atamsalimia, atakwenda kama ana mzigo anampokea na mambo mengine, lakini jambo lile leo limepotea.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na kupotea kwa lugha ya Kiswahili, yale maneno ya asili ya Kiswahili leo yamepotea taratibu yanaanza kutoweka. Jambo hili mim nalizungumza kila siku na ninakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja pia uniambie mkakati wako ulionao juu ya kukitunza na kuienzi hii lugha ya Kiswahili sasa hivi na kuweza kuyarejesha yale maneno ya asili ili watoto wetu wakaweza kuyajua. Kwa sababu leo mimi naamini kuna mambo mengi ambayo maneno watoto wetu hawayajui. Pengine ukimwambia kwa zamani anaona mageni, hii inatokana na kwamba watoto wetu sisi wenyewe hatukuwalea katika kuwafundisha maneno ya asili ambayo tumeyarithi sisi kutoka kwa wazazi wetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana na namuomba Mhe. Waziri uanzishe programu ya kukitunza Kiswahili hususan kwa kuyatumia yale mambo ya asili, maneno ya asili ni dhahabu, tukiwa nayo tutaweza kuyatunza na kuyaendeleza na yataweza kutunza mila, silka na utamaduni wetu wa Kizanzibari.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana juzi kutugaiya ile Kamusi nakupongeza kwa dhati kwa kugawa Kamusi ya Kiswahili. Watu wengi sasa wataweza kusoma kwa kupitia Kamusi ile na wakajua baadhi ya maneno ya Kiswahili, ambayo yalikuwa yameanza kupotea kidogo kidogo na mengine nimeyaona yamo. Kwa hivyo nichukuwe fursa hii kukupongeza sana kwa kuanzisha jambo hili.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kwenda kwenye suala la kujikita kwenye Mabaraza yao ya Vijana ambapo tulianzisha Mabaraza ya Vijana kwa madhumuni ya kuwakusanya vijana wetu kwa pamoja ili waweze kujiajiri na waweze kujiendeleza kwa namna mbali mbali. Leo nashukuru kwa sababu ya huo utekelezaji wa mpango wake, lakini nina tahadhari moja ambayo nataka niitowe kwamba sasa hivi vijana wengi wanaanza kukimbilia kwenye mambo ambayo hayana muelekeo. Kwa hivyo niwaombe sasa kwa kupitia Baraza hili la Vijana lililoanzishwa, tuanze utaratibu wa kushuka chini ili kuweza kuwatambua vijana wetu na kuweza kuwapatia elimu ya huo ujasiriamali na mambo mengine na kuweza kujiweka pamoja jambo ambalo litatusaidia sana kwenye Baraza la Vijana na liwezeshwe.

Mhe. Mwenyekiti, leo ukisoma kwenye maelezo yao wanasema Programu ya Vijana, kuimarisha huduma za ustawi ndani ya Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana, iliyokuwa ikitekelezwa chini ya wizara hiyo, walipangiwa shilingi milioni 427, mara hii wamepangiwa shilingi milioni mia nne kama na hamsini na kidogo hivi, pesa ambazo ni kidogo sana, tukitilia maanani kwamba vijana ndio taifa la kesho na ndio nguvu kazi ya taifa na pia wapo wengi kiwilaya. Sasa shilingi milioni 457 ukizigawa kwa wilaya zetu wastani sijui wa kiasi gani kwa kila wilaya tunaweza kupata, kwa sababu Mheshimiwa utanisaidia tuna wilaya ngapi karibia 11. Hebu ziangalie wilaya hizi tulizonazo tukizigawa pesa hizi utakuta vijana sawa sawa, mimi naomba sana kwamba

kwenye Mabaraza ya Vijana yaongezewe bajeti ili kuyawezesha haya Mabaraza yaweze kufanya kazi zake vizuri. Kufanya hivyo Mhe. Mwenyekiti, kutatusaidia kuweza kutoa hayo yote ya ajira, wataweza kujiajiri, elimu wataweza kupata na mambo mengine wataweza kujiendeleza. Lakini kama tutaendelea na hili basi tutakuja kuwalaumu watendaji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mwengine nayachukua haya kwenye utendaji wa ofisi Pemba. Leo ukiangalia Pemba katika jadweli lao wamesema kwamba wameipatia Ofisi Kuu Pemba, mwenzangu Mhe. Rashid Makame amesema shilingi milioni 110 ambayo imewezeshwa wamepangiwa kwa ajili ya kazi za uendeshaji wa ofisi. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili mimi nataka niombe sana kwamba hebu aiangalie tena Wizara kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba shs.110,000,000 ni pesa ndogo sana, iko haja ya kuwaongezea bajeti angalau wende shs.150,000,000 waweze kufurukuta furukuta kidogo, na mimi nimepaona naona kuna Idara ya Mipango Sera na Utafiti wamewekewa shs.152,000,000, Idara ya Utumishi na Uendeshaji na matumizi mengine shs. 842,000,000 kwenye jumla hiyo. Sasa mimi naomba kwa sababu hizi idara ambazo zipo Unguja na Pemba zipo, kwenye mfumo huo huo, waongezewe tujikasim, kasim kidogo kidogo tuweze kuwaongezea na hawa kwa upande wa Afisi Kuu Pemba ili waweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Hii Wizara inadili na Vijana lazima washuke chini, lazima waitishe vikao, lazima waratibu kila kitu, tutakaposhindwa kuwaongezea hawa bajeti yao tutakuja kuwalaumu mwisho. Mimi sioni vizuri kulaumiana watu wazima hawalaumiani, sisi sote watu wazima tuna maarifa, tuna busara. Kwa hivyo nikuombe tu Mhe. Waziri ile Ofisi yako iliyepo Pemba uiangalie kwa jicho jengine la huruma uwaongezee wale kidogo, umege mege upande mwengine, uwaongezee wale waweze kutekeleza majukumu yao ya kazi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nilitaka nilichangie katika hotuba hii ni suala zima la vyombo vya habari ambavyo vinasemekana vipo katika ukurasa wa 23 kwamba, naanza ukurasa wa 22 naomba kunukuu anasema, "wabunifu wasanii, wagonjwa 33 wamefikiwa kwa maeneo ya Unguja na Pemba lakini kuna changamoto jumla ya shs.300,300,000 zilitumika kwa shughuli hiyo hata hivyo bado kuna changamoto ya muitikio mdogo wa ulipaji wa mirabaha na heshimu haki za matumizi za haki miliki za kibiashara*"* na vikatajwa baadhi vikatajwa baadhi ya vyombo hapo ambavyo vinaonekana kama ni changamoto wakavitaja vikiwemo *ZBC TV, Radio, TV Coconut Radio* sijui, *ZENJ FM, BOMBA FM, BAHARI FM* pamoja na vyombo vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili nakuommba sana kwamba liangaliwe kwa namna yake na hivi vyombo vinavyohusika viwajibike kwa namna yake, hatuvisemi vibaya, ni vyombo vinafanyakazi ya kuelimisha, wanaelimisha jamii, jamii yetu inapata elimu, inapata kujua, inapata uelewa, lakini mihimili hii au vitu hivi au vyombo vyote vinakuwa vitegemeane kwa kulipiana ada mbali mbali ili viweze kujiendesha. Sasa ushauri wangu kwa jambo hili juu ya suala hili ni kwamba kupitia wizara yako na Wizara ya Habari zikae pamoja kuliangalia namna gani hivi vyombo viweze kufanya marejesho ya hizo pesa, wanaodaiwa waweze kulipa ili na hii wizara nayo waweze kujiendesha kinamna yake.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya habari si kitu cha kukitilia mdomo mimi naviheshimu na wenzangu wote najua ni hivyo, lakini niwaombe sana wamiliki wa vyombo hivi wachukulie

uzito wa aina yake kwa kurejesha marejesho haya ambayo wanadaiwa kwa sababu wao wanafanyakazi kibiashara, hawafanyi kazi kwa kujitolea, kwa nini wakashindwa kulipa madeni ambayo yanawakabili.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mwisho Hakimiliki kwa wasanii wetu. Mhe. Mwenyekiti, na mimi naungana na Mhe. Nassor Ali Salim Jazira aliposema kama sisi Zanzibar tuna hazina ya vipaji hasa vya usanii. Niombe sana sana kwamba wale wasanii wetu wakongwe, yeye kawataja hao, kuna wengi ilikuwa ni vyema ukaanzishwa utaratibu angalau wa kwenda kuwaona wale na kupitia wizara yako Mheshimiwa, ukapanga utaratibu angalau wa kuwapatia cho chote wale ili na wao wakajisikia kama wametoa mchango katika taifa lao na bado kwamba taifa lao linawathamini. Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo wale wasanii tutafika pahala watu wataiba zile nyimbo zao watazitumia na wao wenyewe wataendele kubakia hivyo hivyo maskini. Leo mazuri yote hawa wasanii wote waliopo tunawasikia wametokana na hawa walio tangulia.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nitowe wito hilo na pia kupitia huu utamaduni wetu kwenye sanaa, wasanii waitumie fursa yao walivyonayo na vipaji vyao walivyonavyo kuelezea na kuitangaza Zanzibar sio kuibomoa. Kwa sababu moja katika kitu ambacho nampongeza sana Rais John Pombe Magufuli, wakati akizindua kule Dodoma ni kulitaja tatizo la mavazi, kuvaa mavazi yasiyostahiki kwa wasanii wetu. Jambo hili kwetu siye linatuondoa katika mila yetu ya asili inatupeleka katika mila za nchi nyengine ambazo sisi hatukurithi kutoka kwa wazazi wetu. Mhe. Mwenyekiti, nitoe wito kupitia kwa wizara yako kuwataka wasanii waitangaze Zanzibar kupitia usanii wao, kupitia vipaji vyao walivyo navyo lakini pia waelewe kwamba wana jukumu pia la kulinda mila na silka na desturi ya Kizanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima mimi naunga mkono hoja hii, sina pingamizi nayo lakini Mhe. Waziri utakapokuja uje unijibu kidogo hayo mambo yangu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid ninakushukuru kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kama muda utaruhusu basi Mhe. Hidaya Ali Makame ajiande.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana, Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi nikaachangia hotuba ya Wizara ya Vijana, Utamaduni na Sanaa na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba katika taasisi hii mpya, kwa sababu taasisi ikawa mpya, Waziri mpya, Naibu Waziri mpya, Katibu Mkuu mpya, nawapongeza wote najua kazi itafanyika kweli. Na naamini sina shaka nao hususan kwa Katibu ambaye aliyekuwepo pale.

Mhe. Mwenyekiti, na nikiendelea mbele katika mchango wangu bora niende moja kwa moja niende katika ukurasa wa 11, walisemea kuhusu vikundi vya vijana. Kama unavyofahamu kwanza vikundi vya vijana vimetoka kwenye Mabaraza ya Vijana vilivyoandaliwa rasmi kwa

sheria kabisa iliyopitishwsa humu Barazani, lakini bado kuna malalamiko vijana wale hatujaweza kuwatumia ipasavyo. Tumetunga tu kama wawepo lakini kuwatumia kama *incubator* kwa kuzalisha vijana ambao watakuwa *competent* katika shughuli zetu mbali mbali mbali bado, na imekuwa bado imekuwa bado kutokana na bajeti yenyewe ilivyokuwa mwaka jana ni ya shs.100,000,000. Kwa hivyo, shs.100,000,000 nafikiri huwezi kuendesha kitu na tumeona mpaka dakika hii robo ya tatu imeshakwenda ni asilimia 63 nafikiria wamepata ni pesa ndogo sana katika masuala mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikiendelea mbele hapa wamesema hapa katika ukurasa huo huo. Idara imeweza kusaidia vikundi vya vijana Unguja na Pemba kuvipatia mashine za maji, vyerahani, mipira ni vikundi 9, vikundi 9 ni vidogo sana. Ingependeza zaidi tungetajiwa ni vikundi vipi. Kwa sababu mara nyingi sana tunaambiwa hata tukiuliza masuala yetu, tunaambiwa tumesaidia 20, vikundi 30 lakini *specific* ni vikundi vipi, tusiandikiwe nambari tu, tuandikiwe vikundi, tujuwe hichi kimesaidiwa ili tupate nguvu ya kuuliza. Je, ni kweli kwa sababu wizarani kule au Barazani mumeambiwa nyinyi mumesaidiwa, lakini kimefungwa hatujui kikundi gani na gani ambacho kilichosaidiwa. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tu Mhe. Waziri unakapokuja hivi vikundi 9 mlivyovisaidia *pump* za maji, vyerahani na vifaa vyengine vya kilimo ni vikundi vipi, vikundi tisa ni kidogo tu kutaja haifiki hata dakika tano umeshamaliza. Ningeomba uje unitajie vikundi hivi ulivyovisaidia vikundi hivi ulivyovisaidia vifaa vya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele vile vile katika ukurasa wa 38 wa kitabu hichi nimeona vipaumbele vya wizara, kuna moja ya kuandaa programu kuwezesha vijana kiuchumi na kuajiri, kufanya tafiti katika maeneo ya vijana utamaduni, sanaa na michezo. Ni kweli, nakubaliana nalo kabisa vipaumbele na sote tunaamini kwamba michezo pamoja na kuwa ni *entertainment,* lakini ni sehemu ya ajira kwa vijana wetu. Ili kwa upande huu hatujaifanyia kazi ipasavyo lakini kama tungeifanyia kazi ipasavyo ili suala la sanaa na michezo basi nafikifri haya tunayozungumza sasa hivi hapa tusingeweza kuzungumza tungelizungumza lugha nyengine kwamba vijana wangapi wamefaidika katika hayo mbali mbali, lakini utaona kwamba tunashindwa, unakuta tumekosa kidogo kama dira ya michezo namna gani tunataka katika michezo yetu tunashindwa kulitumilia.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliopita wamesifu tu wasanii hapa mbali mbali ambao wapo kweli hapo juu tunawaona, wapo kina Ray, Mwinyichande, akina *Spider* na wengineo, wapo wengi sana ni kundi kubwa ambalo limejiajiri, ajira ambazo zisizo rasmi. Lakini kama ajira zile hii sanaa ingepewa kipaumbele kabisa nafikiri leo hii tungekuwa tunapata hata kodi ya kutosha katika wasanii hawa. Lakini tunashindwa sasa hivi kupata kodi kwa wasanii hawa hata kuchangia kwa taifa lao baada ya wao kujikidhi wenyewe.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana wizara hii, naamini kwamba ni watendaji wazuri kwenye fani zote basi waangalie hawa wasanii kuwapa kipaumbele, kuona kwamba kuondosha pale walipo sasa hivi iko katika *moderation* gani waliyoitaka ya sanaa ambayo itakuwa inatuingizia na sie kama serikali. Ningeomba sana nizungumze suala kama hilo.

Lakini vile vile nikienda mbele nizungumze suala zima la Baraza michezo. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana hapa tulipiga kelele sote kwenye bajeti ya Baraza la Michezo shilingi milioni thamanini naa., tukasema Baraza la Michezo ina vyama vingi. Kweli milioni hizi thamanini na

nne sijui zitatosheleza, wakati unaambiwa kuandaa timu ya taifa tu peke yake ukiepeleka Kenya na kurudi imetumia zaidi ya shs.120,000,000. Lakini bajeti ya Baraza la Michezo ambayo ni Chama ni mtoto wa Baraza la Michezo, mwenyewe baba ana bajeti ya shs.80,000,000 bila ya kuwa na nguvu ya serikali hatuwezi kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nishukuru na niipongeze sana serikali kwa kusaidia pamoja na wafadhili mbali mbali waliojitokeza toka kuweka kambi timu yetu ya taifa na mpaka kwenda kwenye mashindano yale kuchukua nafasi ya pili. Kwa kweli tulifarijika sana tulipoona namna gani Waziri aliyekuwa anahudumu katika Wizara ile wakati ule kwamba alikuwa anafanya kila njia, kila mbinu kuona kwamba vijana wale kule Kenya hawapati shida ni kweli, ni kwa mara ya kwanza angalau wachezaji kutoka Zanzibar wameweza kupata posho alau ya Dola 500 kwenda Kenya katika mashindano haijawahi kutokea.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri aliyekuwa katika wizara hiyo basi naomba Mhe. Ali Karume urithi ya mazuri aliyokuwa nayo Mhe. Rashid Ali Juma kwa wakati ule ambayo vijana wale walikwenda kwa nia safi kidogo wakapeperusha bendera nzuri ya taifa na wakawa na ari na moyo mkubwa sana mpaka kuchukua nafasi ya pili na ikawa faraja kwa Zanzibar. Kwa kweli Zanzibar ilisimama ni kwa sababu ya mpira. Mpira au *soccer* ni katika mchezo ambao yenye kundi kubwa sana la vijana linaloajiri au linalipa vizuri basi mpira haitokei wanne duniani, ukiondoa *basketball, American soccer, football* imo na ndio mana ukakuta wachezaji wa mpira duniani wanalipwa pesa nyingi, lakini kwetu sisi hatujafikia huko kutokana na kuwa tumekosa sera nzuri au tumekosa mambo mazuri au kiongozi mzuri wa kusimamia mpira.

Mhe. Mwenyekiti, sisi sote humu tunaosimamia ni wadau wa michezo na tunaona namna gani, michezo kwa upande mpira wa miguu unavyoendeshwa katika nchi yetu ya Unguja, imekuwa ni kilio baada ya kuwa ni faida. Tunashuhudia kwamba mchezo wa mpira Zanzibar ni hasara, ukiondoa vilabu vya serikali yaani vilabu vya vikosi, yaani vilabu vya vikosi, timu za uraiani zote, timu za mitaani, haziwezi ku-*struggle* katika ligi hata ukipimo ukiangalia kwamba timu zote zilizoshuka daraja mwaka huu ni timu za uraiani, kwa sababu hawana nguvu na kwa sababu hatuna mdhamini na kwa sababu uendeshwaji wa ubabaishaji wa Chama cha Mpira *ZFA.*

Mhe. Mwenyekiti, nyinyi nyote ni mashahidi mpaka dakika hii *ZFA* kuna mgogoro si mdogo. Mhe. Waziri nafikiri utakumbuka kwamba turithi wenzetu Kenya waliwahi mpaka kuvunja Chama cha Mpira, ijapokuwa walisimamishwa kushiriki katika mashindano ya *CAF*. Hata nafikiri na Burundi vile vile lakini sisi Zanzibar sio wanachama wa *CAF* wala *FIFA,* tunakwenda katika wanachama wa *CAF* kwa mgongo wa Tanzania Bara. Nafikiri kuna haja katika ku- *modify ZFA* mpya. Ninafikiri ingevunjwa *ZFA* ile pale wakaandaa Katiba mpya na kuweza kutafuta watu wenye uwezo wa kuendesha mpira nchi hii ukaendeshwa, kuliko sasa hivi kila kukicha malumbano tu, kambi hii na kambi hii au mpira uchezwe huku mpira uchezwe huku hatuwezi kufika, imekuwa tatizo katika mpira wa Zanzibar ukiongozwa na Chama cha Mpira wenyewe wa *ZFA.*

Mhe. Mwenyekiti, nimethubutu kusema hayo kwa sababu nayajua, nakumbana nayo siku hadi siku. Leo hii imefika hatua hata watendaji Rais na Katibu basi hawakai wakazungumza lugha moja mpira tunaupeleka wapi. Je, tutacheza kweli mpira, ikiwa hawa wasimamizi ambao

wanawasimamia wachezaji mpira imefika hatua kama hiyo, mmoja anakwenda Kusini na mwengine anakwenda Kaskazini, hatuwezi kucheza mpira katika hali kama hiyo. Huko nje kuna watu wanachochea *ZFA* iondoke ije nyengine, hatuwezi kwenda ni lazima tutowe maamuzi magumu.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwa nchi za wenzetu vyama kama hivi vya mpira. Mhe. Mwenyekiti, nitakupa mfano kama nchi ya Morocco. Nchi ya Morocco *footballFfederation* yake nafikiri inaongozwa na *CAG*, Mkaguzi Mdhibiti Mkuu wa Serikali wa Morocco ndio Rais wa Chama cha Mpira wa Morocco. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Burundi inaongozwa na Spika wa Bunge au Baraza la Burundi. Lakini ukiangalia Rwanda inaongozwa na *Major General* wa Jeshi, nini maana yake. Kwa sababu lazima apatikane mtu mwenye uwezo na mwenye ushawishi kwa pande zote, kwa upande wa serikali na huku kwenye michezo ili aweze kuzungumza lugha nzuri kuona namna gani ataweza kuisaidia michezo yetu au mpira wetu. Lakini kwa mwenendo wa sasa hivi na kwa Katiba iliyokuwepo Zanzibar, tusitegemee kupata kiongozi mzuri wa kuendesha mpira wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Tanzania Bara walikuwa na kadhia kama hii lakini walikaa wale wachezaji wa zamani wakasema aah, mpira unakokwenda siko tuandae *program.* Basi walifanikiwa na nafikiri wakamuandaa Leodergan Tenga kuwa Rais wa Chama cha Mpira na wakampigia kura na akaja kuwa Rais wa mpira wa Tanzania, tumeona. Tunaondoka katika zogo la akina Ndolanga na yule mwengine, tukaona Tanzania inaanza kuondoka zake. Mhe. Mwenyekiti, hata juzi tu baada ya vurumai hili tumeona waliokuwepo wale walikuwa na kashfa za wizi, walifunguliwa kesi na wapo ndani mpaka dakika hii hawajajua hatma yao, yupo Karia anaongoza mpira kila mmoja anaridhika kwa uwazi uliokuwepo pale juu ya matumizi ya fedha na uongozi wenyewe. Kwa nini Zanzibar tushindwe.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri hili suala la *ZFA* aliangalie kwa kina ili mpira uchezwe, Wazanzibari wanapenda mpira. Kama unaamini kwamba siku tulipocheza *final* ya Kenya na timu ya Taifa ya Zanzibar, basi Zanzibar ilisimama na watu walirindima kwa ushindi ule na hata mapokezi yalikuwa makubwa, kwa sababu watu wanapenda mpira lakini viongozi wa mpira hawataki mpira uchezwe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri aliangalie kwa kina, najua hujashuka zaidi huku umeingia sana kwenye Mabaraza tu. Ningekuomba sana uingie kwenye *ZFA* tumekosea wapi, tuondoke pale ili tuone mpira uchezwe na ili iwe ni ajira kwa wachezaji wa mpira wetu isionekana kwamba vilabu vya taasisi za ulinzi tu peke yake au vilabu vya vikosi viwe vinafanya vizuri na vilabu hivi vya uraiani ambavyo ndivyo vilabu vyenye watu wengi sana vikakosa kufanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kama mimi ningekuwa ndio kiongozi wa mpira, basi nisingekubali hata siku moja kuona kwamba timu kama Taifa ya Jangómbe inashuka. Sisemi kwa sababu Taifa ya Jangómbe ina jina la jimbo langu hapana, ndio klabu ambazo zimeweza ku-*stimulate* mpira wa nchi hii, mpira wa nchi hii ulielekea kuzimu. Lakini baada ya kupanda daraja timu zile ikawa Taifa ya Jangómbe na timu ya *Jang'ombe Boys*, sisi sote tulikuwa ni mashahidi kwenda kuangalia mpira na uwanja ulikuwa unajaa, tukarudisha kule kwenye miaka ya zamani

ya kuangalia Small Simba, Miembeni, Malindi na vilabu vyengine. Sasa hivi kile kilabu kimoja kimeshuka kutokana na mambo tu changamoto hizi tulizozungumza za *ZFA*, ambapo tumepoteza *icon* moja ya Taifa ya Jangómbe na kufanya tupunguze washabiki katika viwanja vyetu. Ningeendelea kukuomba Mheshimiwa kwamba lazima uchukuwe maamuzi magumu tuone namna gani tunausaidia mpira wetu sisi.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nikiendelea mbele kuna michezo mingi, nimeganda sana kwenye mpira, kuna mchezo wa *badminton*. Hii *badminton* hata baadhi ya watu wengine ukiwauliza hawajui mpira gani huu, *badminton* lakini upo unachezwa na baada ya kuondoka Baraza la Wawakilishi pale watapelekwa Skuli ya Ben-Bella pale. Kuna changamoto katika ule uwanja waliopewa Skuli ya Ben-Bella kucheza mchezo huu wa *badminton* kuna changamoto zake.

Mhe. Mwenyekiti, ni mchezo ambao umeipatia sifa nyingi sana Zanzibar. Nyinyi nyote mnakumbuka pale Kikwajuni familia ya kina Nasra Juma ambao ndio walikuwa wachezaji wakubwa *badminton* katika Zanzibar hii na wameshiriki mashindano mbali mbali ya Afrika, wamelipa sifa kubwa katika nchi hii. Lakini leo huu hauna nafasi hauzungumzwi mchezo ule wa *badminton*. Sasa hivi wanacheza Ben-Bella pale lakini mara wanaambiwa hili ni darasa msicheze mara hivi, namna gani. Lazima serikali tujipange kuona namna gani tunaisaidia michezo hii ya *badminton*. Hivi karibuni walifika hata kukabidhiwa vifaa na Mhe. Rais wa nchi hii. Je, vile vifaa wafanyie nini bila ya kupata kiwanja cha kuchezea mchezo ule. Ningeomba sana Mhe. Waziri hilo uliangalie na pengine umejipangaje kuangalia mchezo wa *badminton* katika Zanzibar.

Lakini pia kuna mchezo wa *Squash* vile vile *Indoor game* zote zilizokuwa zinailetea sifa sana Zanzibar. Tunajua wachezaji *Squash* maarufu hapa Zanzibar, akina Nadir Mahfoudh, wapo aliyekuwa Naibu Gavana ni wachezaji *Squash* wazuri sana, lakini wanakosa, ukiondoa sasa hivi katika kiwanja cha Polisi Ziwani hakuna kiwanja chengine na wakati zamani walikuwa mpaka Hoteli ya Bwawani walikuwa wanacheza. Sasa tungeomba na hii michezo ya ndani pengine nadhani katika michezo ya *Indoor game* katika uwanja huo mpya na haya yatakuwepo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kilio changu nakileta tena kwako Mhe. Waziri, bajeti iliyopita ya Wizara hii nililalamikia sana Chama cha Wainua Vitu Vizito, (*Zanzibar Weighting lift)* ni chama pekee cha michezo katika Zanzibar hii chenye kushiriki au chenye uwakilishi wa Kimataifa, tokea 1964 wale wapo katika Shirikisho la Dunia la Wainua Vitu Vizito, wamekuwa na kilio cha muda mrefu sana. Niseme kwamba eti wanadaiwa ada ya uwanachama dola 400 mpaka dakika hii bado. Nilimwambia Mhe. Rashid lakini ikawa bado hakuna kilichofanyika. Nasema tena hii katika Chama kile Cha Wainua Vitu Vizito, ni chama ambacho kilituletea sifa kubwa sana Zanzibar, walikuwepo kila Marwa, Magwa na wengineo ambao walikuwa wakiinua vitu vizito nchi hii na wameleta sifa nyingi tu na walikuwa wanashinda.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kustaajabisha kwamba tunataka kwenda mbele wakati haya tuliyokuwa nayo ya zamani hatuwezi kuyatunza, tunaangalia kutafuta *FIFA* na *CAF*, lakini leo hii kuwasaidia hawa watu wainua vitu vizito dola 400 ya uwakilishi ya uwanachama wao katika vyama vya Dunia tunashindwa, tutegemee nini. Ningeomba sana Mhe. Waziri katika hicho

ulichukue na uje na suala zuri sana juu ya kadhia hii iliyokuwepo katika suala hili la Wainua vizito.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende katika suala zima la Uwanja wa Amani. Suala la Uwanja wa Amani na sisi sote ni wadau baadhi yetu tunakwenda mpirani mara kwa mara na kumekuwa kama kuna ubaguzi wa utumiaji wa vifaa pale Uwanja wa Amani. Mimi nathubutu kusema haya pindi tunapokwenda kuangalia mechi kuna bao la matokeo, lakini bao lile kama hazichezi baadhi ya timu nafikiri timu nyengine haziwashiwi. Kuwashwa ukaona matokeo ukiingia unaona matokeo yapo moja moja au mbili mbili, lakini baadhi ya timu zikichezwa linakuwa linawashwa. Tatizo nini. Je, linabaguliwa kwa watu maalum ndio wenye mamlaka ya kutumia vitu vile au timu zote za Zanzibar zina haki kutumia chombo kile. Limekuwa ni tatizo la muda mrefu, ukiuliza unaambiwa limeharibika lakini siku ikicheza timu nyengine linafanya kazi. Naomba Mhe. Waziri ukija ulijibu swali hilo tatizo la *scoreboard* la Uwanja wa Amani ni nini, uwendeshaji au pengine ufundi, *technician* ni matatizo na mengineyo, nitaomba sana unisaidie katika hilo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea mbele niende katika suala zima la Baraza la Michezo. Nampongeza sana Mhe. Rais kwa kuchagua Mwenyekiti mpya wa Baraza la Michezo, Kocha Gulamu Abdalla lakini cha kusikitisha hadi leo hii hakuna kilichofanyika tokea lile Baraza limechaguliwa. Inavyosemekana maelewano ya watu hawa watendaji wa juu hayapo mazuri, hawawezi kukaa meza moja wakazungumza. Sasa katika hali kama hiyo hatuwezi kutegemea kwamba michezo nchi hii itakuwa. Nakutegemea sana *your diplomacy*, unajua kila kitu kuhusu masuala hayo, utumie diplomasia yako kuona ni namna gani hawa viongozi wanakaa pamoja, wanazungumza ili kama kuna changamoto zao wanaziweka pembeni wanakuja na uzalendo kuona kwamba michezo Zanzibar inachezwa na kung'arisha nchi yetu katika nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na mambo mengi sana ambayo hayazungumziki katika watu wale. Kwa hivyo ndio maana ukaona Katibu yupo kwake, Mwenyekiti yupo kwake, chama kimekaa tu, hata siku moja tokea kuwekwa kukaa kikao wakazungumza hakijafanyika, inafika zaidi ya miezi minne, miezi mitano sasa hivi tokea kuchaguliwa Mwenyekiti yule wa Baraza la Michezo, sijui tatizo nini na pengine kwenye kalenda yao ya vikao ipo vipi, imefuatwa au haijafuatwa, hilo siwezi kulijua nilitaka liseme hilo tu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote hayo lazima tuwapongeze sana wazee wetu, wasanii wetu wa zamani mbali mbali ambao walioichukua sanaa mpaka ikafika hapa sasa hivi ambao sisi wajukuu wao au watoto zao tunaendelea kuwa nayo. Tutakuwa wachoyo wa fadhila sana bila ya kuwashukuru wao walipoteza nguvu zao kubwa sana akina Mwalimu Iddi Farahani na wengineo, akina Seif Salum, Maulid Machaprala, akina Khamis Shehe, tumeona katika fani ya muziki ya taarab Zanzibar. Mpaka sasa hivi basi bado watu wanahamu kusikia ile *old is gold* za taarab, nyimbo za zamani, kwa sababu ni nzuri, zina mafumbo mazuri, zina maudhui mazuri, zimeficha mambo mengi, tofauti na nyimbo zinazoimbwa sasa hivi ambazo zipo wazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kuna Baraza la Sensa la muziki nafikiri ziangalie nyimbo zinazoimbwa katika vikundi vyetu vya sanaa, zimekuwa nyingi zinatoka na maudhui mazuri au mambo mengi yapo wazi wazi hawajabana bana kama zamani. Zamani unaambiwa asiyekula

nanasi hajala kitu kitumu, unajiuliza nanasi hili lakini ukiangalia kumbe kuna kitu kimekusudiwa lakini kimefichwa, mpaka utumie sanaa na wewe ujuwe nanasi lililokusudiwa hapa lipi. Kunguru ndege laghai, kunguru gani, kunguru huyu. Kuna mambo mengi tu lakini sasa hivi mara akwambie mke wangu kikojozi, mara hatandiki, hatuwezi kufika.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nasema ahsante sana. Siungi mkono hoja namsubiri Mhe. Waziri atakapokuja kunijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe tumebakiwa na dakika kama 10 kama sikosei na nilimtaja Mchangiaji Mhe. Hidaya Ali Makame lakini dakika hizo anasema hazitomtosha hasa ukizingatia Wizara hii inamuhusu yeye ni kijana na kaja humu kwa nafasi za vijana. Kwa hivyo anataka aiongelee ipasavyo, hivyo ananambia dakika 10 hazitomtosha. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha nitataja wachangiaji wa mwanzo kesho tukijaaliwa akiwemo yeye wa kwanza Mhe. Hidaya Ali Makame, atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na wa tatu atakuwa ni Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa utulivu wenu na pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Wizara hii kwa uwasilishaji wake, pamoja na Mwenyekiti, wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, na Waheshimiwa wote wale waliopata nafasi kwa siku ya leo kuchangia nawashukuru sana na watakia Ramadhani njema na futari njema, Inshallah.

Naomba niakhirishe Kikao hiki mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 8:45 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 29/5/2018 saa 3:00 Asubuhi)